ORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

MHE. PANDU AMEIR KIFICHO - SPIKA

1.Mhe. Balozi Seif Ali Iddi	MBM/Makamo wa Pili wa Rais/Kuteuliwa na Rais
2.Mhe. Dr. Mwinyihaji Makame Mwadini	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi/Jimbo la Dimani.
3.Mhe. Omar Yussuf Mzee	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo/ Kuteuliwa na Rais
4.Mhe. Haji Omar Kheri	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Utumishi wa Umma na Utawala Bora/Jimbo la Tumbatu
5.Mhe. Fatma Abdulhabib Fereji	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais/Kuteuliwa
6.Mhe. Mohammed Aboud Mohammed	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamo wa Pili wa Rais/Kuteuliwa
7.Mhe. Abubakar Khamis Bakary	MBM/Waziri wa Katiba na Sheria/Jimbo la Mgogoni.
8.Mhe. Hamad Masoud Hamad	MBM/Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Jimbo la Ole.
9.Mhe. Ramadhan Abdalla Shaaban	MBM/Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Kuteuliwa
10.Mhe. Juma Duni Haji	MBM/Waziri wa Afya/Kuteuliwa

11.Mhe. Zainab Omar Mohammed	MBM/Waziri wa Ustawi wa Jamii na Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto/Kuteuliwa
12.Mhe. Abdillah Jihad Hassan	MBM/Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo/Jimbo la Magogoni
13.Mhe. Ali Juma Shamuhuna	MBM/Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati/Jimbo la Donge.
14.Mhe. Mansoor Yussuf Himid	MBM/Waziri wa Kilimo na Maliasili/Jimbo la Kiembesamaki
15.Mhe. Nassor Ahmed Mazrui	MBM/Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko/Jimbo la Mtoni
16.Mhe. Said Ali Mbarouk	MBM/Waziri wa Mifugo na Uvuvi/Jimbo la Gando
17.Mhe. Haroun Ali Suleiman	MBM/Waziri wa Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika/Jimbo la MaMakunduchi
18.Mhe. Suleiman Othman Nyanga	MBM/Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Jang'ombe
19. Mhe. Haji Faki Shaali	MBM/ Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Mkanyageni
20.Mhe. Machano Othman Said	MBM/Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Chumbuni.

21.Mhe. Omar Othman Makungu	Mwanasheria Mkuu
22.Mhe. Issa Haji Ussi	Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Jimbo la Chwaka
23.Mhe. Zahra Ali Hamad	Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Nafasi za Wanawake
24.Mhe. Dr. Sira Ubwa Mamboya	Naibu Waziri wa Afya/Kuteuliwa na Rais
25.Mhe. Bihindi Hamad Khamis	Naibu Waziri wa Habari,Utamaduni,Utalii na Michezo/ Nafasi za Wanawake
26.Mhe. Haji Mwadini Makame	Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati/Jimbo la Nungwi
27.Mhe. Thuwaybah Edington Kissasi	Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko/Jimbo la Fuoni
28.Mhe. Abdalla Juma Abdalla	Jimbo la Chonga
29.Mhe. Abdalla Moh'd Ali	Jimbo la Mkoani
30.Mhe. Abdi Mosi Kombo	Jimbo la Matemwe
31.Mhe. Ali Mzee Ali	Kuteuliwa na Rais
32.Mhe. Ali Abdalla Ali	Jimbo la Mfenesini
33. Mhe. Ali Salum Haji	Jimbo la Kwahani
34.Mhe. Amina Iddi Mabrouk	Nafasi za Wanawake

35. Mhe. Asaa Othman Hamad	Jimbo la Wete
36.Mhe. Asha Abdu Haji	Nafasi za Wanawake
37.Mhe. Asha Bakari Makame	Nafasi za Wanawake
38.Mhe. Ashura Sharif Ali	Nafasi za Wanawake
39.Mhe. Bikame Yussuf Hamad	Nafasi za Wanawake
40.Mhe. Farida Amour Mohammed	Nafasi za Wanawake
41.Mhe. Fatma Mbarouk Said	Jimbo la Amani
42.Mhe. Hamza Hassan Juma	Jimbo la Kwamtipura
43.Mhe. Hassan Hamad Omar	Jimbo la Kojani
44.Mhe. Hija Hassan Hija	Jimbo la Kiwani
45.Mhe. Ismail Jussa Ladhu	Jimbo la Mji Mkongwe
46.Mhe. Jaku Hashim Ayoub	Jimbo la Muyuni
47.Mhe. Kazija Khamis Kona	Nafasi za Wanawake
48.Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa	Jimbo la Kikwajuni
49.Mhe. Makame Mshimba Mbarouk	Jimbo la Kitope
50.Mhe. Mbarouk Wadi Mussa	Jimbo la Mkwajuni
51.Mhe. Mgeni Hassan Juma	Nafasi za Wanawake
52.Mhe. Mlinde Mbarouk Juma	Jimbo la Bumbwini
53.Mhe. Mohammed Haji Khalid	Jimbo la Mtambile
54.Mhe. Mohammed Mbwana Hamad	Jimbo la Chambani

55.Mhe. Mohammed Said Mohammed	Jimbo la Mpendae
56. Mhe. Mtumwa Kheir Mbarak	Nafasi za Wanawake
57.Mhe. Mussa Ali Hassan	Jimbo la Koani
58. Mhe. Mussa Khamis Silima	Jimbo la Uzini
59.Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa	Nafasi za Wanawake
60.Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi	Nafasi za Wanawake
61.Mhe. Nassor Salim Ali	Jimbo la Rahaleo
62.Mhe. Omar Ali Shehe	Jimbo la Chake-Chake
63.Mhe. Panya Ali Abdalla	Nafasi za Wanawake
64.Mhe. Rashid Seif Suleiman	Jimbo la Ziwani
65.Mhe. Raya Suleiman Hamad	Nafasi za Wanawake
66.Mhe. Rufai Said Rufai	Jimbo la Tumbe
67.Mhe. Saleh Nassor Juma	Jimbo la Wawi
68.Mhe. Salim Abdalla Hamad	Jimbo la Mtambwe
69.Mhe. Salma Mohammed Ali	Nafasi za Wanawake
70.Mhe. Salma Mussa Bilali	Nafasi za Wanawake
71.Mhe. Salmin Awadh Salmin	Jimbo la Magomeni
72.Mhe. Salum Amour Mtondoo	Jimbo la Bububu
73.Mhe. Shadya Mohamed Suleiman	Nafasi za Wanawake
74.Mhe. Shamsi Vuai Nahodha	Jimbo la Mwanakwerekwe

75. Mhe. Shawana Bukheti Hassan	Jimbo la Dole
76.Mhe. Subeit Khamis Faki	Jimbo la Micheweni
77.Mhe. Suleiman Hemed Khamis	Jimbo la Konde
78.Mhe. Ussi Jecha Simai	Jimbo la Chaani
79.Mhe. Viwe Khamis Abdalla	Nafasi za Wanawake
80.Mhe. Wanu Hafidh Ameir	Nafasi za Wanawake

Ndugu Ibrahim Mzee Ibrahim **Katibu wa Baraza la Wawalishi**

Kikao cha Ishirini na Tisa – Tarehe 26 Julai, 2011

(Kikao kulianza saa 3:00 asubuhi)

DUA

Mhe. Naibu Spika (Ali Abdalla Ali) alisoma dua

MASWALI NA MAJIBU

Nam. 201

Ujenzi wa Barabara ya Mtambile – Gando

Mhe. Hija Hassan Hija - Aliuliza:-

Naipongeza Serikali ya Norway na SMZ kwa mashirikiano kwa msaada wa Ujenzi wa barabara sita za Kusini Pemba ikiwemo ile ya Mtambile – Mwambe 9.4 km. Msaada huo wa ujenzi wa barabara kitaalamu ulipangwa kujengwa kwa hatua nne muhimu ambazo ni:-

- subgreding (10 – 15) cm,
- sub-base (10 – 15) cm.
- Base 10 cm.
- Asphate 0.14 cm

ambapo hatua zote hizi nne zimetengewa kiasi chake cha fedha kwa kila barabara.

(a) Zipo taarifa kuwa Mjenzi (*contractor*), Mshauri Muelekezi (*consultant*) na Mfadhili (Donor) ni mmoja. Je, hilo ni kweli.

(b) Zipo taarifa kuwa taratibu za ujenzi zinaendelea kukiukwa kwa kiasi kikubwa na Serikali imechukua hatua ya kuzuia ujenzi huo kwa muda; Je, hilo ni kweli.

(c) Katika ujenzi wa barabara hizo inasemekana kuwepo kwa harufu ya wizi. Je, hilo ni kweli.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano - Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 201 lenye kifungu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Hakuna *contractor*, anayejenga mradi huu zaidi ya Idara ya *UUB* na Mshauri Mwelekezi ni kampuni ya *Poyry Ifra* inayotoka Uswiss akishirikiana na na Kampuni ya *Intechbeusch* inayotoka Uswiss pamoja na usimamizi wa Idara ya *UUB*.

(b) Wizara haijazuia ujenzi wa barabara hiyo, isipokuwa kasi ya ujenzi ilipungua kidogo kwa ajili ya kuchunguza tuhuma zilizokuwepo.

(c) Wizara yangu bado haijathibitisha shutuma za wizi kama alivyosema Mhe. Mwakilishi.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Naibu spika, kabla ya kujibiwa swali langu la nyongeza naomba nimpongeze sana Ndugu yangu Mhe. Naibu Waziri kwa kupata nafasi nyengine ya kuwa Mkurugenzi wa Habari na Uenezi wa CCM Zanzibar.

Baada ya hayo Mhe. Naibu Spika, naomba kuuliza swali la nyongeza lenye vifungu a na b.

(a) Kwa kuwa amesema kwamba hakuna hatua ya ujezi iliyozuiliwa, naomba kujua tu, mradi ule ulipangwa kuanza lini na kumalizika lini na sasa hivi tuko katika kipindi gani cha kumalizika.

(b) Amesema kwamba hakuna wizi uliofanyika. Mimi ninavyojua yuko mfanyakazi mmoja wa wizara yake ambaye alikuwa ni *site engineer* aliondoshwa kusimamia barabara ya Mzingani – Wambaa kwa sababu ya madai ya wizi yaliyofanyika kwa kifedha. Je, kauli hii ilikuwa sahihi na kwa hivyo walimuonea kumuondosha katika nafasi hiyo.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Naibu Spika, barabara hiini miongoni mwa barabara sita zilizoko katika Mkoa wa Kusini zenye kujengwa kwa mfumo wa lami baridi. Mategemeo yetu kwamba barabara hii aliyoiulizia Mhe. Mwakilishi itakamilika katika mwezi wa Disemba, 2011. mategemeo hayo yanaendana na kasi inayoendelea hivi sasa ya ujenzi wa barabara hiyo.

Jibu la pili, Mhe. Naibu spika, tumeeleza kwamba, wizara yangu bado haijathibitisha tuhuma za wizi anazozisema Mhe. Mwakilishi. Lakini kwa kuweza kuona mfumo wa utawala bora na kuweka uwazi yule anayeshitakiwa ni vyema akaondoka katika sehemu ile ili kupisha taratibu za kiuchunguzi na upembuzi ili kuweza kufuatlia vizuri kupata kubaini ukweli wa mambo ukoje. Tumechukua hatua hiyo kwa mnasaba huo wa kutaka kuona uwazi na uajibikaji ili kugundua upungufu unaofikiriwa kutokea.

Mhe. Mohammed Mbwana Hamad: Ahsante Mhe. Naibu Spika, kwa kunipa nafasi ya kumuuliza Mhe. Naibu Waziri swali moja la nyongeza lenye a na b.

(a) Mhe. Naibu Spika, miongoni mwa barabara za Mkoa wa Kusini Pemba sita zinazojengwa ni barabara ya Kenya – Chambani. Ujenzi wa barabara unapitia hatua nne, hatua ya kwanza ni *sub grading, sub base, base* na hatua ya nne *asphase*. Mhe. Naibu Spika, barabara hii ya Chambani hatua ya kwanza ya kuchimbwa haikuchimbwa. Kwa sababu ilionekana kwamba ina jiwe la msingi ambalo lilijengwa zamaji. Je, fedha hii ambayo ilikuwa ichimbiwe barabara ile imetumika vipi.

(b) Miongoni mwa matengenezo yaliyopitia katika barabara ile ya Chambani ni kung'olewa kwa miti ya wananchi wa eneo lile. je, serikali ina mpango gani kuwalipa fidia watu hawa walong'olewa miti yao.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Naibu Spika, utaratibu wa ujenzi wa barabara ni kama zilivyo tasnia nyengine ni jambo la kitaalamu. Uwezo wetu wanasiasa ni kuona na kusikiliza, lakini napenda nimthibitishie kwamba barabara hiyo ya Chamani wakandarasi walijiridhisha na kuona utaratibu uliopo unakidhi kuendeleza mfumo ule wa kuendeleza ujenzi. Katika hayo baadhi ya maeneo unayoyasema kwamba kulikuwa kuna barabara haikuwa *graded* na fedha zake hazikutumika.

Salim Abdalla Hamad: Mhe. Naibu Waziri katika kujibu swali lake alisema kuwa ujenzi wa barabara ni wa kitaalamu na kuwa sisi ni kuona tu, kama kwamba hakuna utaalamu huo. Kwa hivyo, kwa sababu katika Baraza hili kuna wataalamu wa kila fani hata Mhe. Waziri wake mwenyewe ni mtaalamu, ningeliomba suala hili lifutike.

Mhe. Naibu Spika: Sikukufahamu hoja yako Mheshimiwa hebu rudia.

Salim Abdalla Hamad: Mhe. Naibu Waziri katika kujibu swali lake alisema kuwa ujenzi wa barabara ni wa kitaalamu na kuwa sisi ni kuona tu na kusikiliza, sasa mimi kauli hii sikubaliani nayo kwa sababu nina jua katika Baraza hili kuna wataalamu wa kila fani, kuna walimu, madaktari, mainjinia. Kwa hivyo, suala hili lifutwe tusionekane kuwa tumo humu hatuna utaalamu wowote hili ni Baraza la kitaalamu.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Naibu Spika, nikiendelea kujibu swali (a) ni kwamba kuna baadhi ya maeneo ambayo yamechimbwa na gharama za fedha zile zimetumika kama zilivyokusudiwa kwa baadhi ya maeneo kuongeza kifusi na baadhi ya maeneo kuchimbwa.

(b) Mhe. Naibu spika, napenda tena kulithibitishia Baraza lako tukufu kwamba kama kuna mwananchi yoyote ambaye mti wake umekatwa kwa ajili ya utanuzi wa barabara ua ujenzi wa barabara serikali itamlipa fidia.

Nam. 227

Wizara Kumiliki Majengo ya Skuli

Mhe. Jaku Hashim Ayoub - Aliuliza:-

Moja kati ya matatizo yanayoikabili Wizara ya Elimu ni kutokuwepo kwa sheria inayowaruhusu kumiliki majengo yake. Hali hiyo imepelekea Wizara hiyo kutokuwa na hati miliki ya majengo kadhaa yanayotumiwa na baadhi ya skuli.

(a) Je, Wizara haioni kwamba kutokuwa na hati miliki za majengo hayo kunawarahisishia baadhi ya wajanja kuweza kuyauza majengo hayo bila ya kufuata utaratibu uliowekwa kwa mujibu wa sheria.

(b) Wizara yako inaliangalia vipi tatizo hilo.

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali - Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 227 lenye kifungu (a) na (b), kwanza naomba kutoa maelezo kama ifuatavyo:-

Ni kweli kwamba mojawapo ya tatizo yanayozikumba baadhi ya taasisi zetu za elimu ni ukosefu wa hati miliki za maeneo yake licha ya juhudi kubwa zinazochukuliwa na Kamati za Skuli na Wizara katika kufuatilia upatikanaji wa hati miliki. Baada ya maelezo hayo naomba kujibu kama ifuatavyo:-

(a) Pamoja na kuwa baadhi ya skuli hazina hati miliki lakini mazingira ya kuuzwa majengo ya skuli na baadhi ya wajanja bila ya kufuatwa utaratibu wa Kisheria ni vigumu

kutokea. Hata hivyo, iliwahi kutokezea kuuzwa kwa nyumba katika vijiji vya maendeleo iliyokuwa na madarasa ya maandalizi lakini nyumba hio haikuwa mali ya Wizara bali ilikuwa inamilikiwa na Wizara ya Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati. Wizara haikuwa na nguvu za Kisheria kuzuia kuuzwa kwa nyumba hiyo kwa vile haikuwa ni mali yetu.

(c) Wizara kwa kushirikiana na Kamati za Skuli na Wizara ya Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati inafanya bidii kuhakikisha skuli zetu zote zinapimwa na kupatiwa hati miliki za maeneo yake.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri naomba kuuliza swali moja la nyongeza.

a) Skuli ngapi zilizokuwa hazina hati miliki kwa upande wa Unguja na kwa upande wa Pemba.
b) Lini zitapata hatimiliki hizo.
c) Ni sababu gani Chuo cha Nkurumah hadi hii leo tokea kuanzishwa kinashindwa kumiliki hati miliki.

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Ni skuli nyingi ambazo siwezi kukutajia skuli ngapi ni skuli nyingi hazina hati miliki lakini zinayo *sate plan* lakini kwa utaratibu tulionao hivi sasa tunajua kwamba hili ni tatizo na kwa kushirikiana na Wizara ya Maji, Nishati na Ardhi pamoja na Wizara Nchi Afisi ya Rais Fedha, Uchumi, na Mipango ya Maendeleo hilo jambo tunalifanyia kazi ili kuona skuli hizo zinapata hati miliki.

Skuli ya Nkuruma ilikuwa na hati tokea zamani maana imeanzishwa tokea miaka ya 1950 na zaidi na wakati huo hati yake ilikuwa ni pan asana, imevuka barabara na kufikia upande

wa pili kule. Lakini kwa bahati hivi sasa ndio katokea mtu kachukua ile sehemu pale ambayo nakiri, lakini kwa sababu kesi ipo Mahakamani siwezi kuieleza kwa uwazi kabisa.

Mhe. Omar Ali Shehe: Mhe. Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi hii kuuliza swali dogo la nyongeza.

Kwa kuwa muongozo uliotolewa na Wizara inayohusika na mambo ya upimaji ilielekeza kwamba Wizara husika ndio inayopaswa kugharamia shughuli za upimaji wa majengo yake naomba nimuulize Mhe. Waziri.

Je, Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kwa mwaka huu imetenga kiasi gani katika kugharamia upatikanaji wa hati katika maskuli.

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Ni kweli Wizara inayohusika ikiwa tayari kwenda kupima na ikijulisha Wizara yangu kwamba sasa hivi tuko tayari kwenda kupima tulipie gharama bila ya shaka tutalipa hatuna tatizo hilo kabisa.

Mhe. Rashid Seif Suleiman: Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba kuuliza suala moja la nyongeza.

Kwa kuwa amekiri kwamba kama ilivyotajwa Wizara ndio muhusika wa kufuatilia hizi hati miliki, naomba nimuulize.

a) Mhe. Waziri ni afsa gani katika Wizara ya Elimu mwenye dhamana ya kufuatilia hati miliki za skuli.

b) Lakini pili kama hati miliki imeshapatikana ni nani mlinzi wa ile mipaka ya skuli wakati hatimiliki imeshapatikana.

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Wizara yangu ina maofisa wanaohusika na majenzi ya skuli kila Mkoa, wao wanakuwa ni dhamana wa kuhakikisha kwamba wanafuatilia na kuona kwamba zile skuli zinapatiwa hatimiliki. La kwanza linatekelezwa vizuri la kupata *site plan* karibu skuli zote sasa hivi wanazo bado skuli chache tu ambazo hizo hazijapimwa.

Kwa upande wa mlinzi Mhe. Naibu Spika, hapa lazima na taka pawe na mashirikiano baina ya walimu wa skuli, wazee wa kijiji, wakuu wa wilaya wote hawa ni walinzi wa kuona kwamba maeneo ya skuli hayavamiwi kwa sababu hiyo hata juzi imetokezea katika skuli moja kuna mtu mmoja kenda kujenga nyumba katika eneo la skuli, wazee wa kijiji wakaiona na wakamueleza wao kwanza kwa sheha halafu sheha yeye akamueleza yule jamaa hakuondoka, badala yake akaelezwa Mkuu wa Wilaya nay eye akamsimamisha asiendelee na ujenzi. Kwa hivyo ulinzi ni suala la kushirikiana kwa sababu waziri na wizara wako mbali lakini wazee ndio wako pale pale, kamati ya skuli ipo pale pale na vizuri tushirikiane.

Mhe. Naibu Spika, inashangaza siku hizi katika hali yetu ni kwamba anaweza mtu akapita skuli hata amkute mtu yuko juu ya paa anaezua bati basi hawezi kuuliza ananyamaza kimya anasema haikumuhusu, sasa hili ni tatizo ulinzi ni wetu sote Mhe. Naibu Spika.

Nam. 233

Hadhi ya Skuli Binafsi

Mhe. Jaku Hashim Ayoub - Aliuliza:-

Serikali iliporuhusu utoaji wa elimu kupitia sekta binafsi walijitokeza watu wengi walioanzisha skuli. Lakini baadhi ya skuli hizo hazina hadhi ya kuitwa skuli kimajengo. Mtu anakodi nyumba ya mtu iliyokusudiwa kwa maisha binafsi ya familia anaanzisha skuli kwa nyumba hiyo.

Kwa nini Serikali inaruhusu skuli kama hizo ambazo majengo yake hayakufuata utaratibu wa majengo ya skuli kwa ukubwa wa vyumba na upatikanaji wa hewa ya kutosha.

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali - Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 233 kama ifuatavyo:-

Ni kweli kwamba baada ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, kuruhusu kuanzishwa tena skuli za binafsi baadhi ya skuli za binafsi zilianzishwa katika majengo ya kawaida ambayo yalikuwa ni makaazi ya watu binafsi yaliyobadilishwa kuwa skuli. Zipo skuli nyingi za watu binafsi na za jamii hasa skuli za maandalizi na msingi ambazo ziko katika majengo ya namna hii. Skuli hizo zilikubalika kwa vile wakati skuli binafsi ziliporuhusiwa kulikuwa hakuna majengo ya skuli yaliyokuwa tayari na hivyo baadhi ya waanzilishi wa skuli binafsi waliruhusiwa kuanzisha skuli katika majengo ya muda. Skuli hizi zimeruhusiwa kufanya kazi baada ya Wizara kuridhika kwamba vyumba vyake vinatosha kuchukua idadi maalumu ya wanafunzi na sehemu ilipo skuli hiyo ina mahitaji makubwa ya huduma hiyo. Skuli zenye majengo ya muda hupewa vibali vya muda tu hadi hapo wamiliki wake watakapoanzisha majengo ya kudumu. Napenda kumuhakikishia Mhe. Mwakilishi kuwa Wizara inazingatia sana afya na usalama wa wanafunzi na walimu wanaosoma na kufanya kazi katika skuli zetu zote.

Hata hivyo, katika miaka ya karibuni kumekuwa na ongezeko la skuli za binafsi zenye majengo ya kisasa, yenye hadhi na vifaa vya skuli na kutokana na ongezeko hilo skuli zilizoko katika majengo ya muda zitapungua hatua kwa hatua.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri naomba kuuliza suala la nyongeza.

Mhe. Waziri ni skuli ngapi ambazo hazikutumia vigezo na huku Wizara imeziruhusu.

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Siwezi kumpa hisabu kama ni ngapi au kumi na mbili, kumi na tatu au kumi na nne, lakini najua kwamba zipo skuli ambazo kwa muda zimetumia vigezo lakini kwa baadae wakitaka tena kukata leseni hawataruhusiwa kwa sababu walipewa watumie maeneo yale kwa muda, baada ya hapo hawatopewa tena leseni kwa sababu lazima baada ya muda fulani wahakikishe kwamba wanajenga majengo ya kudumu na hili linaendelea kutekelezwa, ndio maana badadhi ya skuli zinabadilika sasa hivi na kuwa na majengo mazuri yenye hadhi ya skuli.

Mhe. Nassor Salim Ali: Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri naomba kuuliza suala moja la nyongeza.

Kwanza nimpongeze Mhe. Waziri wa Wizara ya Elimu kwa kujenga jengo la kisasa la madrasa pale katika skuli ya Mwembeshauri. Kuna taarifa kwamba jengo lile linataka kupewa wanafunzi wa skuli ya sekondari katika skuli nyengine kuja pale kusoma.

Je? suala hili ni kweli na kama si kweli haioni kwamba Wizara ipo haja ya jengo lile kulipandisha Skuli ya Mwembeshauri kuwa ya Sekondari.

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Nadhani niliposoma bajeti yangu hapa nilisema kwamba kuna matengenezo makubwa yanayofanywa katika skuli ya Tumekuja, na Hamamni sasa inabidi wanafunzi wa skuli hii wapate mahali pa kujishikiza kwa hivyo ni kweli skuli ile ambayo imeshajengwa pale ndio maana imeharakishwa sehemu ile kumalizwa kujengwa, ni kwa sababu tuwaazime watoto wanaotoka katika skuli hizi ambazo sasa hivi zitafanyiwa matengenezo makubwa.

Sasa katika hali hiyo ningemuomba Mheshimiwa akastahamili katika kipindi kifupi cha matengenezo baadae tukishamaliza matengenezo wanafunzi wale watarudi katika skuli yao na hiyo skuli hapo tutafikiria kufanya sekondari hiyo hatuoni tabu kwa sababu wanafunzi wanaongezeka kila siku, lazima tutanue skuli za sekondari.

Mhe. Subait Khamis Faki: Pamoja na majibu mazuri naomba kuuliza suala moja la nyongeza.

Kwanza na mimi naishukuru sana Wizara ya Elimu pamoja na serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ya kutoa nafasi kuona kwamba kuna haja ya kuwaruhusu watu binafsi kuanzisha skuli hizi. Ili kuendelea kuleta elimu na kuleta maendeleo zaidi katika nchi yetu, sasa kwa sababu kuna vigezo maalum ambavyo vinatakiwa ili mmiliki wa binafsi anayetaka kuanzisha skuli aidha akamilishe ndio anapewa ruhusa ya kuendeleza kuwa skuli.

Sasa napenda kumuuliza Mhe. Waziri, je kwa sababu majengo nayo ni moja ya masharti kwa sababu skuli inatakiwa iwe na majengo maalum ili ionekane kama ni skuli.

a) Je, kuna kamati maalum ya wizara yake ainayopitia kwa watu binafsi wanaoomba kuanzishwa skuli na kupita kuona katika majengo hayo ya skuli.

b) Haoni Mheshimiwa kama kuna haja ya kuanzisha kamati maalum wizara yake ya kupitia hayo majengo ya watu binafsi wanaotaka kuanzisha hizo skuli.

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Tulikuwa tuna ofisi ya mkaguzi wa elimu ambayo sasa hivi tumeipandisha cheo na inakuwa ni Afisi ya Mkaguzi mkuu wa Elimu, ambao hawa wakati unapotaka kuanzisha skuli unapeleka maombi kwa Mrajis, Mrajis anaijulisha ofisi ya Mkaguzi Mkuu na wao ndio wanakwenda kukagua hiyo skuli inayotaka kuanzishwa, kama imeridhika na hivyo vigezo ndio inatoa ruhusa. Lakini Afsisi ya Mkaguzi Mkuu wa Elimu ikiwa haikuridhika huwezi kuanzisha skuli hiyo na bila ya sahaka mrajis atakupa kibali cha kuanzisha hiyo skuli.

Mhe. Naibu Spika: Mwenyekiti wa *PAC* kaleta t angazo kwamba wajumbe wake waende wakakutane kwa muda wa dakika kumi kuna jambo muhimu, kwa hivyo nawatangazia wajumbe hao kabla ya kusomwa hii hotuba watoke nje wakazungumme na Mwenyekiti, na baada ya dakika kumi warejee.

HOJA ZA SERIKALI

Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fedha kwa Mwaka wa Fedha

2011/2012 Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko

Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko: Mhe. Naibu Spika**,** naomba kutoa hoja kwamba Baraza lako tukufu sasa likae kama Kamati ya Mapato na Matumizi kwa ajili ya kupokea, kuzingatia, kuchangia na hatimae kuidhinisha makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko kwa kazi za kawaida na maendeleo kwa mwaka wa fedha 2011/2012.

Mhe. Naibu Spika, awali ya yote naomba kuchukua fursa hii adhimu kumshukuru Mwenyezi Mungu Mtukufu, kwa kutuwezesha leo hii kukutana hapa tukiwa na afya njema. Aidha, kama walivyotangulia Waheshimiwa Mawaziri wengine, na mimi naomba uniruhusu kuchukua fursa hii kumpongeza kwa dhati kabisa Mheshimiwa Dk. Ali Mohammed Shein kwa kuchaguliwa kwake kuwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi na kumuwezesha kuunda Serikali ya Awamu ya Saba yenye mfumo wa Umoja wa Kitaifa. Ni matumaini yangu kuwa muundo huu wa Serikali utatuwezesha kustawisha zaidi misingi ya utawala bora na kuimarisha shughuli za maendeleo ya kijamii, kisiasa na kiuchumi kwa kasi kubwa zaidi. Ni matumaini yangu vile vile kuwa mfumo wa Serikali tulionao utachochea zaidi kasi ya kuimarika kwa uchumi wa Zanzibar na Tanzania kwa ujumla chini ya Uongozi wa Mheshimiwa Dk. Shein.

Mhe. Naibu Spika, naomba vile vile, kuchukua fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Seif Sharif Hamad kwa kuteuliwa kuwa Makamu wa Kwanza wa Rais na Mheshimiwa Seif Ali Iddi kuwa Makamu wa Pili wa Rais. Ni dhahiri kuwa Zanzibar na Wananchi wake wamejenga matumaini makubwa na kuwa na imani na Viongozi wao ya kuwaletea mabadiliko na kuijenga Zanzibar kwa kasi kubwa zaidi.

Mhe. NaibuSpika, naomba kwa mara nyengine tena kuchukua fursa hii kumshukuru sana Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa kuniamini na kuniteua kuwa Waziri katika Serikali anayoingoza. Wizara niliyokabidhiwa ni moja ya Wizara kubwa zinazosimamia uchumi wa nchi yetu na ni Wizara yenye changamoto nyingi katika juhudi zetu za kuimarisha uchumi na ustawi wa wananchi wetu. Kwa nafasi hii naomba kutoa Ahsante kwa Mheshimiwa Rais na kuahidi kuzifanya kazi zangu za uwaziri kwa juhudi na maarifa yangu yote.

Mhe. Naibu Spika, napenda pia kuchukua nafasi hii kukupongeza wewe binafsi kwa kuchaguliwa tena kuliongoza Baraza hili tukufu. Kuchaguliwa kwako kuliongoza tena Baraza hili ni ushahidi tosha wa imani waliyonayo Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi kwako na kwa uongozi wako wenye busara na ukomavu mkubwa wa kujenga misingi ya demokrasia ndani na nje ya Baraza la Wawakilishi. Aidha, nawashukuru Waheshimiwa Wawakilishi wote kwa michango yao ya dhati kwa Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko. Ni mategemeo yangu kuwa watakuwa karibu sana na mimi kwa kunishauri kunikosoa na kunieleza ili niweze kutekeleza majukumu yangu kwa ufanisi wa juu kabisa.

Mhe. Naibu Spika, shukurani za pekee zimwendee Mheshimiwa Naibu Waziri wangu Nd. Thuwaibah Edington Kisasi kwa msaada na mashirikiano yake makubwa anayonipa. Aidha, nawashukuru kwa dhati itokayo kwenye sakafu ya moyo wangu Nd. Julian Banzi Raphael – Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu wangu Nd. Rashid Ali Salim pamoja na Wakurugenzi wote na Meneja wa *ZSTC* na *MTC* kwa juhudi zao za kupigiwa mfano na kwa namna wanavyochapa kazi bila ya kujali saa za kazi au siku za

mapumziko. Juhudi zao hizo ni za kupigiwa mfano na nawaombea kila la kheri katika maisha yao. Bila ya msaada wao ningeshindwa kufanya kazi zangu ipasavyo. Nawaomba wazidishe mashirikiano yao kwangu ili tuweze kutekeleza majukumu yetu kwa mafanikio makubwa.

Mhe. Naibu Spika, kwa kuwa hili ni Baraza la kwanza la Bajeti baada ya Uchaguzi Mkuu wa Oktoba 2010, naomba kuliarifu Baraza lako kuwa Muundo wa Wizara hii ulifanyiwa mabadiliko na kuundwa Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko. Majukumu ya uratibu wa uwekezaji vitega uchumi pamoja na uendelezaji wa utalii ambayo yalikuwa ni sehemu ya Muundo wa Wizara hii yalihamishiwa katika Wizara nyengine. Marekebisho hayo ya Muundo yaliambatana pia na marekebisho ya majukumu ya kifedha ambapo bajeti ya Wizara ya mwaka 2010/2011 ilirekebishwa pia kama itakavyofafanuliwa katika hotuba hii hapo baadae. Muundo na majukumu mapya ya Wizara yamechambuliwa zaidi katika Kiambatisho Nam. 1.

Mabadiliko hayo Mhe. Naibu Spika, yamesababisha pia kufanyika kwa mapitio ya maudhui ya ala (*instruments*) kuu za kiutendaji kama vile, Dira ya Wizara, Dhamira na Malengo yake Makuu, Mpango Mkakati wa Viwanda n.k. ili kujielekeza katika utekelezaji wa majukumu mapya ya Wizara.

Mhe. Naibu Spika, maandalizi ya mapendekezo ya bajeti hii yamepitia na kuzingatiwa katika hatua na taasisi mbali mbali. Naomba kutanguliza shukurani zangu kwa Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo ya Baraza la Wawakilishi inayoongozwa na Mhe. Salmin Awadh Salmin Mwakilishi wa Jimbo la Magomeni kwa kuchambua mapendekezo ya bajeti ya Wizara na kuikubali na hatimae kuridhia kuwasilishwa mbele ya Baraza lako Tukufu. Baadhi ya maelezo ya mapendekezo ya bajeti hii yamegusiwa

kwa muhtasari katika Hotuba ya Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo ya kuwasilisha Mapendekezo ya Bajeti ya Serikali ambayo tayari imezingatiwa na kuidhinishwa na Baraza lako Tukufu.

Hivyo, katika hotuba hii, Mhe. Naibu Spika, nitafanya mapitio ya jumla ya hali ya biashara ulimwenguni na jinsi mwenendo huo wa biashara ulivyoathiri mwendo wa biashara wa Zanzibar. Kadhalika nitafanya mapitio kuhusu hali ya maendeleo ya Viwanda, utekelezaji wa bajeti ya Wizara kwa mwaka 2010/2011, mwenendo wa mashirika ya serikali yaliyochini ya wizara, kubainisha changamoto mbali mbali na hatimae kubainisha malengo kwa mwaka 2011/2012 na sura ya bajeti ya Wizara kwa kipindi hicho.

Hali ya Biashara Duniani:

Mhe. Naibu Spika, kwa ujumla hali ya biashara duniani iliendelea kuimarika ambapo usafirishaji wa bidhaa uliongezeka na kufikia asilimia 14.5 kwa mwaka 2010 kutoka asilimia 12 mwaka 2009 ingawa kwa mwaka 2011 usafirishaji huo unategemewa kupunguwa kwa asilimia 6.5. Upungufu huo wa usafirishaji unatokana na matukio ya hali ya majanga ya kimaumbile kama vile Tsunami, mafuriko, uharamia wa vyombo vya baharini (*pirates*) katika ukanda wa Bahari ya Hindi pamoja na machafuko yanayozikumba nchi za kiarabu.

Mhe. Naibu Spika, taarifa za biashara ya kimataifa zinaonesha kuwa mwaka 2010 nchi za Ulaya zimeongoza kwa kusafirisha bidhaa zenye thamani ya dola 5.63 trilioni sawa na asilimia 38 ya usafirishaji duniani (*world total export*) na kuagiza bidhaa zenye thamani ya USD 5.84 trilioni sawa na asilimia 39 ya uagiziaji wa bidhaa duniani (*world total import*). Nchi za Asia ni za Pili zikiwa

zimesafirisha bidhaa zenye thamani ya USD 4.69 trilioni sawa na asilimia 32 na kuagiza bidhaa zenye thamani ya USD 5.50 trilioni sawa na asilimia 30. Marekani ya Kaskazini ni ya tatu ambayo imesafirisha bidhaa zenye thamani ya USD 1.96 trilioni sawa na asilimia 13 ya usafirishaji wa dunia na imeagiza bidhaa zenye thamani ya USD 2.68 trilioni sawa na asilimia 18.

Mhe. Naibu Spika**,** nchi zinazofuatia katika kusafirisha na kuagiza bidhaa ni Nchi za Mashariki ya Kati (*Middle East*), Nchi za Jumuiya ya Madola (*Commonwealth Independet States- CIS*), Marekani ya Kusini na mwisho ni Nchi za Afrika. Nchi za Afrika zimesafirisha bidhaa zenye thamani ya USD 500 bilioni sawa na asilimia 3 na kuagiza bidhaa zenye thamani ya USD 463 bilioni sawa na asilimia 3. Kiambatanisho Nam. 2 Jadweli Nam. 1(a) kinafafanua zaidi.

Mhe. Naibu Spika, kwa upande wa nchi moja moja, taarifa hizo zinaonesha kuwa China ndiyo nchi inayoongoza katika kusafirisha bidhaa, ikifuatiwa na Marekani na Ujerumani. Kwa upande wa uagiziaji bidhaa, Marekani ndiyo nchi inayoongoza katika kuagiza bidhaa ikifuatiwa na China na Ujerumani. Nchi Sita (6) zinazongoza kwa usafirishaji na uagiziaji bidhaa kwa mwaka 2010 zinaoneshwa katika Kiambatanisho Nam. 2 Jadweli Nam. 1(b).

Hali ya Biashara ya Zanzibar:

Mhe. Naibu Spika, kwa upande wa Zanzibar hali ya biashara ya usafirishaji imekuwa ikipanda na kushuka kutegemea na uzalishaji wa bidhaa hapa ndani na mwenendo wa bei za bidhaa hizo katika soko la dunia. Katika mwaka 2010, Zanzibar ilisafirisha nje ya nchi bidhaa zenye thamani ya Tshs. 17,907.0 milioni, ukilinganisha na bidhaa zenye thamani ya Tshs. 29,744

milioni zilizosafirishwa mwaka 2009 na Tshs. 30,189 milioni zilizosafirishwa mwaka 2008 kama inavyoonekana katika Kiambatanisho Nam. 2 Jadweli Nam. 2.

Mhe. Naibu Spika, kwa sasa Zanzibar imejikita zaidi katika usafirishaji wa mazao ya kilimo na ya baharini. Katika mwaka 2010, zao la karafuu limechangia asilimia 62.45 ya thamani ya usafirishaji na bidhaa za baharini ukiwemo mwani zimechangia asilimia 22.16 ya usafirishaji wote. Katika kipindi hicho Zanzibar ilisafirisha karafuu zenye thamani ya Tshs. 11,181/= milioni ikilinganishwa na karafuu zenye thamani Tshs. 14,077 milioni mwaka 2009. Kiasi hicho ni asilimia 27 ya usafirishaji wote wa mwaka huo. Bidhaa hizo zilisafirishwa zaidi katika nchi za Denmark, Marekani, Ufaransa, China, Nchi za Falme za Kiarabu, Singapore, na India.

Mhe. Naibu Spika, uagiziaji wa bidhaa kutoka nje kwa upande mwengine unaonesha mwenendo wa kuongezeka kila mwaka, kutegemeana na mahitaji ya bidhaa hizo hapa Zanzibar. Katika mwaka 2010, bidhaa zenye thamani ya Tshs. 129,137 milioni ziliagiziwa ikiwa ni ongezeko la asilimia 6.83 ukilinganisha na uagiziaji wa Tshs. 120,882 milioni katika mwaka 2009. Kiambatanisho Namb. 2 Jadweli Nam. 2 linaelezea zaidi.

Mhe. Naibu Spika, uagiziaji wa bidhaa hapa Zanzibar unajumuisha bidhaa za magari na vyakula zenye thamani ya Tshs. 38,464 milioni, vifaa vya ujenzi, umeme na machine zenye thamani ya Tshs. 35,220 milioni, bidhaa za kemikali na madawa zenye thamani ya Tshs. 7,153 milioni. Bidhaa zinazoagizwa Zanzibar kwa wingi zinatoka katika Nchi za Falme za Kiarabu, China, Ubelgiji, Japan, Singapore, India, Pakistani, Marekani, na Australia.

Mhe. Naibu Spika, biashara kati ya Zanzibar na Tanzania Bara imekuwa ya aina mbili, ikihusisha bidhaa zinazozalishwa Zanzibar na kuuzwa Tanzania Bara na zile zinazoagizwa kutoka nje na kahaulishwa kwenda Tanzania Bara kwa upande mmoja, na bidhaa zinazotoka Tanzania Bara kuja Zanzibar kwa upande wa pili. Kwa mwaka 2010, uagiziaji kutoka Tanzania Bara ulikuwa Tshs. 23,268.69 milioni ukilinganishwa na Tshs. 19,651 milioni katika mwaka 2009. Kwa upande wa usafirishaji, bidhaa zenye thamani ya Tshs. 3,303.51 milioni zilisafirishwa kwenda Tanzania Bara katika mwaka 2010 ukilinganisha na bidhaa zenye thamani ya Tshs. 4,256.6 milioni zilizosafirishwa kwa mwaka 2009.

Mhe. Naibu Spika, kuongezaka kwa mahitaji ya chakula na kukua kwa shughuli za ujenzi kutokana na kukua kwa sekta ya utalii na ongezeko la idadi ya watu, kunaifanya Zanzibar kuzidi kuagizia bidhaa kutoka Tanzania Bara ili kuziba pengo la mahitaji ya bidhaa hizo. Bidhaa zinazoagizwa zaidi ni pamoja na chakula kama vile nafaka, matunda na mbogamboga, vifaa vya ujenzi kama vile saruji, nondo, mbao na bidhaa nyenginezo.

Mhe. Naibu Spika, katika uendeshaji biashara baina yetu na Tanzania Bara kumekuwepo malalamiko kwa wafanyabiashara kulipa kodi mara mbili wakati wanaposafirisha bidhaa zao kupeleka Tanzania Bara hasa katika Bandari ya Dar-es-Salaam. Suala hili limejadiliwa na kushughulikiwa katika vikao mbali mbali vya kutatua kero za Muungano. Katika kikao cha Mawaziri kilichofanyika mwezi Februari, 2011 ilielezwa kwamba Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) inaweka mfumo mpya wa kutathmini bidhaa (*Import Valuation Data base*), ambao ulitarajiwa kutekelezwa kwa majaribio kwa kipindi cha miezi sita ili kuwezesha kufanyika kwa tathmini halisi ya bidhaa kwa ajili ya malipo ya kodi. Hivyo, wizara inafuatilia utekelezaji wa utaratibu huo mpya ili kuweza kutoa taarifa hapo baadae.

Ukuzaji biashara:

Mhe. Naibu Spika, katika kuendeleza biashara hapa Zanzibar, Serikali ilianzisha maeneo ya Bandari Huru, Maruhubi na Uwanja wa Ndege, (katika mwaka 1998) kwa ajili ya kukuza biashara ya Mpito *(Transit Trade)* kama njia moja wapo ya kukuza biashara na kupunguza nakisi katika urari wa biashara. Takwimu zilizopo zinaonesha kuwa uagiziaji uliofanywa katika biashara ya Bandari Huru kwa kipindi cha mwaka 2006- 2010 ulikuwa ni USD 7.07 milion. Kwa upande wa usafirishaji nje *(re-export)* bidhaa zenye thamani ya USD 162,663 tu, ndizo ziliweza kusafirishwa nje ya nchi chini ya utaratibu wa bandari huru. Kwa upande mwengine jumla ya bidhaa zenye thamani ya USD 7.65 milion ziliuzwa katika soko la ndani kupitia fursa hiyo.

Mhe. Naibu Spika, kwa kuzingatia jumla ya mauzo yote chini ya utaratibu wa bandari huru ambayo ni USD 7.81 million, thamani ya bidhaa zilizouzwa katika soko la nje ni asilimia 2.08 tu. Kwa mwenendo huu ni dhahiri kuwa azma ya Serikali ya kukuza biashara ya nje kwa utaratibu wa bandari huru haionekani kutekelezwa ingawa imepanua wigo wa kodi za ndani. Kiambatisho Nam. 2 Jadweli Nam. 3 kinafafanua zaidi.

Hali ya Chakula na Mwenendo wa Bei:

Mhe. Naibu Spika**,** hali ya uzalishaji chakula ulimwenguni kwa mwaka 2010 haikuwa ya kuridhisha kutokana na nchi zinazozalisha kwa wingi mazao ya nafaka kukumbwa na majanga ya kimaumbile kama vile ukame na mafuriko. Nchi za Marekani, Urusi, Mashariki ya Mbali na Australia kwa nyakati tofauti, zilikumbwa na majanga hayo na kuathiri mwenendo wa bei za chakula ulimwenguni. Kadhalika kupanda kwa bei za mafuta

katika soko la dunia kumechochea zaidi kasi ya upandaji wa bei za chakula ulimwenguni. Kwa upande wa Nchi za Afrika Mashariki, gharama za uagiziaji bidhaa hasa chakula zimeongezeka zaidi kutokana na uharamia unaoendelea katika ukanda wa Mashariki ya Bahari ya Hindi.

Mhe. Naibu Spika, kwa upande wa Zanzibar, hali ya upatikanaji chakula kwa mwaka 2010 na katika kipindi cha Januari – Juni 2011 ilikuwa ya kuridhisha ingawa iliambatana na upandaji wa bei. Uagiziaji wa vyakula vikuu (Mchele, Ungangano, Sukari na Mafuta ya kupikia) uliendelea vizuri wakati ambapo uzalishaji wa ndani wa mazao mbali ya chakula nao uliendelea kuwa mzuri. Jadweli Nam. 4 na Jadweli Nam. 5 yanaonyesha mahitaji ya mwaka ya Mchele, Ungangano, Sukari na Mafuta ya Kupikia na uzalishaji wa ndani wa bidhaa za chakula.

Jadweli Nam.4

Matumizi ya Chakula kwa Mwaka (tani):

AINA	UAGIZIAJI	UZALISHAJI	JUMLA
Mchele	53,000	8,000	61,000
Sukari	30,000	0	30,000
Ungangano	42,000	0	42,000
Mafuta ya kupikia (Ltr)	5,000	3,000	8,000

Chanzo: *Wizara ya Kilimo na Maliasili – Zanzibar.*

Jadweli Nam. 5

Uzalishaji wa Ndani wa Chakula:

AINA YA CHAKULA	2009	2010
Mahindi	2,063	3,112
Mtama	457	572
Mpunga	26,980	31,000
Muhogo	195,674	229,284
Ndizi	100,873	102,258
Mbatata	53,596	58,958
Viazi vidogo	11,373	7,488
Majimbi	5,883	5,812
Njugu nyasa	320	432
Mbaazi	2,292	510
Kunde/Choroko	1,394	1,103
Jumla	**402,914**	**442,539**

Chanzo: Mtakwimu Mkuu wa Serikali.

Bei za Chakula Ulimwenguni:

Mhe. Naibu Spika, kama nilivyoeleza hapo awali kuwa uzalishaji wa chakula ulimwenguni kwa ujumla haukuwa wa kuridhisha na hivyo kusababisha upandaji wa jumla kwa mwenendo wa bei zake. Kutokana na hali hiyo, bei za bidhaa muhimu za chakula (Mchele, Sukari, Ungangano na Mafuta ya Kupikia) ambazo pia zinatumika kwa wingi hapa Zanzibar zilipanda kwa wastani mkubwa. Jadweli Nam. 6 hapa chini linaonesha mwenendo wa bei katika soko la uliwenguni kwa kipindi cha Oktoba Disemba 2010 na Januari – Juni 2011.

Jadweli Nam. 6:

Wastani wa bei za Bidhaa Duniani (USD/Ton):

Aina ya chakula	Okt. – Disemba	Jan. - Juni	Asilimia
Mchele	550	590	7.3
Sukari	760	900	18.4
Ungangano	440	540	22.7
Wastani wa bei	583.33	692.33	18.4

Chanzo: *Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko – Zanzibar.*

Mhe. Naibu Spika, kwa kuzingatia mwenendo wa bei wa hapo juu ni wazi kuwa mwenendo wa bei za chakula ulimwenguni umesababisha kuwepo kwa ongezeko la wastani wa bei za chakula katika soko la Zanzibar kwa bidhaa hizo. Hivyo, mwenendo wa bei za bidhaa hizo katika kipindi cha Oktoba 2010 hadi Juni 2011 umejitafsiri kwa kiasi kikubwa katika wastani wa ongezeko la bei za bidhaa hizo katika soko la Zanzibar. Kwa mfano, bidhaa ya mchele iliongezeka kwa wauzaji wa jumla kwa wastani wa asilimia 20.2, sukari asilimia 27.6. Kwa bei za rejareja wastani wa ongezeko la bei ulikuwa ni asilimia 20 kwa mchele na asilimia 38.4 kwa sukari (Jadweli Nam. 7(a) na 7(b)).

Mhe. Naibu Spika, katika taarifa zinazochambuliwa hapa, itabainika kuwa licha ya ongezeko kubwa la wastani wa bei ya ungangano (asilimia 22.7) katika soko la ulimwenguni, hapakuwepo na ongezeko la bei ya bidhaa hiyo katika soko la ndani. Sababu kubwa tunayoweza kuielezea hali hiyo ni kuwepo kwa uzalishaji wa ndani (Tanzania Bara) wa bidhaa hiyo na hivyo kuweza kujenga ushindani mkubwa ambao ulilazimisha waagiziaji wa bidhaa hiyo kupunguza viwango vya faida zao. Jadweli Nam. 7(a) na Nam. 7(b) yanaonyesha wastani wa mwenendo wa bei za jumla na rejareja kwa bidhaa muhimu za chakula kwa kipindi cha Oktoba 2010 hadi Juni 2011.

Jadweli Nam 7(a):

Wastani wa Bei za Chakula Kwa Jumla (50kg) katika Soko la Zanzibar":

akula	Oktoba	Novemba	Disemba	Januari	Februari	Machi	April	Mei	Juni	As m
hele	42,000	42,000	47,500	47,500	50,500	50,500	52,000	50,000	48,000	20
kari	58,000	58,000	68,000	68,000	72,0000	73,000	73,000	73,000	74,000	2
ga no	46,000	46,000	46,000	46,000	46,000	46,000	46,000	46,000	46,000	

Chanzo: *Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko – Zanzibar*

Jadweli Nam 7(b):

Wastani wa Bei za Reja Reja (Kilo Moja (1kg):

na ya akul a	Oktoba	Novemba	Desemba	Januari	Februari	Machi	April	Mei	Juni	Asi ia
hele	1000	1000	1100	1100	1150	1200	1,200	1,150	1,150	
kari	1300	1300	1550	1550	1750	1800	1,700	1,600	1,600	38
ga no	1000	1000	1000	1000	1000	1000	1,000	1,000	1,000	

Chanzo: *Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko – Zanzibar.*

Mhe. Naibu Spika, licha ya kuwepo kwa upandaji wa jumla wa wastani wa bei za bidhaa za chakula ulimwenguni, mwendo wa bei za bidhaa za chakula hapa Zanzibar, uliathiriwa pia na sababu nyengine ambazo zilitoa mwanya wa kuwepo kwa upandishaji wa bei za bidhaa mbali mbali. Baadhi ya sababu hizo ni kama ifuatavyo:-

i) Kuwepo kwa usimamizi dhaifu wa mwenendo wa biashara nchini.

ii) Kuwepo kwa ushirikiano wa kibiashara usiofaa ambapo wafanyabiashara hushirikiana kuweka bei kwa kuua ushindani.

iii) Kutengeneza uhaba wa makusudi wa bidhaa za chakula kwa lengo la kupandisha bei.

Haya yote Mhe. Naibu Spika, yameendelea kuyumbisha mwenendo wa bei kwa bidhaa za chakula katika kipindi tunachozungumzia.

Maendeleo ya Viwanda:

Mhe. Naibu Spika, Moja ya malengo makubwa ya Serikali katika kuanzisha viwanda hapa nchini ni kupunguza uagiziaji wa bidhaa kutoka nje ya nchi, kuongeza usafirifishaji wa bidhaa, kutumia malighafi za hapa nchini, kuongeza ajira pamoja na kuongeza mapato ya Serikali na hivyo kupunguza nakisi katika urari wa biashara.

Mhe. Naibu Spika, kama tunavyoelewa kuwa baada ya Mapinduzi Matukufu, Serikali ilivitaifisha viwanda mbali mbali na kujenga viwanda vipya vikiwemo viwanda vya maziwa, ngozi na viatu,

sigara, soda, chakula cha kuku, na kiwanda cha sukari cha Mahonda. Aidha, Serikali pia ilianzisha viwanda vidogo vidogo vikiwemo viwanda vya utengenezaji misumari, masufuria, rangi, nguo, mafuta ya nazi, kiwanda cha matunda, sabuni, maboksi, na waya za umeme.

Hata hivyo Mhe. Naibu Spika, baada ya kufanyakazi kwa muda mfupi, viwanda hivyo vilianza kudorora na hatimae kufa kutokana na sababu mbali mbali zikiwemo utaalamu mdogo wa uendeshaji wa viwanda hivyo; uhaba wa malighafi zinazopatikana hapa nchini kutokana na uzalishaji mdogo; uchache wa fedha za kigeni kwa ajili ya kuagizia malighafi kutoka nje mbinu dhaifu za kibiashara na gharama kubwa za uendeshaji katika sekta hiyo.

Mhe. Naibu Spika, kwa lengo la kutekeleza na kuimarisha azma ile ile ya kuendeleza viwanda, serikali ilifanya juhudi za kuifufua sekta hiyo kwa kushajihisha sekta binafsi kuwekeza katika eneo hili. Aidha katika mwaka 1992 serikali ilitangaza Maeneo Huru ya kiuchumi (EPZ) katika maeneo ya Amani, Fumba na Micheweni kwa ajili ya kuimarisha usarifu wa bidhaa kwa ajili ya usafirishaji nchi za nje. Kadhalika, serikali iliandaa Sera ya Viwanda ya mwaka 1998 na Sheria ya Ukuzaji Vitega Uchumi ya mwaka 2004 kwa madhumuni hayo hayo. Katika kuikuza sekta hiyo na kushajihisha wawekezaji kuekeza, Serikali pia imeweka mfumo wa kisheria kuhusu utoaji vivutio kwa kuendeleza uwekezaji kama ifuatavyo:

- Misamaha ya ushuru kwa vifaa vya ujenzi, mashine na mali ghafi za viwanda.
- Nafuu ya kodi ya mapato *(tax holiday).*
- Misamaha ya kodi kwa bidhaa zinazosafirishwa.

- Misamaha ya malipo (*fees*) kutoka Serikali za mitaa kwa bidhaa zinazozalishwa katika maeneo huru (EPZ).
- Kuajiri wataalam wa viwanda, nk.

Pamoja na kuchukuliwa kwa hatua zote hizo na kuweka mfumo wa vivutio mbali mbali, sekta ya viwanda bado imeendelea kuporomoka na kuwa na mchango mdogo katika muundo wa uchumi wa Zanzibar. Fundisho kubwa tunalolipata hapa Mhe. Naibu Spika, ni kuwa kuweka mfumo wa vivutio kwa ajili ya kuhamisha uwekezaji ni hatua muhimu lakini haitoshelezi kuweka mazingira mazuri ya uwekezaji. Tunapaswa kuangalia pia uendelezaji wa miundombinu muhimu kama vile umeme wa uhakika na nafuu, barabara bora, bandari na huduma imara, viwanja vya ndege vya kisasa na kuwepo kwa maji kwa ajili ya matumizi ya uzalishaji viwandani.

Mhe. Naibu Spika, kama nilivyoeleza hapo juu, mchango wa sekta hii bado ni mdogo kuweza kutegemewa kuleta mabadiliko ya muundo wa uchumi wa Zanzibar. Kwa mujibu wa Sensa ya Viwanda ya mwaka 2008, muundo wa sekta ya viwanda Zanzibar unajengwa kwa viwanda vidogo na vya kati 150 vilivyo ajiri wafanyakazi kuanzia 10 na kuendelea. Aidha, sekta hiyo ina viwanda vidogo vidogo *(small scale)* 2,050 vilivyoajiri wastani wa wafanyakazi chini ya kumi (10) kwa kila kiwanda.

Mhe. Naibu Spika, hivi sasa viwanda vinavyoendelea na kazi ya uzalishaji ni pamoja na Kiwanda cha Soda, Kiwanda cha Makonyo, Kiwanda cha Kaseti, Viwanda vya Samani, Viwanda vya Maji na Juisi, Kiwanda cha usagishaji nafaka, Viwanda vya Uchapishaji pamoja Viwanda vidogo vidogo vya Usindikaji, Tambi, Ushoni na utengenezaji Matufali. Muundo kamili wa Sekta ya viwanda vidogo na vya kati vilivyoajiri watu kumi (10)

na kuendelea, ambavyo kwa ujumla wake vimeajiri wafanyakazi 5,568, kama unavyoonekana katika Kiambatanisho Nam. 2 na Jadweli Nam. 8(a) na 8(b).

Mhe. Naibu Spika, thamani ya mchango wa sekta ya viwanda katika pato la Taifa kwa bei za sasa *(current price)* iliongezeka mwaka 2010 na kufikia Tshs. 39.5 bilioni kutoka Tshs. 36.1 bilioni mwaka 2009. Ongezeko hilo ni sawa na asilimia 9.4. Mchango wa sekta hii unatarajiwa kuongezeka kwa asilimia 14.08 mwaka 2011. Kasi ya ukuaji wa sekta hii ingawa imeongezeka kutoka asilimia 2.4 mwaka 2009 hadi asilimia 3.1 katika mwaka 2010 bado ni ndogo sana kuweza kuchochea ukuaji mkubwa wa uchumi. Mchango wa sekta hii umeongezeka kutoka asilimia 4.1 kwa mwaka 2009 hadi kufikia asilimia 4.2 katika mwaka 2010. Kiambatanisho Nam. 2 Jadweli Nam. 9 linafafanua zaidi.

Usarifu wa Bidhaa:

Mhe. Naibu Spika, Usarifu wa bidhaa hapa Zanzibar umegawika katika maeneo makubwa mawili; usarifu kwa ajili ya soko la ndani na ule unaofanywa kwa ajili ya soko la nje. Kwa upande wa usarifu kwa ajili ya usafirishaji katika soko la nje sehemu kubwa ya usarifu huo unafanyika katika Maeneo Huru ya Kiuchumi (EPZ). Usafirishaji wa bidhaa chini ya utaratibu wa Maeneo Huru umefikia USD 16.3 milioni kwa kipindi cha mwaka 2005 - 2010, sawa na wastani wa USD 2.72 milioni kwa mwaka. Usafirishaji kwa mwaka 2007 ulikuwa USD 4.1 milioni sawa na asilimia 25.1, wakati usafirishaji kwa mwaka 2010 ulipungua hadi kufikia USD 0.84 milioni sawa na asilimia 5.4 ya usafirishaji wote kama inavyoonekana katika Kiambatanisho Nam. 2 Jadweli Nam. 10.

Mhe. Naibu Spika, pamoja na juhudi kubwa za kuhuisha sekta ya viwanda kama zilivyoelezwa hapo awali, bado uwekezaji katika

Sekta za Viwanda hauridhishi hata kidogo. Kudorora kwa uwekezaji katika sekta hiyo kumetokana na baadhi ya sababu kuu zifuatazo:-

- Ukosefu wa maeneo maalum kwa ajili ya uwekezaji wa viwanda nje ya utaratibu wa EPZ,

- Ukosefu wa miundo mbinu ya umeme, maji, barabara katika maeneo ya EPZ ya Fumba na Micheweni na gharama kubwa za nishati.

- Huduma dhaifu za bandari ambazo zinasababisha meli kubwa za kuleta shehena kushindwa kuja Zanzibar,

- Kuondoshwa kwa vikomo vya uingizaji bidhaa *(Import quotas)* katika soko la Marekani na Ulaya, jambo ambalo lilitoa fursa kwa wazalishaji wa nchi za Ghuba na Asia kuweka viwanda katika nchi zao na kusafirisha bidhaa katika masoko hayo bila ya ukomo. Hali hii imeathiri baadhi ya nchi za Kiafrika kama Botswana kwa kuondokewa na wawekezaji kutoka China;

- Uwezo mdogo wa wafanyakazi (*productivity*) unaosababisha baadhi ya wakati miradi kushindwa kukidhi mahitaji ya wateja (*Orders*);

- Ukosefu wa ubora wa viwango na namba ya usafirishaji bidhaa (*export code*) hasa kwa bidhaa za chakula zinazopelekwa nchi za Ulaya,

Mhe. Naibu Spika, licha ya juhudi tulizofanya za kuendeleza sekta ya viwanda, juhudi hizo bado hazijafanikiwa sana. Hata hivyo, uendelezaji viwanda ni jambo la msingi katika kuiletea nchi yetu mageuzi ya kiuchumi na kuufanya uchumi wake uwe wa kisasa. Kadhalika, Mhe. Naibu Spika, Zanzibar ni mshiriki katika juhudi za kimaendeleo za kikanda ambazo shabaha yake kubwa ni kuimarisha biashara na maendeleo baina ya nchi wanachama. Kwa ajili hiyo, Zanzibar inapaswa kuwa mshiriki imara ili kufaidika na hatua hizo za mtangamano (*regional integration*). Hivyo, kwa kuzingatia umuhimu huo, ni lazima kuchukua hatua za kujiandaa na kuimarisha uwezo wetu wa kuweza kuwa washiriki imara katika biashara na uchumi wa kikanda.

Mhe. Naibu Spika, kama nilivyoeleza hapo awali kuwa, Serikali ilichukua hatua mbali mbali za kuendeleza viwanda ingawa mafanikio yake hayakuwa mazuri sana. Kwa madhumuni hayo hayo na kwa lengo la kuitayarisha vizuri Zanzibar kuwa mshiriki thabiti katika biashara na uchumi wa kikanda, Serikali imeanzisha juhudi mpya za kuiwezesha Zanzibar kuwa mshiriki imara katika mfumo wa Soko la Pamoja la Afrika Mashariki (*East African Community Common Market)* na katika mfumo wa Soko Huru (*Free Trade Area*) la Jumuiya ya Maendeleo ya nchi za Kusini mwa Afrika (*Southern African Development Community – SADC*). Ili kutayarisha mkakati wa maandalizi hayo na pia kuweza kufanya maamuzi makini, Serikali imeanzisha utafiti wenye lengo la kubainisha uwezekanao wa kuifanya Zanzibar kuwa eneo tengefu la kiuchumi *(Special Economic Zone – SEZ)* ndani ya mfumo wa Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Taarifa za awali za utafiti huo Mhe. Naibu Spika, zinabainisha wazi umuhimu wa Zanzibar kujiandaa ipasavyo ili kushiriki kikamilifu katika biashara za kikanda na za kimataifa. Kati ya nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki, Zanzibar

imejitokeza kuwa nchi ya mwisho katika usafirishaji bidhaa nchi za nje ambapo kiwango chake kimebainika kuwa ni asilimia 3.38 ya Pato la Taifa wakati ambapo nchi za Kenya na Uganda zina asilimia 14.78 na 17.16 kama inavyoonekana katika Jadweli hapa chini.

EAC Partner Countries	Import (US$ Mn)	Export (US$ Mn)	GDP Nominal (US$ Mn)	Imports as % of GDP
Kenya	10,207	4,463	30,200	33.8
Uganda	3,844	2,700	15,736	24.4
Rwanda	1,204	192	5,064	23.7
Burundi	402	62	1,325	30.3
Tanzania	6,296	2,368	21,623	29.1
Zanzibar	**81**	**20**	**586**	**13.7**

Mhe. Naibu Spika, Eneo Tengefu la Kiuchumi (SEZ) ni mkakati maalum wa maendeleo ya uchumi na biashara wenye tafsiri pana ambapo shughuli mbali mbali za kiuchumi hutekelezwa kwa utaratibu maalum kwa lengo la kuendeleza usarifu wa bidhaa kwa ajili ya usafirishaji, kujenga miundo mbinu ya kisasa, kuimarisha huduma za kijamii na makaazi ya kisasa, kurahisisha na kuimarisha taratibu za kuanzisha biashara na kuingiza teknolojia za kisasa.

Hivyo, shughuli za sasa za Maeneo Huru na Bandari Huru zitakuwa ni moja wapo ya shughuli zitakazoendeshwa ndani ya utaratibu wa eneo tengefu. Kwa ujumla muundo wa shughuli za kiuchumi katika eneo tengefu (SEZ) zinajumuisha Maeneo Huru

ya uzalishaji bidhaa (EPZ), Bandari Huru (*Free Port*) na Eneo Huru la Biashara (*Free Trade Zone – FTA)*, Maeneo Maalum ya Kukuza Sayansi na Teknolojia (*Science and Technology Parks*), Eneo Huru la Biashara za Mazao ya Kilimo (*Agricultural Free Zone*), Maeneo ya Kukuza Utalii (*Tourism Development Zone*), Maeneo ya jumla ya Uwekezaji Viwanda (*Industrial Parks*) na mengineyo kama vile teknolojia ya habari na mawasiliano (ICT), maeneo ya ukuzaji ujasiriamali (*Business Incubation*) n.k.

UTEKELEZAJI WA BAJETI YA MWAKA 2010/2011:

Mhe. Naibu Spika, baada ya kutoa maelezo hayo ya utangulizi, hali ya biashara ulimwenguni, athari zake kwa mwenendo wa biashara katika soko la Zanzibar na mapitio ya hali ya sekta ya viwanda, naomba sasa kufanya mapitio ya utekelezaji wa bajeti na malengo ya Wizara kwa mwaka 2010 – 2011.

Mhe. Naibu Spika, Kama nilivyogusia hapo awali, Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko ni moja wapo ya vyombo vya Serikali vilivyokabidhiwa jukumu la kusimamia utekelezaji wa malengo ya maendeleo ya sekta kuu za uchumi wa Zanzibar ambazo ni biashara, uendelezaji viwanda na ukuzaji masoko. Katika kutekeleza majukumu hayo, wizara kwa kutumia muundo ulioambatishwa katika Hotuba hii inajihusisha na uimarishaji mazingira ya biashara, maendeleo ya viwanda, kuimarisha misingi ya ushindani wa kibiashara, ubora wa bidhaa, kukuza ushirikiano wa kikanda na kimataifa kuhusu biashara na maendeleo yake.

Mhe. Naibu Spika, katika kipindi cha mwaka 2010/2011 wizara ilipangiwa kutumia jumla ya Tshs. 3,729.0 milioni ambapo jumla ya Tshs. 1,939.0 milioni kwa ajili ya matumizi ya kazi za kawaida na Tshs. 1,790.0 milioni kwa kazi za maendeleo. Matumizi hayo

yalipangwa kwa kuzingatia muundo wa iliyokuwa Wizara ya Utalii, Biashara na Uwekezaji. Baada ya mabadiliko ya muundo wa Wizara na kuwa Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko bajeti yake imekuwa kama ifuatavyo:

	Tshs. (Mil.)
Kazi za Kawaida	1,239.0
Kazi za Maendeleo	1,200.0
Jumla:	**2,439.0**

Mchanganuo wa bajeti kwa muundo wa zamani unafafanuliwa katika **Kiambatisho Nam. 2 Jadweli Nam. 11(a)** na **11(b)**.

Kadhalika, mchanganuo wa bajeti ya Wizara kwa muundo wa sasa wa Wizara unafafanuliwa zaidi katika **Jadweli Nam. 12(a)** na **12(b).**

Mhe. Naibu Spika, katika kipindi hicho, wizara ilipangiwa pia kukusanya mapato ya Tshs. 23.53 milioni. Hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2011, wizara iliweza kukusanya jumla ya Tshs. 28.65 milioni ikiwa ni ongezeko la asilimia 22 ya lengo lililowekwa.

Matumizi:

(i) **Kazi za Kawaida:**

Mhe. Naibu Spika, hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2011, wizara iliweza kupatiwa asilimia 94.5 ya fedha

zilizopangwa kwa matumizi ya bajeti ya kazi za kawaida. Mwenendo wa upatikanaji huo wa fedha unaonekana katika **Jadweli Nam. 12(a)** hapa chini.

(ii) **Kazi za Maendeleo:**

Kwa upande wa matumizi ya maendeleo Mhe. Naibu Spika, jumla ya Tshs. 1,132.4 milioni sawa na asilimia 94.4 ziliingizwa kwa ajili hiyo. Mchanganuo wa matumizi hayo ni kama unavyoonekana katika **Jadweli Nam. 12(b)** hapa chini.

Jadweli Nam.12(a):

Matumizi kwa kazi za Kawaida Julai 2010 - Juni 2011:

Idara	Makisio ya Bajeti 2010 - 2011	Kilichoingi-zwa Julai 2010 – Juni 2011	Asilimia ya Makisio ya mwaka
Idara ya Mipango na Sera (04)	659,035,632	638,773,339	96.92
Idara ya Biashara na Masoko (06)	192,125,911	161,172,005	83.89
Idara ya Maendeleo ya Viwanda (05)	80,951,598	77,535,598	95.78
Afisi Kuu Pemba (03)	183,647,394	183,647,394	100.0
Baraza la Biashara	200,000,000	182,530,000	91.27
JUMLA	**1,315,760,535**	**1,243,658,336**	**94.52**

Jadweli Nam.12(b):

Matumizi kwa kazi za Maendeleo Julai 2010 – Juni 2011:

Mradi	Makisio Ya Bajeti Kwa Mwaka 2010-2011	Kilichoingizwa	Asilimia Ya Fedha Zilipatikana
Mapitio ya sheria zinazoendana a biashara	65,000,000	40,000,000	61.5
Kuimarisha mazingira ya biashara	500,000,000	463,447,365	92.6
Mpango wa kuendeleza Viwanda idogo vidogo (SMEs)	635,000,000	629,000,000	99.0
JUMLA	**1,200,000,000**	**1,132,447,365**	**94.3**

Mhe. Naibu Spika, matumizi yaliyofanywa kwa upande wa bajeti ya maendeleo yalielekezwa katika utekelezaji wa malengo kumi na mbili (12) yaliyopangwa kutekelezwa na wizara katika kipindi hicho. Malengo hayo yanaorodheshwa katika **Kiambatisho Nam. 3** na ambapo ufafanuzi wake unafanywa kama ifuatavyo:

(i) **Ukuzaji Biashara:**

Mhe. Naibu Spika, eneo hili la malengo ya wizara lilijumuisha utekelezaji wa hatua mbali mbali zilizolenga katika kukuza biashara kwa ujumla wake. Hatua hizo ni kwanza, kuimarisha mazingira ya biashara kwa kufanya mapitio ya Sheria za biashara ambazo ni:-

a) Sheria ya Biashara Nam. 4 ya Mwaka 1989;

b) Sheria ya Mizani na Vipimo Nam. 4 ya mwaka 1983;

c) Sheria ya Ushindani na Kumlinda Mtumiaji Nam. 2 ya Mwaka 1995.

Kwa ujumla, Sheria hizi zimeandikwa upya ili kukidhi mazingira ya sasa ya biashara ikiwemo uendeshaji uchumi na biashara kwa kuzingatia misingi ya nguvu za soko, maendeleo ya teknolojia na kuzigeuza sheria kuwa rafiki wa kukuza uchumi na ustawi wa biashara. Kadhalika, katika kuendeleza hatua hizo, wizara inaendelea na mapitio ya sheria ya Leseni Nam. 4 ya 1983 kwa dhamira ya kuweka mfumo, taratibu na sheria mpya ya leseni itakayohamasisha ukuzaji biashara. Mapitio hayo pia yanatarajiwa kukamilika katika mwezi wa Septemba, mwaka 2011. Vile vile, wizara imeweza kuandaa Sheria ya Viwango ambayo utekelezaji wake unaotarajiwa kuanza hivi karibuni utaimarisha usimamizi wa biashara nchini kwa kuzingatia viwango vya bidhaa vinavyohitajika.

Mhe. Naibu Spika, katika juhudi za kuhakisha kuwa Zanzibar inashiriki na kufaidika na mfumo wa kimataifa wa uchumi na biashara, wizara imekuwa ikishiriki katika majadiliano ya ngazi za kimataifa kwa lengo hilo. Moja kati ya mipango ya kimataifa ambapo Zanzibar inafaidika ni ule unaoratibiwa na Shirika la Biashara la Kimataifa (*WTO*) ambao lengo lake ni kuziwezesha nchi changa kushiriki kikamilifu katika mfumo wa uchumi na biashara wa dunia. Kwa madhumuni hayo, Shirika hilo lilianzisha mpango wa Misaada ya Kiufundi (*integrated framework for trade-related technical assistance*) kwa nchi wanachama wa jumuiya hiyo. Mpango huo ulianza mwaka 1996 na kuhusisha wafadhili mbali mbali wakiwemo Mkutano wa Umoja wa Mataifa kuhusu Biashara na Maendeleo (*UNCTAD*), Benki ya Dunia, Shirika la Biashara la Kimataifa (*WTO*), Mpango wa Maendeleo

wa Umoja wa Mataifa (*UNDP*), Shirika la Fedha la Kimataifa (IMF) na Taasisi ya Kimataifa ya Biashara (*ITC*).

Mhe. Naibu Spika, Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni moja kati ya nchi 12 za awali zilizofaidika na msaada huo baina ya mwaka 1999 na 2000. Kutokana na ushiriki huo Tanzania ilisaidiwa katika mradi wa kuimarisha Mazingira ya Biashara (*Business Environment Strenghtening for Tanzania – BEST*) ambao ulianza Disemba mwaka 2003. Zanzibar imefaidika katika mpango huo wa *BEST* ambapo sasa mpango huo unagharimia mapitio ya sheria zinazohusu biashara kwa madhumuni ya kuimarisha mazingira ya kufanya biashara.

Aidha, Mhe. Naibu Spika, Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Shirika hilo chini ya mradi huo zimekubaliana kuimarisha zaidi mafanikio yaliyopatikana katika utekelezaji wa mpango wa awali kwa kutekeleza hatua ya juu zaidi ya mradi huo ili kuimarisha biashara. Zanzibar kwa upande wake, imefaidika kwa kupata mafunzo ya muda mrefu na muda mfupi yanayohusiana na mambo ya kuendeleza miradi (*Project Cycle Management*) na mbinu za Majadiliano (*negotiations skills*)

Mhe. Naibu Spika, katika hatua hii, Zanzibar itafaidika pia na utekelezaji wa mpango huu kwa kugharimia mambo yafuatayo:

a. Kutoa mafunzo kuhusu utumiaji wa mbinu za mali bunifu (*intellectual Property*) kwa lengo la kujenga uwezo wa uzalishaji na kuimarisha tija ya kibiashara kwa mazao yanayosafirishwa nje ya nchi ili kupata faida kubwa zaidi.

b. Kuweka madaraja ya hoteli za kitalii (*Hotel Classification*) yenye lengo la kuweka alama

(*stars*) za kimataifa kwa mahoteli ya Zanzibar ili kuhimili ushindani wa kimataifa

c. Kuanzisha kitengo cha uratibu cha utekelezaji wa mpango huo hapa Zanzibar;

Hivi sasa Mhe. Naibu Spika,tayari Zanzibar inajadiliana na Shirika hilo la Mali Bunifu Duniani (*World Intellectual Property Organization – WIPO*) na wadau wengine ili kuiwezesha kutoa utambulisho maalum (*branding*) kwa karafuu zake kufaidika zaidi na zao hili, kupambana na magendo na uuzaji holela wa zao hilo bila ya Zanzibar kufaidika na uuzaji huo.

Mhe. Naibu Spika, **k**atika juhudi hizo za kuendeleza na kukuza biashara, Serikali iliendelea kushiriki majadiliano ya kiuchumi na biashara baina ya Jumuiya ya Afrika Mashariki (*EAC*) na Jumuiya ya nchi za Ulaya (*EU*) chini ya mkataba wa Ubia wa kiuchumi (*Economic Partnership Agreement – EPA*). Kama tunavyoelewa kuwa nchi za Jumuiya ya Afrika ya Mashariki (*EAC*) ziliamua kuanzisha majadiliano haya na Jumuiya ya Ulaya (*EU*) kama kundi moja (*configuration*) na kusaini Mkataba wa muda ujulikanao kama Mkataba wa Mpito wa Ubia wa Kiuchumi (*Framework for Economic Partnership Agreement – FEPA*). Mkataba huo ulifikiwa ili kupata muda wa kuanzisha majadiliano ya mkataba kamili wa ushirikiano wa kiuchumi (*Economic Partnership Agreement*) na Jumuiya ya Ulaya (EU) kufikia Novemba, 2007.

Lengo la kuwa na Mkataba huo ni kutimiza masharti ya WTO ya kuondoa uhusiano wa kibiashara wa upendeleo uliokuwepo kwa miaka mingi baina ya Jumuiya ya Ulaya (*EU*) na kundi la nchi za *ACP* (*African Carribean and Pacific).* Awali, WTO iliridhia kuanzishwa kwa uhusiano huo wa kibiashara kwa kipindi maalum

ambacho kilimalizika mwaka 2000. Chini ya utaratibu huo, nchi za *ACP* ziliruhusiwa kuingiza bidhaa zao katika soko la nchi za Jumuiya ya Ulaya bila ya 'Ushuru'.

Mhe. Naibu Spika, kundi la nchi za *ACP* na zile za Jumuiya ya Ulaya zilitakiwa kukubaliana utaratibu mpya wa kibiashara ambao utaondokana na utoaji upendeleo kwa bidhaa za nchi za *ACP* na kwamba utaratibu huo mpya uwe umekamilika ilipofika Julai, 2007. Majadiliano hayo yamekuwa na changamoto nyingi ambazo hadi sasa bado hakujawa na maendeleo mazuri ya majadiliano hayo kutokana na tofauti za kimtazamo baina ya pande hizo kuhusu ushirikiano wa kiuchumi na maendeleo.

Mhe. Naibu Spika, misingi ya majadiliano ya *EPA* ni kuimarisha mashirikiano ya kikanda, kuleta maendeleo endelevu, kupunguza umasikini kwa kuzisaidia nchi maskini za *ACP* kupata misaada na kuondoa vikwazo vya ndani vya uzalishaji na biashara za kimataifa. Kutokana na misingi hiyo, Tanzania imeingia katika majadiliano ya *EPA* kwa mategemeo kuwa itapata msaada wa kuiwezesha kukabiliana na changamoto za uzalishaji na usambazaji (*production and supply side constraints*). Majadiliano hayo yalitarajiwa kuwa maeneo makubwa mawili ambayo ni ushirikiano wa uchumi na maendeleo (*economic and development cooperation*) na ufunguaji masoko (*market access*). Hata hivyo, majadiliano hayo yalisita mwezi Juni mwaka 2010 kutokana na kutofikiwa makubaliano katika masuala ya ushirikiano wa kiuchumi na maendeleo. Hivi sasa, nchi hizo zinatayarisha mwelekeo (*road map*) kwa ajili ya kuanza tena majadiliano hayo.

Mhe. Naibu Spika, pili wizara iliendelea na matayarisho ya utekelezaji wa mradi mkubwa wa kujenga uwanja wa kimataifa wa maonesho ya kibiashara. Huu ni mradi mkubwa ambao unahitaji uwekezaji mkubwa. Hivi sasa tayari wizara

imetayarisha maelezo ya awali ya kuwezesha kupata mshauri mwelekezi wa kufanya upembuzi yakinifu, matumizi ya ardhi iliyopo, kutayarisha michoro ya kihandisi na usanifu wake na pia kuandaa gharama za mradi wote.

Lengo la mradi huu Mhe. Naibu Spika, ni kuchangia katika juhudi za kuimarisha mazingira na kukuza biashara na kuiweka Zanzibar katika ramani ya nchi zenye uwezo wa kuandaa maonesho ya biashara ya kimataifa. Wizara inaendelea na utekelezaji wa mradi huu licha ya uchache wa raslimali uliyopo.

Mhe. Naibu Spika, Tatu, wizara ilianza kuchukua hatua za kuiandaa Zanzibar kushiriki na kufaidika kikamilifu na mtangamano wa kiuchumi hasa *SADC* na *EAC*. Kama nilivyoeleza hapo awali kuwa Serikali inafanya utafiti wa kuiwezesha kufanya maamuzi makini katika suala la kuigeuza Zanzibar kuwa eneo tengefu la kiuchumi inatarajiwa kuwa utekelezaji wa hatua na azma hii utaiwezesha Zanzibar kujenga msingi muhimu wa uzalishaji na hivyo kuimarisha uwezo wake wa ushindani katika Soko la Afrika Mashriki na *SADC*.

Mhe. Naibu Spika, eneo la nne, lililozingatiwa katika hatua za kuimarisha mazingira ya biashara ni Ukaguzi. Kazi ya ukaguzi ni moja kati ya majukumu muhimu ya kisheria yanayotekelezwa na Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko kwa madhumuni ya kusimamia mwenendo wa biashara, maslahi na usalama wa watumiaji. Katika kipindi cha Julai 2010 – Juni, 2011 ukaguzi ulifanyika katika maeneo yafuatayo:-

(i) Ukaguzi wa Mizani;
(ii) Ukaguzi wa Vituo vya Mafuta;
(iii) Ukaguzi wa Maghala;
(iv) Ukaguzi wa bekari;

(v) Ukaguzi wa Maduka ya kawaida; na

(vi) Ukaguzi wa maduka ya 'Super Market'.

Matokeo ya ukaguzi katika kipindi hicho yanaonekana hapo chini:-

ENEO	**IDADI**
Mizani	1,855
Vituo vya Mafuta	37
Maghala	188
Bekari	45
Maduka ya kawaida	1,801
Maduka ya 'Super Market'	3

Aidha, ukaguzi huo ulibaini bidhaa kadhaa zisizofaa kwa matumizi ya binaadamu ambapo wizara ilichukua hatua ya kuziangamiza bidhaa hizo ambazo zilikuwa na thamani ya Tshs. 5.50 milioni. Bidhaa hizo ni pamoja na maharage, mchele, unga wa sembe, mafuta ya kupikia na bidhaa nyengine mchanganyiko kama vile majani ya chai, siagi, achari, dawa za meno, tende, '*cheeze'* na bidhaa nyengine za makopo.

Mhe. Naibu Spika, kwa madhumuni ya kuimarisha ukaguzi kwa mwenendo wa biashara ya mafuta ya nishati; wizara ilichukua hatua ya kifaa maalum kinachojulikana kama '*Prover'* kwa ajili ya ukaguzi wa ujazo kwa bidhaa za mafuta ya nishati katika vituo vya kuuzia mafuta, magari ya kubebea mafuta na katika matangi ya chini au juu ya ardhi ili kuhakikisha kuwa vipimo vya ujazo wa bidhaa hizo unazingatiwa kwa mujibu wa sheria. Kadhalika, wizara inafanya maandalizi ya kwenda hatua nyengine zaidi ya kuimarisha ukaguzi wa ubora wa bidhaa hizo ili kudhibiti uchakachuaji wa bidhaa za mafuta. Udhibiti wa ujazo na ubora wa bidhaa hizo utaimarisha uwezo wa Serikali wa kukusanya kodi

zake kwa ufanisi zaidi na kuwapatia watumiaji bidhaa zenye ubora unaostahili.

Mhe. Naibu Spika, kwa upande wa kuimarisha udhibiti na usimamizi wa mwenendo wa biashara na bei za bidhaa mbali mbali, Serikali imechukua vile vile hatua za kisoko (kuingilia kati bila ya kuathiri misingi ya uchumi wa nguvu za soko) kwa kuandaa kanuni na taratibu mpya za ufanyaji biashara nchini. Kanuni hizo zinahusu taratibu za uagiziaji na usafirishaji bidhaa pamoja na kanuni za kufuatilia mwenendo wa biashara na kumlinda mtumiaji. Chini ya utaratibu huo mpya bei za bidhaa hasa chakula sasa zitapangwa kwa kushirikiana baina ya Serikali na wafanyabiashara wenyewe baada ya kuzingatia gharama zote na kwamba Serikali itatangaza bei za bidhaa hizo hasa bei za chakula na kubainisha viwango vya faida kuanzia muagiziaji hadi muuzaji reja reja wa bidhaa inayohusika. Chini ya utaratibu huu, itakuwa ni makosa kwa mfanyabiashara kuuza bidhaa kwa bei tofauti na ile iliyotangazwa na Serikali baada ya makubaliano na wafanyabiashara wenyewe.

(ii) **Ukuzaji wa Masoko:**

Maonesho ya Biashara:

Mhe. Naibu Spika, hili ni eneo jengine ambalo wizara ililifanyia kazi kwa lengo la kutafuta masoko ya ndani na nje ili kuwasaidia Wafanyabiashara na wazalishaji wadogo wadogo. Wizara iliratibu ushiriki wa wafanyabiashara wa Zanzibar katika maonyesho ya Biashara ya Kimataifa ya SabaSaba **(***DITF*) kwa lengo la kuwawezesha kuzitangaza bidhaa zao na kujifunza kutoka kwa wenzao jinsi ya kupata masoko mapya. Jumla ya wafanyabiashara 50 waliwezeshwa na kushiriki maonesho hayo kwa mwaka 2010/2011.

Mhe. Naibu Spika, juhudi zetu za ukuzaji masoko na ujasiriamali zimeweza kupiga hatua nyengine ya maendeleo hivi karibuni baada ya kuungwa mkono na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dk. Jakaya Mrisho Kikwete. Naomba kuliarifu Baraza lako tukufu, Mhe. Naibu Spika, kuwa katika ziara yake ya kutembelea mabanda ya Maonesho ya Saba Saba hivi karibuni Mhe. Rais wa Jamhuri ya Muungano aliahidi kuchangia Tshs. 200.0 milioni kwa ajili ya kuendeleza ujasiriamali Zanzibar. Naomba kuchukua fursa hii Mheshimiwa Spika kumshukuru kwa dhati Mhe. Rais wa Jamhuri ya Muungano na kumuahidi kuwa fedha hizo zitatumika kama alivyokusudia na kwamba Wizara yangu itaandaa utaratibu wa namna bora ya kuendeleza ujasiriamali kwa kutumia fedha hizo na pia kuufanya utaratibu huo kuwa endelevu. Ni matumaini yangu vile vile, kuwa Mhe. Rais wa Zanzibar ataunga mkono juhudi hizi ili kujenga msingi bora wa kuimarisha ujasiriamali hapa Zanzibar.

Mhe. Naibu Spika, hatua hii ya Serikali ya kuwasaidia wajasiriamali na wafanyabiashara wadogo wadogo kushiriki katika maonyesho hayo imesaidia kuwakutanisha na wanunuzi wa bidhaa mbali mbali na kuanzisha uhusiano wa kibiashara. Hata hivyo, bado wajasiriamali na wafanyabiashara wengi wanaoshiriki wanakabiliwa na changamoto nyingi hasa zinazohusiana na uwezo mdogo wa uzalishaji (*supply side constraints*) kukidhi mahitaji ya soko la bidhaa wanazozionyesha na kwa viwango vinavyokubalika. Kutokana na kuwa na uwezo mdogo wa kuzalisha bidhaa wanazozionesha, wengi wa wajasiriamali na wafanyabiashara hao huchukulia ushiriki wao katika maonyesho hayo kama ni fursa ya kupata soko la kuuzia bidhaa zao na kusubiri tena kwa mwaka mwengine kupata fursa nyengine. Hii ni changamoto inayotukabili kwa sasa na kwamba Wizara yangu itaelekeza nguvu zake katika kusaidia wajasiriamali hao ili

waweze kujenga misingi ya kujitegemea baada ya kupewa msaada na Serikali.

Mhe. Naibu Spika, ushirikiano wa kimataifa kuhusu biashara ni eneo jengine ambalo Wizara iliifanyia kazi kwa madhumuni ya kuimarisha uchumi na kupanua masoko ya bidhaa. Nchi za Afrika Mashariki (*EAC*) na zile zilizo wanachama wa nchi za Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (*SADC*) zimeamua kuanzisha Jumuiya hizo kwa malengo ya kukuza uchumi na biashara. Zanzibar kupitia Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni mwanachama wa Jumuiya za *SADC* na Afrika Mashariki (*EAC*) kwa madhumuni ya kuimarisha uchumi wake na kukuza biashara.

Kwa madhumuni hayo Mhe. Naibu Spika, wizara iliendelea kushiriki katika majadiliano ya kuandaa Kanuni na Taratibu za kuendesha Itifaki ya Soko la Pamoja la Afrika Mashariki ambayo Itifaki hiyo ilikamilika na kuwekwa sahihi mwezi Novemba, 2009 na kuanza utekelezaji wake mwezi Julai 2010. Hivyo, majadiliano ya matayarisho ya kanuni za uendeshaji wa Itifaki hiyo kama vile kanuni za biashara ya huduma (*trade in sevices*), hifadhi ya jamii (*Social Security*) na mzunguko huru wa wafanyakazi yalimalizika mwezi Februari 2011. Kuanzishwa kwa Itifaki ya Soko la Pamoja la Afrika Mashariki ambayo inaruhusu mzunguko huru wa watu, wafanyakazi, huduma, bidhaa na mitaji kunatoa fursa kubwa za biashara na masoko kwa bidhaa zinazozalishwa hapa Zanzibar.

Mhe. Naibu Spika, vile vile katika kipindi hiki, Wizara ilishiriki katika Mikutano ya Baraza la Mawaziri wa Biashara na Viwanda wa Nchi za Maendeleo ya Kusini mwa Afrika (*SADC*) na ya Wakuu wa Nchi hizo (*Summit*) na kujadili masuala yanayohusu biashara ya huduma na kuanzishwa kwa Eneo Huru la Biashara la Pande Tatu (*EAC-SADC-COMESA-Tripartite FTA*). Suala hili Mhe. Naibu Spika,ni muhimu sana na linatarajiwa kuongeza fursa

za kiuchumi na biashara na vile vile kupanua masoko na kukuza biashara kwa Zanzibar. Hata hivyo, changamoto kubwa itakayotukabili ni jinsi wafanyabiashara wetu na wananchi kwa jumla watakavyoweza kuchangamkia na kutumia fursa hizo za masoko kwa kuzalisha bidhaa zenye ubora na kuhimili ushindani pamoja na kukidhi mahitaji ya soko.

(iii) **Uendelezaji Viwanda:**

Mhe. Naibu Spika, eneo hili la malengo ya wizara linajumuisha utekelezaji wa hatua mbali mbali zenye shabaha ya kujenga mazingira bora yatakayowezesha kushamiri kwa uwekezaji katika sekta ya viwanda. Hatua hizo ni kwanza, kufanya mapitio ya sera ya viwanda na kuandaa mkakati wa kuendeleza viwanda. Licha ya kuendelea na utafiti wa kutathmini uwezekano wa kuifanya Zanzibar kuwa eneo tengefu la kiuchumi Wizara imefanya matayarisho ya awali kwa ajili ya kufanya mapitio ya sera ya sasa ya viwanda (1998- 2008) na kuandaa mkakati wa maendeleo ya viwanda Zanzibar (*Zanzibar Industrial Development Strategy).*

Mkakati huo Mhe. Naibu Spika, utaonesha na kubainisha aina ya viwanda vitakavyoendelezwa kwa kuzingatia raslimali zilizopo hapa Zanzibar, vivutio vitakavyohitajika kwa uendelezaji huo na pia kuainisha maeneo (*Locations*) ya viwanda.

Mhe. Naibu Spika, mapitio ya sera ya sasa ya Maendeleo ya Viwanda yanalenga katika kutathmini mafanikio, matatizo na changamoto zilizojitokeza katika utekelezaji wa sera hiyo. Hivyo mapitio hayo yanaokusudiwa kuweka msingi wa kuandaa mkakati mpya wa kuelekeza rasilimali na juhudi za Serikali katika uendelezaji wa Sekta hiyo ili iweze kutoa mchango mkubwa katika pato la taifa na hivyo kuiwezesha Serikali kufikia malengo

yake ya kuwapatia wananchi wake ajira, kuongeza mapato na kubadilisha muundo wa sasa wa uchumi. Kadhalika, mkakati huo unatarajiwa kujenga mfumo wa kuhamasisha sekta binafsi kuanzisha viwanda vidogo vidogo na vya kati vinavyotumia malighafi zinazopatikana nchini kwa kuzalisha bidhaa zinazokubalika katika masoko ya ndani na nje ambazo pia zitasaidia katika kukuza uchumi na kustawisha kasi ya ongezeko la kipato.

Pili, Mhe. Naibu Spika, katika mwaka uliopita, wizara ilichukua hatua zilizolenga katika ukuzaji wa ujasiriamali kwa kuandaa mafunzo mbali mbali ya ujuzi, kuandaa mfumo wa kitakwimu wa kuainisha maeneo walipo wajasiriamali hao na aina ya shughuli za uzalishaji wanazozifanya; na pia kubainisha matatizo na changamoto zinazowakabili.

Mhe. Naibu Spika, katika utekelezaji wa hatua hizo mbali mbali wizara imebaini kuwa hivi sasa wajasiriamali waliowengi wanakabiliwa na matatizo mengi yanayokwaza maendeleo ya uzalishaji na biashara zao. Matatizo hayo ni pamoja na ubora duni wa bidhaa zinazozalishwa, udhaifu katika ufungashaji (*packaging*), udhaifu katika mbinu za kibiashara na ujasiriamali, ukosefu wa taarifa za masoko, upatikanaji mdogo wa mitaji na uwezo mdogo wa kuzalisha kama nilivyoeleza hapo awali hata pale soko linapopatikana.

Mhe. Naibu Spika, ili kuwawezesha wajasiriamali hao kukabiliana na matatizo na changamoto hizo, Wizara iliandaa na kuwapatia mafunzo wajasiriamali 84 Unguja na Pemba katika maeneo ya usindikaji bidhaa (*food processing*), ujasiriamali (*entrepreneuriship*), kuongeza thamani ya bidhaa (*value addition*) na mbinu za kuendeleza biashara (*business development skills*).

Mafunzo hayo Mhe. Naibu Spika, yamewasaidia baadhi ya wajasiriamali kuzalisha bidhaa kwa viwango vinavyokubalika, kuimarisha vifungashio kulingana na mahitaji ya soko pamoja na kuimarisha mfumo wa uwekaji kumbukumbu zao za kibiashara zikiwemo taarifa za uzalishaji, fedha, gharama za uzalishaji na uuzaji.

Mhe. Naibu Spika, uchapishaji na usambazi wa vijarida 2,000 vya Sera ya Maendeleo ya Viwanda na biashara ndogo ndogo na kati (*SMEs*) kwa lunga nyepesi (*popular version*) ulichangia pia katika ukuzaji ujasiriamali kwa wajasiriamali hao kuweza kufahamu Sera hiyo kwa urahisi na kuitekeleza.

Mhe. Naibu Spika, Tatu, wizara ilichukua hatua mbali mbali za ukaguzi na kutathmini maendeleo ya viwanda. Katika mwaka wa fedha 2010/2011, jumla ya viwanda 24 vilifanyiwa ukaguzi kwa lengo la kubainisha mafanikio na matatizo yaliyopo na pia changamoto zinazokabili sekta ya viwanda hapa Zanzibar. Viwanda vilivyokaguliwa ni vya vinywaji baridi, samani, uzalishaji sukari, chumvi, usarifu wa mazao ya baharini (samaki, dagaa), usarifu wa mazao ya kilimo (mpunga), utengenezaji wa karatasi laini (*tissue*) na uzalishaji wa gesi. **Kiambatisho Nam. 2 Jadweli Nam. 13** kinatoa ufafanuzi zaidi.

Kwa ujumla, ukaguzi huo umebaini kuwa viwanda hivyo vinakabiliwa na matatizo mengi yakiwemo gharama kubwa za umeme, upatikanaji wa mitaji, ushindani usiofaa unaotokana na bidhaa kama hizo zinazoingizwa kutoka nje kutolipishwa kodi ipasavyo, utaalamu mdogo wa uendeshaji viwanda na mbinu duni za ujasiriamali.

Mhe. Naibu Spika, Nne, wizara ilichukua hatua za kufanya tathmini ya viwanda mbali mbali kama vile kiwanda cha sukari – Mahonda, Kiwanda cha ukaushaji samaki – Nungwi, Mradi wa kukaushia dagaa – Ndagoni ambapo Wizara imesaidia kupunguza matatizo ya upatikanaji wa maji, ukosefu wa vifaa vya kupimia ubora wa bidhaa na kusaidia kuwajengea uwezo wa ujasiriamali wa viwanda hivyo hasa vya ukaushaji samaki na dagaa.

Mhe. Naibu Spika, kwa upande wa hali ya Kiwanda cha Sukari – Mahonda kwa sasa naomba kukiri kuwa siyo nzuri na kinakabiliwa na matatizo mengi yakiwemo ya uzalishaji, utawala na uendeshaji, uhusiano wake na wananchi wa vijiji vinavyozunguka mashamba na kiwanda, huduma hafifu katika mashamba na uwezo kifedha na kiwanda. Kutokana na matatizo hayo na pia kwa kuzingatia umuhimu na azma yetu ya kuendeleza viwanda nchini, wizara iliunda Kamati maalum ya Watalaam kutathmini kwa undani hali ya Kiwanda, mashamba ya miwa na uzalishaji sukari na kuishauri Serikali namna ya kushughulikia matatizo ya shirika hilo.

Mhe. Naibu Spika, kamati ya wataalamu kuhusu Kiwanda cha Sukari cha Mahonda iliandaa taarifa yake na kuiwasilisha wizarani kwa mazingatio. Taarifa hiyo pamoja na mapendekezo yake yaliwasilishwa Serikalini kwa mazingatio na maelekezo ya utekelezaji wa mapendekezo yake. Baada ya mazingato yake, Serikali ilifanya maamuzi yafuatayo:-

- Kwanza**,** kuunda Kamati ndogo ya Baraza la Mapinduzi itakayotathmini masuala ya kisheria kuhusu Mkataba uliopo baina ya Muekezaji na Serikali. Lengo ni kuiwezesha Serikali kuwa na msingi madhubuti wa kisheria utaoiwezesha kulishughulikia suala la ubinafsishaji wa Shirika hilo

kisheria ili uwezekano wa kujitokeza athari kubwa za madai.

- Pili**,** kuunda Kamati ndogo ya Mawaziri na kupewa jukumu la kufanya kazi ya kisiasa kwa kuzungumza na wananchi wanaozunguka eneo la kiwanda na kushauriana nao kuhusu umuhimu wa kiwanda kwa uchumi wa nchi na ukuzaji ajira.

- Tatu, kuunda Kamati ya Wataalamu itakayotathmini hali ya sasa ya uchumi na uzalishaji sukari na matarajio ya baadae ya kiwanda hicho ikiwa ni pamoja kuzingatia na matumizi mbadala ya mashamba ya miwa iwapo itaonekana haja ya kubadilisha matumizi yake ya sasa.

Hivi sasa, Mhe. Naibu Spika, utekelezaji wa kazi za Kamati hizo unaendelea.

Mhe. Naibu Spika, kwa upande wa mradi wa kusarifu mazao ya baharini (dagaa) huko Ndagoni, hali ya uzalishaji bado sio ya kuridhisha na kwamba mradi huo unakabiliwa na matatizo mengi. Mradi ulianzishwa kama moja ya njia za kuimarisha maendeleo ya viwanda, kutoa ajira kwa wananchi na kuongeza kipato chao. Hata hivyo, utekelezaji wa mradi huo unakabiliwa na matatizo ya ukosefu wa umeme, maji, utaalamu mdogo, vifungashio duni, mtaji na vifaa vyengine vya uzalishaji. Kama nilivyoeleza hapo awali, Wizara kwa upande wake imechukua hatua ya kufikisha umeme katika kiwanda, kununua tangi la kuhifadhia maji, kuongeza idadi ya trea za kukaushia dagaa, kununua jokofu kwa ajili ya kuhidhi dagaa na kutoa mafunzo ya uhifadhi wa dagaa kwa wanaushirika. Hatua hiyo ya Serikali, Mhe. Naibu Spika,

inakusudia kutoa msaada kwa ushirika husika ili uweze kusimama wenyewe na kujitegemea na kuwa mfano wa kuendeleza sehemu nyengine nchini.

(iv) **Kuimarisha Mazingira ya Kuifanyia kazi:**

Mhe. Naibu Spika, kwa madhumuni ya kuimarisha tija ya utendaji kazi wizara ilichukua hatua mbali mbali za kujenga na kuimarisha maizingira ya kazi kwa kutoa mafunzo ya muda mrefu na muda mfupi, kuimarisha vitendea kazi na kukarabati majengo na ofisi za wizara.

Mhe. Naibu Spika, katika juhudi za kuendeleza wafanyakazi, jumla ya wafanyakazi tisa (9) wamepatiwa nafasi za masomo ya muda mrefu katika fani za usimamizi na uendeshaji wa biashara, uhasibu, teknolojia ya habari na mawasiliano, uhazili. Kwa upande mwengine, wafanyakazi kumi na nane (18) wamepatiwa mafunzo ya muda mfupi katika fani za usimamizi na uendeshaji biashara, teknolojia ya habari na mawasiliano, usimamizi wa uchumi, utandawazi na biashara za kimataifa, usimamizi na usalama wa chakula. Mafunzo hayo yamefanyika ndani na nje ya nchi.

Mhe. Naibu Spika, kwa upande wa kuimarisha sehemu za kufanyiakazi wizara imeanzisha ukarabati wa jengo la Makao Makuu na moja ya majengo yake chakavu ambalo linatumiwa na Idara ya Maendeleo ya Viwanda. Kadhalika, hivi sasa wizara inaendelea na matayarisho ya ujenzi wa ofisi ya wizara huko Pemba. Kwa ujumla, inatarajiwa kuwa kumalizika kwa ukarabati wa majengo ya ofisi za Wizara kutaimarisha sana mazingira ya kufanyia kazi na hivyo kulinda afya na kunusuru maisha ya watumishi wa wizara wanaotumia majengo machakavu na

hatarishi. Kwa jumla, uimarishaji huo utachochea tija ya wafanyakazi na kuimarisha ufanisi wa kazi.

Mhe. Naibu Spika, katika kipindi hicho, wizara ilichukua hatua za kukondoesha (*mainstream*) masuala ya UKIMWI na jinsia katika kazi za kila siku za wizara. Aidha, semina moja (1) imetayarishwa na vikao viwili vya Kamati Tendaji ya UKIMWI vimeitishwa kwa ajili ya kutoa taarifa za utekelezaji wa masuala yanayohusiana na hayo.

Mashirikiano Kati ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi

Mhe. Naibu Spika, **k**ama unavyoelewa kuwa katika kuimarisha mashirikiano kati ya sekta ya umma na sekta binafsi, serikali imeunda chombo maalum kwa ajili ya kufikia madhumuni hayo makubwa. Baraza la Biashara liliundwa ambalo ni jukwaa maalum la majadiliano kwa pande hizo mbili kwa lengo la kukabiliana na changamoto zinazoikabili sekta kuu za uchumi. Hali hiyo ya majadiliano ya pamoja baina ya sekta ya umma na sekta binafsi inaleta faida kubwa katika kukuza biashara na utoaji wa huduma hapa Zanzibar.

Mhe. Naibu Spika, katika kipindi cha Julai, 2010- Juni 2011, Baraza la Biashara la Zanzibar limefanya mkutano mmoja (1) ambapo hoja mbalimbali zilijadiliwa na kutolewa ufafanuzi. Hoja hizo zilihusiana na mambo yafuatayo:

- Changamoto zinazoikabili sekta ya utalii zikiwemo udhaifu katika kutangaza utalii wa ndani, uthibiti wa mapapasi na ukosefu wa ajira kwa wazalendo.

- Kuimarisha sekta ya biashara na viwanda katika kukabiliana na ushindani kwa kushughulikia ubora

wa viwango vya bidhaa, kuongeza thamani ya mazao, na utambulisho wa bidhaa (*branding*).

- Kuongeza uzalishaji wa mazao ya kilimo na rasilmali za baharini ili kuwa na mazao ya kutosha ya kusafirisha.

- Kutenga biashara maalum kwa ajili ya wawekezaji wazalendo na kuandaa vivutio maalum kwa wawekezaji hao.

- Kuanzisha Benki ya Maendeleo ya Uwekezaji ili kuweza kutoa mikopo ya muda mrefu kwa wawekezaji na wafanyabiashara.

- Matatizo ya wafanyabiashara wanayokumbana nayo katika bandari ya Dar es Salaam wakati wa kusafirisha bidhaa.

- Matayarisho ya sekta binafsi kukabiliana na ushindani wa biashara katika masoko ya Kikanda na Kimataifa.

Mashirika ya Serikali

Mhe. Naibu Spika, Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko inasimamia mashirika mawili ya biashara ambayo ni Shirika la Biashara ya Magari (*MTC*), na Shirika la Biashara la Taifa (*ZSTC*).

Shirika la Biashara la Taifa (*ZSTC*)

Mhe. Naibu Spika, Shirika la Biashara la Taifa (*ZSTC*) limepewa jukumu la kutafuta masoko, kununua, kuuza na kusafirisha bidhaa mbali mbali za kilimo na bahari. Hata hivyo, kwa sasa shirika hilo linashughulikia zao la karafuu peke yake na kusindika bidhaa zinazotokana na zao hilo.

Katika msimu uliopita, shirika lilinua tani 2,164.54 za karafuu zenye thamani ya shilingi 7,162 milioni sawa na asilimia 74.62 ya makadirio yaliyowekwa. Aidha, shirika limefanya mauzo ya tani 2,090 zenye thamani ya shilingi 10,917.9 milioni sawa na US$ 7,350 milioni.

Mhe. Naibu Spika, kwa upande wa usindikaji wa mazao ya karafuu na mazao mengine shirika limezalisha tani 14.6 za mafuta ya Mkaratusi, Makonyo, Mchaichai, Mrehani na Majani ya Mkarafuu yenye thamani 155.07 milioni.

Zao la Karafuu

Mhe. Naibu Spika, zao la karafuu ni moja kati ya mazao yenye tija na umuhimu mkubwa kwa uchumi wa Zanzibar na wananchi wake. Takwimu za ununuzi wa zao la karafuu zinaonesha kuwa wakulima wa zao hilo hasa Pemba wanafaidika na malipo ya ununuzi huo ambao ulifikia kati ya shilingi 7,000.00 milioni na shilingi 12,000 milioni katika misimu ya mwaka 2008 na mwaka 2010. Kwa kuzingatia mchango huo mkubwa katika mapato ya wananchi, ni dhahiri kuwa zao la karafuu kwa sasa ndiyo shughuli muhimu ya kiuchumi inayochangia kwa kiasi kikubwa mapato ya wananchi na hivyo kuwa zao muhimu katika utekelezaji wa mpango wa kundoa umasikini.

Mhe. Naibu Spika, uchambuzi wa mwenendo wa uzalishaji wa karafuu umebaini kuwa zao la karafuu kwa ujumla linakabiliwa na matatizo ya uzalishaji na matatizo ya kibiashara. Matatizo ya uzalishaji yanajumuisha uhaba wa ardhi ya kuzalisha zao hilo, teknolojia ya uzalishaji, uzee wa mikarafuu, uhaba wa huduma za kifedha, udhaifu katika usimamizi na uendelezaji wa kilimo cha mikarafuu na uanikaji wa zao la karafuu. Changamoto hizo zimesababisha kushuka kwa uzalishaji wa zao hili kwa mwendo wa kasi kubwa.

Mhe. Naibu Spika, kwa kutathmini takwimu hizo za uzalishaji, imebainika kuwa kila baada ya miaka kumi (10) uzalishaji wa karafuu unapungua na kwamba hivi sasa 2008/2009 – 2009/2010 uzalishaji huo ni wastani wa tani 2,673 sawa na asimia 27 tu ikilinganishwa na wastani wa tani 9,952 uliokuwepo katika kipindi cha 1964/1965 - 1973/1974. Uchambuzi zaidi unaonekana katika **Jadweli Nam.14**

Jadweli nam 14:

Wastani wa uzalishaji karafuu kwa vipindi vya miaka 10:

MWAKA	UZALISHAJI	ASILIMIA
1964/65-1973/74	9,952	100
1974/75-1983/84	5,525	55.5
1984/85-1993/94	5,705	57.4
1994/95-2003/04	3,327	33.4
2004/05-2009/10	2,673	27.0

Chanzo: ZSTC

Mhe. Naibu Spika, matatizo mengine yanayolikabili zao la karafuu ni ya kibiashara ambayo yanayojumuisha uwezo mdogo wa *ZSTC* kutafuta masoko, kuendesha biashara kwa gharama kubwa na kushindwa kutoa bei ya ushindani kwa wakulima, ushindani katika masoko ya nje, udhaifu katika kusarifu mazao ya karafuu na kushamiri kwa magendo ya karafuu na makonyo. Serikali imechukua hatua madhubuti za kusimamia utendaji wa *ZSTC* na kulibadilisha ili liweze kuendesha shughuli zake kwa ufanisi.

Mhe. Naibu Spika, kuhusu kushamiri kwa tatizo la magendo ya karafuu wizara ilifanya utafiti na kubaini kuwa nchi moja ya jirani hivi sasa imejitokeza kuwa msafirishaji mkubwa wa karafuu, ingawa nchi hiyo haizalishi karafuu. Katika kipindi cha mwaka 2001 hadi 2009 nchi hiyo ilisafirisha jumla ya tani 9,510 zenye thamani ya US$ 16,046,000. Kwa kutumia takwimu za biashara ya karafuu duniani imebainika kuwa nchi hiyo jirani ni msafirishaji mzuri wa bidhaa hiyo. **Jadweli Nam 15** linatoa ufafanuzi zaidi kuhusu mwenendo wa usafirishaji wa zao hilo baina ya Tanzania (Zanzibar) na nchi jirani.

Jadweli nam.15:
Usafirishaji wa karafuu kwa tani:

	2001	2002	2003	2004	2005	2006	20
TANZANIA (ZANZIBAR)	2,456	1,224	5,547	4,363	2,967	3,033	3,
NCHI JIRANI	2,036	543	350	476	728	969	
JUMLA	4,492	1,767	5,897	4939	3,695	4,002	3,
ASILIMIA	45.3	30.7	6.0	9.6	19.7	24.2	2

Ili kupambana na tatizo hili Mhe. Naibu Spika, Serikali imeanza kuchukua hatua za kisoko za kupunguza na hatimae kuondosha kabisa pengo la bei ya mkulima na ile ya soko la dunia ili kuondoa kishawishi cha kufanya biashara hiyo kwa magendo. Kadhalika, Serikali inakamilisha taratibu za kuunda Mfuko wa Maendeleo ya karafuu kwa madhumuni ya kusimamia vyema zao hilo.

Mhe. Naibu Spika, uanzishaji wa Mfuko wa Maendeleo ya Zao la Karafuu ni moja wapo ya eneo muhimu la utekelezaji wa Mkakati wa Kuimarisha zao la karafuu (*Clove Development Strategy*) ambao utatekelezwa kwa kipindi cha miaka kumi (10) kuanzia sasa. Katika utekelezaji wa Mkakati huo, serikali itajielekeza katika maeneo makuu yafuatayo:

(i) Kuwa na msingi wa kisera kuhusu biashara ya karafuu (*commercial policy*) ili kusimamia biashara hiyo. Kwa sasa serikali imeamua kumlipa Mkulima wa karafuu asilimia themanini (80%) ya bei ya karafuu itakayouzwa katika soko la dunia.

(ii) Kurekebisha muundo wa Shirika la Taifa la Biashara (*ZSTC*) kwa kubainisha majukumu yake mapya, kuweka sheria mpya kwa ajili hiyo na kuliimarisha kiutendaji kwa kuajiri wafanyakazi wenye uwezo zaidi na mbinu za kibiashara.

(iii) Kuimarisha mfumo na taratibu za uendeshaji wa biashara ya karafuu kimataifa ikiwa ni pamoja na kuipatia karafuu ya Zanzibar utambulisho maalum

wa kimataifa (*Branding*) kwa kutumia misingi ya "*Intellectual Property – IP*" ili kudhibiti magendo na uuzaji holela wa karafuu za Zanzibar.

(iv) Kuanzisha Mfuko wa Maendeleo ya Karafuu ambao pamoja na mambo mengine, utashughulikia kilimo cha karafuu, pamoja na kutoa huduma za kitaalamu za kuendeleza zao hilo.

Biashara ya Mwani

Mhe. Naibu Spika, uzalishaji wa mwani umejitokeza kuwa ni shughuli muhimu na maarufu ya kiuchumi na biashara hapa Zanzibar katika miaka ya hivi karibuni. Hivi sasa kiwango cha usafirishaji mwani kimefikia wastani wa kati ya tani 10,000 hadi 12,000 kwa mwaka. Kiasi hicho ni mara tatu ya wastani wa uzalishaji na usafirishaji zao la karafuu. Kwa upande wa utengenezaji nafasi za kazi hasa kwa wawanake, shughuli za uzalishaji mwani zinatoa ajira ya moja kwa moja kwa wananchi kati ya 3,000 na 4,000 kwa mwaka.

Pamoja na umuhimu huo wa kiuchumi Mhe. Naibu Spika, zao la mwani bado limeendelea kukabiliwa na matatizo mbali mbali kama vile vifaa vya uzalishaji, ukaushaji duni ambao hupoteza ubora wa mwani wenyewe, mikataba dhaifu baina ya wanunuzi na wazalishaji ambayo husababisha wazalishaji kulipwa bei duni na pia kuwepo kwa huduma ndogo za ugani (*Extension Services*) kutoka serikalini. Kwa mwaka ujao wa fedha, Wizara yangu itachukua hatua ya kutafiti na kubainisha mfumo wa gharama (*Cost Structure*) kwa uzalishai na usafirishaji wa zao hilo. Hatua hiyo inalenga katika kuwapatia wakulima bei stahiki kulingana na

mwenendo wa bei katika soko la dunia. Kadhalika, kwa kushirikiana na Shirika la Maendeleo ya Viwanda la Umoja wa Mataifa (*UNIDO*), Wizara yangu itatafiti uwezekano wa kuongeza thamani kwa kuzalisha bidhaa mbali mbali za mwani badala ya kuuza ikiwa ghafi.

Shirika la Biashara ya Magari (*MTC*)

Mhe. Naibu Spika, madhumuni makubwa ya kuanzishwa shirika hili ilikuwa ni kuagiza vipando vya moto vya aina mbali mbali kama magari na vyombo vyengine vya moto kwa lengo la kuwauzia wananchi na serikali kwa mkopo na fedha taslimu. Kutokana na mabadiliko ya sera za kiuchumi na biashara, shughuli za biashara hii kwa sasa zinafanywa kwa asilimia kubwa na sekta binafsi, ambapo shirika hilo kwa sasa limekosa nafasi ya kufanya biashara hiyo kwa ufanisi na ushindani. Kadhalika, kutokana na mtaji mdogo, shirika linashindwa kutekeleza kazi zake ipasavyo na hivyo kutoa mwanya kwa sekta binafsi kuhodhi soko la biashara hiyo. Kwa kuzingatia hali hiyo na matarajio kwa siku za usoni, serikali imefikia uamuzi wa kulifunga Shirika hilo. Taratibu za kulifunga shirika hilo kwa mujibu wa sheria na kuwalipa wafanyakazi wote maslahi yao zinakamilishwa.

CHANGAMOTO

Mhe. Naibu Spika, katika utekelezaji wa malengo na majukumu mbali mbali ya Wizara kwa mwaka 2010/2011 yapo mafanikio makubwa yaliyopatikana. Hata hivyo, pamoja na mafanikio hayo, zipo pia changamoto kadhaa ambazo ziliendelea kuathiri utekelezaji wa malengo yaliyopangwa na ufanisi wa sekta ya biashara na maendeleo ya viwanda. Miongoni mwa changamoto hizo ni kama hizi zifuatazo:-

i. Mwenendo wa biashara katika masoko ya kimataifa ambao kwa kiasi kikubwa umeendelea kutibuliwa na matokeo mbali mbali ya majanga ya kimaumbile ikiwemo ukame na mafuriko, matukio ya kisiasa na vita vinavyoendelea katika nchi za kiarabu na kuathiri bei za mafuta duniani, uharamia katika pembe ya Afrika. Kasi ndogo ya kuimarika chumi za magharibi kunatokana na mtikisiko wa kifedha uliojitokeza hivi karibuni na athari zake kwa mwenendo wa bei za chakula katika soko la Zanzibar.

ii. Uwezo mdogo wa uzalishaji wa ndani wa bidhaa na udhaifu wa kutumia fursa za masoko ya kikanda kuongeza usafirishaji pamoja na thamani za uzalishaji huo.

iii. Ari ndogo ya wajasiriamali na wafanyabiashara wadogo wadogo, kujifunza mbinu mpya za kibiashara ili kujijengea uwezo wa kujitegemea wenyewe.

iv. Mwitikio mdogo wa sekta binafsi kuwekeza katika viwanda na kuongeza pato la sekta hiyo. Kadhalika, utaalamu mdogo katika uendeshaji viwanda, mitaji, gharama za umeme na malighafi zimeendelea kuainishwa kama ni kikwazo katika maendeleo ya viwanda hapa Zanzibar.

v. Mfumo na utekelezaji wa sheria za kodi ambao unaacha mwanya kwa bidhaa za nje ambazo pia huzalishwa nchini, kuingia na kuuzwa kwa bei za

chini kuliko gharama halisi za kuzalisha bidhaa hizo hapa nchini.

vi. Utayari na uwezo wa wafanyabiashara wa Zanzibar kuzitumia fursa za kibiashara zilizopo katika masoko ya Jumuiya za Kikanda kama vile *SADC* na *EAC*.

MALENGO YA MWAKA 2011/2012

Mhe. Naibu Spika, malengo ya mwaka 2011/2012 yamewekwa kwa kuzingatia jukumu mahsusi la utekelezaji wa Dira 2020, Mpango Mkuu wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umasikini (MKUZA), Mkakati wa Kusafirisha bidhaa nje (*NES*), Maagizo Maalum ya Serikali kwa Wizara, Mpango Mkakati wa Wizara na Maelekezo na Hotuba ya Rais katika uzinduzi wa Baraza la Wawakilishi. Kwa mnasaba wa utekelezaji wa matarajio hayo, malengo ya Wizara yatakuwa kwa kipindi kama ifuatavyo:-

(i) Kuendelea kuimarisha mazingira bora ya ukuzaji biashara:

- kufanya mapitio makubwa mfumo wa utoaji leseni za biashara nchini ili kurahisisha uanzishwaji na ufanyaji biashara;

- Kuanza utekelezaji wa Sheria ya Viwango ya Zanzibar;

- Kuwasilisha serikalini kwa mazingatio Sheria za Ushindani na Kumlinda Mtumiaji, Mizani

na Vipimo na sheria ya biashara pamoja na kuandaa utekelezaji wake.

(ii) Kuendeleza Eneo la Uwanja wa Kimataifa wa Maonesho ya biashara kwa kutayarisha michoro ya matumizi ya ardhi (*Land use Plan*), kutayarisha michoro ya kiufundi (*Structural and Architectural Design*) pamoja na kuatayarisha gharama za mradi (*Bill of Quantity*), na kuanzisha maeneo mengine ya maonesho madogo madogo na masoko ya Jumapili ili kuwakutanisha wazalishaji na wafanyabiashara wa ndani na wanunuzi.

(iii) Kukamilisha utafiti wa kuiwezesha serikali kufanya maamuzi makini kuhusu mkakati wake wa kuimarisha uchumi na uendelezaji viwanda wenye lengo la kuchangamsha biashara. Utafiti huo kama nilivyoeleza hapo awali, unakusudia kuigeuza Zanzibar kuwa eneo tengefu la uchumi (*SEZ*) kwa kuzingatia nafasi yake ya kuimarisha ushindani ndani ya soko la Afrika Mashariki na nchi za Jumuiya ya *SADC*.

(iv) Kuratibu utekelezaji wa mkakati wa kuimarisha usafirishaji bidhaa (*Export Strategy*);

(v) Kuliimarisha Shirika la Biashara la Taifa (*ZSTC*) kwa kulifanyia mageuzi makubwa ya kisheria na muundo ili liweze kusimamia vizuri uendelezaji wa zao la karafuu, biashara yake na kuweza kushindana katika soko;

(vi) Kuanzisha Mfuko maalum wa kuendeleza karafuu (*Clove Development Fund*);

(vii) Kuimarisha mazingira ya uwekezaji katika sekta ya viwanda kwa kufanya mapitio ya Sera ya viwanda, kuchunguza vikwazo vinavyokwamisha maendeleo ya viwanda Zanzibar, na kuweka mfumo mpya wa vivutio kwa ajili ya kuendeleza sekta hiyo hapa Zanzibar;

(viii) Kusimamia na kuratibu maendeleo ya viwanda vichache vilivyopo ili kuelewa matatizo yao na kutoa usaidizi wa kitaalamu, kisera na mbinu za biashara ili viweze kuendesha shughuli za uzalishaji kwa ufanisi;

(ix) Kuimarisha mashirikiano baina ya sekta binafsi na serikali (*PPP*) kwa kutoa fursa kubwa zaidi kwa sekta hiyo kushiriki katika maendeleo ya uchumi wa nchi;

(x) Kuandaa mapendekezo ya matumizi mbadala ya kibiashara ya eneo la Bwawani na mpango wa uendelezaji wake;

(xi) Kuandaa mpango kazi wa taarifa ya utafiti kuhusu kuongeza thamani mazao (*value chain study*), na Sera ya Biashara ndogo ndogo na za kati (*SMEs*) kwa ajili ya utekelezaji;

(xii) Kufanya tathmini ya utekelezaji wa Sera ya Biashara ya Zanzibar ya mwaka 2006;

(xiii) Kuimarisha mfumo wa ukusanyaji na utoaji wa taarifa na takwimu za biashara;

(xiv) Kuendeleza mazingira mazuri ya kazi na maendeleo ya wafanyakazi kwa kuwapatia wafanyakazi mafunzo ya muda mrefu na muda mfupi;

(xv) Kupitia Shirika la Biashara la Taifa (*ZSTC*) wizara imepanga kununua tani elfu tatu (3000 tons) za karafuu kwa thamani ya shilingi 30,000.00 milioni.

(xvi) Kukamilisha taratibu za kulifunga (*wind up*) Shirika la Biashara la Magari (*MTC*) katika msimu unaoanzia Julai, 2011.

(xvii) Kukusanya mapato ya shilingi 30.0 milioni.

SHUKRANI

Mhe. Naibu Spika, mafanikio ya wizara yaliyopatikana ni matokeo ya mashirikiano makubwa ya Wajumbe wa Baraza hili chini ya uongozi wa Mhe. Spika na wewe Naibu Spika kwa uongozi wenu mahiri. Ninakushukuruni na hasa wewe binafsi Mhe. Naibu Spika. Wenyeviti wa Kamati za Kudumu za Baraza na Wajumbe wote kwa ushauri na michango mliyotupa katika kipindi cha utekelezaji wa bajeti.

Mhe. Naibu Spika, sina budi kukiri vile vile kuwa, mafanikio ya kiutendaji yaliyojitokeza katika kipindi cha mwaka 2010/2011 ni matokeo ya ushirikiano mkubwa uliopatiwa wizara yangu kutoka wadau mbali mbali wa ndani na nje ya nchi yetu ikiwa pamoja na Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako tukufu pamoja na Kamati zake za Kudumu. Kwa madhumuni ya kutambua mchango

mkubwa wa Wadau mbali mbali kwa wizara, naomba kutoa shukurani zangu za dhati kwa nchi na taasisi za ndani na nje zifuatazo:-

(i) Jamhuri ya Watu wa China;
(ii) India;
(iii) Korea Kusini;
(iv) Umoja wa Falme za Kiarabu (*UAE*);
(v) Mpango wa Maendeleo wa Umoja wa Mataifa (*UNDP*);
(vi) Shirika la Umoja wa Mataifa la Maendeleo ya Viwanda (*UNIDO*);
(vii) Benki ya Dunia (*World Bank*);
(viii) Shirika la Biashara Duniani (*WTO*);
(ix) Sekretarieti ya Jumuiya ya Madola;
(x) Umoja wa Wafanyabiashara wa Zanzibar (*Zanzibar National Chamber of Commerce, Industry and Agriculture – ZNCCIA*);
(xi) Baraza la Biashara la Tanzania (*TNBC*); pamoja na
(xii) Wafanyabiashara wote na Wawekezaji wa Viwanda.

Mhe. Naibu Spika, napenda nichukue fursa hii kuwapongeza kwa dhati wafanyakazi wote wa Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko kwa kazi kubwa yenye ufanisi mzuri wanayoifanya kila siku licha ya kukabiliwa na changamoto mbali mbali, ni matarajio yangu kwamba wataongeza juhudi zao ili kuzidisha ufanisi kwa kuwahudumia wananchi na kutekeleza majukumu yao ipasavyo. Kadhalika, napenda kuwapongeza wafanyakazi wote walioshiriki katika maandalizi ya Hotuba hii kwa kazi nzuri waliyoifanya, nawaombea dua njema katika kazi zao.

Mhe. Naibu Spika, naomba vile vile kutoa shukurani za pekee kwa Mpiga Chapa Mkuu wa Serikali na wafanyakazi wake wote kwa kuweza kufanikisha uchapaji wa hotuba hii kwa wakati. Kadhalika, naomba vile vile kutoa shukurani za dhati kwa jumuiya mbali mbali, wafanyabiashara na wananchi kwa jumla kwa ushirikiano walioutoa katika kufanikisha utekelezaji wa majukumu ya wizara kwa mwaka unaomalizika na kuwaomba kuendelea kushirikiana na wizara ili kwa pamoja tuweze kuijenga nchi yetu na kufikia malengo tuliyojipangia kwa ustawi wa wananchi wetu.

Mhe. Naibu Spika, naomba niwashukuru wafanyabiashara wote wakubwa, wakati, wadogo na Juakali na wengine kwa juhudi zao kubwa za kuwahudumia wananchi kwa kuwapatia huduma mbali mbali pamoja na bidhaa muhimu za nguo, chakula na vifaa vya ujenzi. Nawaomba waendelee kushirikiana na wizara yangu kwa kufanya kazi pamoja kwa lengo la kuimarisha biashara na kutoa huduma bora kwa wananchi. Nawaomba wafanyabiashara wote kuwahurumia wananchi kwa kuwawekea bei nafuu ili wamudu maisha yao. Aidha, nawaomba wafanyabiashara waekeze katika viwanda na biashara ya viungo (*spices*) kama vile mdalasini, manjano na viungo vyengine kwani vina faida kubwa katika kuendesha biashara na kuongeza ajira.

Mhe. Naibu Spika, hotuba yangu hii haitokamilika kama sijatoa shukurani zangu za dhati kwa wananchi wa Jimbo la Mtoni, kwa ushirikiano wao mkubwa wanaonipa na kunivumilia pale ninapokua mbali nao kutokana na majukumu mengine ya kitaifa yanayonikabili, nakiri kwamba imani na heshima yao kwangu ni kubwa na ya kipekee na ninaithamini sana.

HITIMISHO

Mhe. Naibu Spika, ili Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko iweze kutekeleza kwa ufanisi majukumu yake kama ilivyojipangia, naliomba Baraza lako tukufu sasa liidhinishe matumizi ya jumla ya Shilingi. 2,662.0 milioni (Shilingi bilioni mbili, milioni mia sita na sitini na mbili) kwa mwaka wa fedha wa 2011/2012. Kati ya fedha hizo Shilingi 1,462.0 (Shilingi bilioni moja, milioni mia nne na sitini na mbili) kwa ajili ya kazi za kawaida, Shilingi 300.0 milioni (Shilingi milioni mia tatu) kwa ajili ya kazi za maendeleo na Shilingi 900.0 milioni (Shilingi milioni mia tisa) kwa ajili ya ruzuku kwa taasisi mbali mbali zilizo chini ya wizara. **Jadweli Nam. 16** hapa chini linafafanua zaidi maombi ya matumizi ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2011/2012.

Mhe. Naibu Spika, kwa upande wa ukusanyaji wa mapato wizara imepewa lengo la kukusanya Shilingi 30.0 milioni katika kipindi hicho.

Jadweli Nam. 16:

Bajeti ya Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko 2011-2012:

Vote Nam.	Idara	Kazi za Kawaida	Kazi za Maendeleo	Ruzuku
03:	Afisi Kuu Pemba	238,4000,000	-	-
04:	Mipango, Sera na Utafiti	230,566,000	300,000,000	-

05:	Maendeleo ya Viwanda	181,460,000	-	-
06:	Biashara na Masoko	255,397,000	-	-
07:	Utumishi na Uendeshaji	556,177,000	-	-
	Baraza la Biashara	-	-	200,000,000
	Taasisi ya Ushindani	-	-	250,000,000
	Taasisi ya Viwango Zanzibar	-	-	250,000,000
	Taasisi ya Vipimo	-	-	200,000,000
	Jumla ndogo:	**1,462,000,000**	**300,000,000**	**900,000,000**
	Jumla Kuu:	**-**	**-**	**2,662,000,000**

Mhe. Naibu Spika, kadhalika naomba kuliarifu Baraza lako tukufu kuwa, utekelezaji wa baadhi ya malengo yaliyoorodheshwa hapo juu utagharamiwa na Washirika wa Maendeleo. Hata hivyo, kiasi cha fedha kitakachotengwa kwa wizara kilikuwa bado kubainishwa na washirika hao ingawa fungu la misaada yao kwa Zanzibar lilijulikana na kuwasilishwa mbele ya Baraza lako kwa kuombewa idhini katika Bajeti ya Serikali.

Mhe. Naibu Spika, kwa heshima na taadhima na unyenyekevu mkubwa naomba kutoa hoja.

(Hoja ilitolewa ijadiliwe)

Kiambatisho Nam. 1

MUUNDO WA WIZARA YA BIASHARA, VIWANDA NA MASOKO:

Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko imeundwa na Idara nne, mashirika mawili pamoja na Afisi Kuu – Pemba kama ifuatavyo:

- Idara ya Mipango, Sera na Utafiti;
- Idara ya Biashara na Ukuzaji Masoko;
- Idara ya Maendeleo ya Viwanda na Ukuzaji Ujasiriamali;
- Idara ya Uendeshaji na Utumishi;
- Afisi Kuu – Pemba;
- Shirika la Biashara la Taifa (ZSTC); na
- Shirika la Biashara ya Magari (MTC).

Hata hivyo muundo huo unatarajiwa kubadilika kulingana na mapitio ya sheria zilizopo pamoja na kutekeleza sheria mpya iliyotungwa ambazo zitapelekea uanzishwaji wa taasisi mpya. Taasisi zinazotegemewa kuanzishwa ni:-

i) Kamisheni ya Ushindani;
ii) Taasisi ya Viwango ya Zanzibar; na
iii) Wakala wa Mizani na Vipimo Zanzibar.

MAJUKUMU YA WIZARA YA BIASHARA, VIWANDA NA MASOKO:

Wizara ina majukumu yafuatayo:-

- Kusimamia kuwepo kwa mazingira mazuri ya biashara;
- Kukuza mashirikiano kati ya sekta banafsi na sekta ya umma;
- Kusimamia kuwepo kwa ushindani halali wa kibiashara ili kumlinda mtumiaji;
- Kuwaimarisha na kuwaendeleza wafanyabiashara ndogo ndogo;
- Kusimamia ubora wa huduma na bidhaa zinazouzwa nchini;
- Kutafuta masoko ndani na nje ya nchi kwa bidhaa za Zanzibar;
- Kuendeleza Viwanda viliopo;
- Kuweka mazingira mazuri yatakayoshajihisha sekta binafsi kuwekeza katika viwanda;
- Kuimarisha na kukuza viwanda vodogo vidogo;
- Kusimamia ubora wa bidhaa zinazozalishwa nchini;
- Kuratibu na kusimamia shughuli za utafiti na sera zinazohusiana na uimarishaji na uendelezaji wa sekta za biashara na viwanda;
- Kuendeleza mashirikiano ya biashara kinchi, kikanda na kimataifa; na
- Kuwaendeleza na kuwajengea mazingira mazuri wafanyakazi wa Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko.

WIZARA YA BIASHARA, VIWANDA NA MASOKO



Kiambatisho Nam. 2

Jadweli 1(a)

Usafirishaji na Uagiziaji Bidhaa Duniani 2010 (USD bilioni):

Kanda	Usafirishaji	Asilimia	Uagiziaji	A
Ulaya	5,630	38	5,840	
Asia	4,960	32	5,500	
Marekani/ kaskazini	1,960	13	2,680	
Mashariki ya Kati	916	6	572	
J.Madola	588	4	484	
Marekani/Kusini	575	4	576	
Afrika	500	3	463	
Jumla	**15,129**	**100**	**16,115**	

Chanzo*: *Shirika la Biashara la Ulimwengu – WTO

Jadweli 1(b)

Usafirishaji kwa nchi 2010 (USD bilioni)

Nchi	Usafirishaji	Asilimia	Uagiziaji	Asilimia
China`	1,580	10	1,400	9
Marekani (USA)	1,280	8	1,970	13
Ujerumani	1,270	8	1,070	7
Japan	770	5	693	4.5
Holand	572	3.8	-	-
France	-	-	606	4

Chanzo:* *Shirika la Biashara la Ulimwengu – WTO

Jadweli Nam 2:

Usafirishaji na Uagiziaji Bidhaa (Tsh.000)

Maelezo	2006	2007	2008	2009
Usafirishaji	15,424.3	21,177.7	30,189.2	29,744.5
Uagiziaji	87,465.3	107,689.9	93,439.6	120,882.0
Ziada/Upunguaji	(72,041.0)	(86,512.8)	(63,250.4)	(91,137.5)
Asilimia	467.06	408.51	209.51	306.40

Chanzo: *Ofisi ya Mtakwimu Mkuu*

Jadweli Nam 3:

Biashara katika Bandari Huru Kutoka mwaka 2006-2010:

MWAKA	UAGIZIAJI	USAFIRISHAJI	MAUZO YA NDANI
2006	1,250,722	48,500	1,380,927
2007	1,264,491	22,710	1,540,370
2008	1,569,071	32,733	1,402,340
2009	1,608,500	40,220	1,780,501
2010	1,374,865	18,500	1,547,218
Jumla	**7,067,649**	**162,663**	**7,651,356**

Chanzo: ZIPA

Jadweli Nam.8(a)

Muundo wa Sekta ya Viwanda:

Nam	Aina ya Viwanda	Idadi	Asilimia
1.	Useremala na samani	38	25.3

2.	Matufali na bidhaa za saruji	30	20
3.	Bekari	18	12
4.	Ushoni	11	7.3
5.	Chokaa na kokoto	14	9.3
6.	Vinywaji baridi (maji na juice)	5	3.3
7.	Usagishaji	6	4
8.	Sukari	1	0.7
9.	"Essential oils" na makonyo	2	1.3
10.	Majani ya chai	1	0.7
11.	Uchapishaji	5	3.3
12.	Mafuta ya Nazi	3	2
13.	Usindikaji, Tambi nk	16	10.7
	Jumla	**150**	**100**

Chanzo: *Ofisi ya Mtakwimu Mkuu*.

Jadweli Nam. 8(b):

Uajiri katika Sekta ya Viwanda:

Nam	Aina ya Kiwanda	Idadi
1.	Chokaa na kokoto	373
2.	Vinywaji baridi (Maji na juice)	557
3.	Bekari	294
4.	Useremala na samani	829
5.	Matufali na bidhaa za saruji	547
6.	Ushoni	179
7.	Uchapishaji	162
8.	Viwanda vyenginevyo	647
	Jumla	**5,568**

Chanzo: *Ofisi ya Mtakwimu Mkuu.*

Jadweli Nam. 9:

Mchango wa Sekta ya Viwanda katika GDP:

	2006	2007	2008	2009	2010
Uzalishaji(Tshs. bilioni)	23.4	26.6	32.5	36.1	39.5
Kasi ya ukuaji	3.5	0.5	1.1	2.4	3.1
Mchango katika Pato la taifa	4.6	4.5	4.3	4.1	4.2

Chanzo: Ofisi ya Mtakwimu Mkuu.

Jadweli Nam 10:

Biashara katika Maeneo Huru 2005 – 2010:

MWAKA	UAGIZIAJI WA MALIGHAFI NA MITAMBO (USD)	USAFIRISHAJI (USD)	ASILIMIA
2005	3,239,055	2,370,450	14.6
2006	3,800,652	3,575,476	22.0
2007	3,986,700	4,100,740	25.1
2008	3,242,230	2,394,360	14.7
2009	4,895,817	2,985,560	18.2
2010	2,027,392	835,524	5.4
JUMLA	**21,191,846**	**16,262,110**	**100**

Chanzo: ZIPA

Kiambatisho Nam. 8

Jadweli Nam. 11(a)

Bajeti kwa Kazi za Kawaida 2010 - 2011:

Vote Nam	Idara	Kiasi
03:	Afisi Kuu Pemba	163,407,000
04:	Idara ya Mipango na sera	631,160,000
05:	Idara ya Maendeleo ya viwanda	72,196,000
06:	Idara ya Biashara na Masoko	172,237,000
	Ruzuku ya Utalii, Baraza la Biashara na Uwekezaji	900,000,000
	Jumla	**1,939,000,000**

Jadweli Nam. 11(b)

Bajeti kwa kazi za Maendeleo 2010-2011:

MRADI	MAKISIO YA BAJETI
Mapitio ya sheria zinazoendana na biashara	65,000,000
Kuimarisha mazingira ya biashara	500,000,000
Mpango wa kuendeleza Viwanda vidogo vidogo (SMEs)	635,000,000
Maendeleo ya Chuo cha Utalii	500,000,000
Eneo la Viwanda Vidogo Vidogo	90,000,000
JUMLA	**1,790,000,000**

Jadweli Nam. 13:

UKAGUZI NA TATHMINI YA MAENDELEO YA VIWANDA:

Jina la Kiwanda		Pahala	Bi
1.	Alawy Supplies	Mbweni	Tissue, toilet p
2.	Zainab Bottlers	Mombasa	Maji, Juice
3.	China Building Contractors	Mtoni	Samani, Ujenz
4.	Mhana	Maruhubi	Samani
5.	Zanzibar Bottlers Ltd	Maruhubi	Vinywaji baric
6.	Mahonda Sugar Factory	Mahonda	Spiriti
7.	Scanza	Selem	Samani
8.	Zatepa	Selem	Ufungashaji w kahawa, mazi na chillie sukari "Toothp
9.	Multicolour Printers		Uchapishaji
10.	Aluminium Construction	Amani	Vifaa vya ujen
11.	Super Shine Safari Factories	Amani	Kaseti, CD, Bi
12.	Zanzibar Quality Tailoring Ltd	Amani	Ushoni wa ngu
13.	Savannah International Ltd	Amani	Ufungashaji w
14.	Zanzibar Fashion Ltd	Amani	Ushoni wa ngu
15.	Al Mahara Processing Ltd	Amani	Ufungashaji w
16.	Drop of Zanzibar Ltd	H. Mchana	Maji ya kunyw
17.	Zanzibar Milling Corp.	Mtoni	Unga ngano na Mahindi
18.	Al Zenjibari F. Products (Maziwa)	Maruhubi	Maziwa
19.	Kiwanda cha kusaga	Masingini	Mchele

	mpunga		
20.	ZAPOCO	Maruhubi	Chakula cha m
21.	Kiwanda cha kukaushia dagaa	Ndagoni	Dagaa
22.	Kiwanda cha kukaushia samaki	Nungwi	Samaki
23.	Kiwanda cha kuzalisha chumvi	Wawi – Pemba	Chumvi
24.	Kiwanda cha kukaushia matunda	kizimbani	Matunda

CHANZO: Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko

Kiambatisho Nam. 3

MALENGO YA MWAKA 2010/2011:

a. Kuimarisha mazingira ya biashara yakiwemo; kukamilisha matayarisho ya Sheria ya Viwango na Ubora wa Bidhaa, kufanya mapitio ya Mfumo wa Utoaji wa Leseni pamoja na Sheria ya Leseni Nam. 4 ya Mwaka 1983.

b. Kufanya upembuzi yakinifu (*feasibility study*), na kutayarisha mpango wa matumizi ya ardhi (*land Use Plan*) kwa ajili ya uwanja wa maonesho ya biashara ya kimataifa ili kupata wafadhili;

c. Kufanya upembuzi yakinifu kwa ajili ya kuifanya Zanzibar kuwa Eneo Tengefu la kiuchumi (*Special Economic Zones*);

d. Kuanza mchakato wa mapitio ya Sera ya biashara ili ikidhi matakwa ya kikanda na kimataifa;

e. Kukusanya mapato ya T.Shs 23,000,000 yanayotokana na ukaguzi wa mizani 2500, vituo vya Mafuta 38, na usajili wa

wafanyabiashara, pamoja na ukaguzi wa madukani 2000, maghala 172 na supermarket 10, na kuingia katika mfuko mkuu wa serikali;

f. Kutoa mafunzo ya muda mrefu kwa wafanyakazi watano (5), na wafanyakazi sita (6)mafunzo ya muda mfupi na kutoa mafunzo kwa wafanyabiashara wadogo wadogo na wajasiriamali hamsini (50);

g. Kuchapisha na kusambaza vijarida elfu mbili (2,000) vya sera ya Viwanda/Biashara ndogo ndogo na za kati (SMEs) iliyotayarishwa kwa lugha nyepesi (*Popular Version*);

h. Kukamilisha "Database" ya Viwanda (*Industrial Database*) kupitia Programu ya JP5;

i. Kutoa mafunzo yakiwemo ya kuongeza thamani (*value addition*) kwa zao la mwani, "*packaging*", masoko (*marketing technique*), udhibiti na ubora wa bidhaa (*quality control*/ *assurance*) na ubunifu wa bidhaa (*products design*) kwa wajasiriamali mia moja na ishirini na tano (125) (Unguja na Pemba);

j. Kukamilisha ukarabati wa kituo cha majaribio ya ukaushaji wa samaki kilichopo Nungwi;

k. Kufanya mapitio ya Sera ya Maendeleo ya Viwanda ya Mwaka 1998-2008

l. Kuendeleza mashirikiano baina ya sekta ya umma na sekta binafsi kupitia Baraza la Biashara.

Mhe. Abdalla Mohammed Ali (Makamo Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo): Mhe. Naibu Spika, naomba kusoma hotuba juu ya Makadirio ya Mapato na Matumizi

ya Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko kwa mwaka wa fedha 2011/2012.
Mhe. Naibu Spika, napenda kuchukua nafasi hii adhimu kwa kuanza kumshukuru Mwenyezi Mungu ambae ametujaalia afya na uzima na kutuwezesha sote kukusanyika hapa leo hali ya kuwa na uwezo wa kutekeleza majukumu yetu mbali mbali ambayo kiujumla tukishirikiana kwa pamoja ni mafanikio kwa nchi nzima.

Naomba pia nichukue fursa hii kwa kumpongeza Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko, Mhe. Nassor Ahmed Mazrui pamoja na Naibu wake Mhe. Thuwaybah Edington Kissasi kwa kuchaguliwa kwao kuiongoza Wizara hiyo. Tunaimani kwa uwezo wao wataweza kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi mkubwa. Pia pongezi hizo ziwaendee wasaidizi wao, Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu, Wakurugenzi na watendaji wengine wote.

Mhe. Naibu Spika, katika shukrani zangu, napenda pia kutoa pongezi kwa wajumbe wa Kamati hii ya Fedha, Biashara na Kilimo kwa mashirikiano yao, michango yao na mawazo yao kwa Serikali kupitia Wizara mbali mbali Kamati hii ilipofanya kazi zake. Kazi na juhudi zao zimetufikisha katika mafanikio makubwa ambayo leo hii yameniwezesha kusimama kwa niaba yao kuwasilisha hotuba hii.

Mhe. Naibu Spika, naomba uniruhusu niwatambue Wajumbe wa Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo kwa kuwataja kama ifuatavyo:

1.	Mhe. Salmin Awadh Salmin	Mwenyekiti
2.	Mhe. Abdalla Mohammed Ali	Makamo Mwenyekiti
3.	Mhe. Mlinde Mabrouk Juma	Mjumbe
4.	Mhe. Rufai Said Rufai	Mjumbe
5.	Mhe. Mahmoud Mohammed Mussa	Mjumbe
6.	Mhe. Raya Suleiman Hamad	Mjumbe

7.	Mhe. Bikame Yussuf Hamad	Mjumbe
8.	Ndg. Amour Moh'd Amour	Katibu
9.	Ndg. Asha Said Mohammed	Katibu

Mhe. Naibu Spika, Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko ina majukumu ya kusimamia utekelezaji wa malengo ya maendeleo ya Sekta kuu za Uchumi wa Zanzibar ambazo ni Biashara, Maendeleo ya Viwanda, Kuimarisha misingi ya ushindani wa kibiashara, ubora wa bidhaa na huduma zinazoingizwa katika soko la Zanzibar, kukuza ushirikiano baina ya sekta binafsi na Serikali na kuimarisha ushirikiano wa kikanda na kimataifa kuhusu biashara na maendeleo yake.

Mhe. Naibu Spika, majukumu hayo ya Wizara ni makubwa na utekelezaji wake unahitaji mashirikiano ya hali ya juu kwani bila ya kufanya hivyo itakuwa ni vigumu kufikia malengo. Pia, majukumu yote hayo yakitekelezwa ipasavyo ni chanzo cha kujikwamua kiuchumi kwa nchi yetu na hivyo tunaweza kufaidika na hali nzuri ya uchumi wa nchi hii.

Mhe. Naibu Spika, katika kipindi cha mwaka 2010 usafirishaji wa bidhaa duniani uliongezeka kwa asilimia 14.5 na kufikia USD 15,129 bilioni, Bara la Afrika liliambulia asilimia 3 ya kiasi hicho ambacho ni sawa na USD 500 bilioni. Kwa upande wa Zanzibar thamani ya usafirishaji bidhaa ilikuwa ni Tshs. 17,906 milioni sawa na USD 11.7 milioni tu. Hivyo, bado kiwango cha usafirishaji bidhaa kinahitaji kuongezeka kwani kiwango cha sasa ni kidogo na hakikidhi haja. Licha ya kuwa kuna sababu mbali mbali ambazo zinaweza kupelekea kiwango cha usafirishaji kushuka zaidi kama vile majanga ya asili (Tsunami, mafuriko, matetemeko ya ardhi na ukame) na pia machafuko ya siasa kwa nchi za Kiarabu. Lakini uwepo wa sababu hizo usitupelekee kupunguza jitihada zetu za uzalishaji na usafirishaji wa bidhaa hizo.

Mhe. Naibu Spika, tumekuwa tukishuhudia kupanda kwa mwenendo wa jumla wa bei za bidhaa na huduma mbali mbali na hasa bidhaa za chakula na nishati. Mwenendo huo umeendelea kuathiri kwa kiasi kikubwa hali ya maisha ya wananchi wa Zanzibar. Kwa mfano, bidhaa muhimu za chakula kama vile mchele, sukari na unga wa ngano. Pia bei ya mafuta nayo ilipanda.

Pamoja na kuwa mabadiliko hayo ya bei ya mara kwa mara yanatokana na sababu nyingi ikiwemo mabadiliko ya tabia nchi, migogoro ya kisiasa kwa baadhi ya nchi lakini bado Serikali kupitia wizara hii ijitahidi kujenga miundo mbinu mizuri ya kiushindani itakayowezesha wafanyabiashara wetu kufanya biashara katika mazingira mazuri ambayo wananchi nao wataweza kumudu bei za bidhaa.

Mhe. Naibu Spika, Sekta ya Biashara, Viwanda na Ukuzaji Masoko imekuwa ikikumbana na changamoto mbali mbali, Wizara kwa kulitambua hilo imeweza kufanya tafiti mbali mbali na kugundua kiini cha matatizo hayo na hivyo kuibua maeneo mapya ya kuyashughulikia pamoja na kuanza utekelezaji wa sera na miradi iliyopo hivi sasa.

Mhe. Naibu Spika, hatua ya kuibua maeneo mapya ni nzuri na ni muhimu na Kamati yetu inaipongeza Wizara kwa hilo.

Mhe. Naibu Spika, naomba sasa nitoe maoni yetu ya Kamati kwa maeneo yafuatayo:

- **Kuimarisha mazingira bora ya ukuzaji biashara**

Mhe. Naibu Spika, Sekta ya Biashara, Viwanda na Ukuzaji Masoko inafanya mapitio makubwa kwenye mfumo wa utoaji wa leseni za biashara nchini ili kurahisisha uanzishaji na uendelezaji wa biashara. Hii itasaidia kuwepo bidhaa mbali mbali sokoni

ambazo mtumiaji atazihitaji na vile vile utakuwepo ushindani mkubwa wa kibiashara utakaopelekea wauzaji kuzalisha bidhaa zao katika kiwango kizuri ili kukabiliana na ushindani wa biashara uliopo.

Mhe. Naibu Spika, kwa upande mwengine utekelezaji wa sheria mbali mbali kama vile Sheria ya Taasisi ya Viwango, Sheria mpya ya ushindani na kumlinda mlaji, Sheria (iliyorekebishwa) ya Mizani na Vipimo na Sheria mpya ya Biashara utaimarisha sana hudumu zilizo bora anazozihitaji mtumiaji.

Mhe. Naibu Spika, uhuru wa kufanya biashara usitumike vibaya na kuifanya nchi yetu kama jaa la kutupa bidhaa mbovu au zile ambazo hazina thamani kwa matumizi ya binadamu. Baadhi ya wafanyabiashara wamekuwa wakileta bidhaa zilizomalizika muda wake wa matumizi na hatari zaidi ni kwamba bidhaa hizo ni za chakula. Kumekuwa na chimbuko na ongezeko la maradhi mbali mbali na ambayo chanzo chake ni matumizi ya vyakula vibovu. Hivyo, Kamati inaiomba Wizara kulisimamia kwa dhati suala hili na kulimaliza.

Mhe. Naibu Spika, ukiachilia mbali bidhaa hizo za vyakula, pia kuna baadhi ya vifaa vya ujenzi. Ni hatari kubwa kutumia bidhaa feki kama vile vifaa vya umeme kwani maharibiko yake yanasababisha madhara makubwa kwa mali na maisha ya watu.

Mhe. Naibu Spika, hivi karibuni Baraza lako Tukufu limepitisha Sheria ya Viwango. Hii ni hatua muhimu sana na utekelezaji wake ni hatua nyengine. Ufanisi wa utekelezaji huo utatokana na kuondoa muhali kwa wale ambao wataleta bidhaa zisizo na viwango. Kwa vile sio bidhaa zote ambazo utazijua uzuri au ubora wake kwa kutumia macho au mkono. Nyenzo pia zinahitajika ili kufanya kazi vizuri na inahitajika kuwepo vifaa vya kisayansi vya kupimia na wataalam wenye taaluma ya kutosha.

Mhe. Naibu Spika, hivi sasa kumekuwa na malalamiko mengi kutoka kwa wananchi kuhusiana na nishati ya mafuta ya petroli na dizeli. Uchakachuaji umekuwa mkubwa sana wakati mwengine mafuta yanapimwa kwa kutumia keni. Halikadhalika, bei zimekuwa zikitofautiana kutoka kituo kimoja hadi chengine.

Mhe. Naibu Spika, kubwa zaidi bei za bidhaa hizi hapa petu hatuzioni kushuka wakati ulimwenguni zimekuwa zikipanda na kushuka. Hivyo, tunaiomba Wizara husika kuhakikisha kuwa bei inaposhuka ulimwenguni basi na hapa nayo ishuke ili kupunguza urari wa bei za bidhaa nyengine.

Mhe. Naibu Spika, Kamati yetu inasisitiza kwa kitengo cha Taasisi ya Viwango *(Zanzíbar Bureau Standard)* ijitahidi kujijenga kwa vifaa na wafanyakazi wenye taaluma ya kutosha. Aidha, kuwe na ukaguzi wa mara kwa mara kwenye maduka na vituo vya kuuziwa mafuta ili kugundua hadaa za baadhi ya wafanyabiashara wanaokiuka maadili na wanapobainika adhabu kali itolewe.

Mhe. Naibu Spika, kwa upande mwengine, katika kuimarisha mazingira bora na ukuzaji biashara Kamati inashauri kuimairisha barabara zetu, umeme, maji, nyanja mbali mbali za mawasiliano na kuangalia uwepo wa masoko ya uhakika. Pia tunaiomba Serikali kuangalia upya zoezi la upunguzaji misamaha ya kodi. Bila ya shaka mazingira bora ya biashara yatachangia kutoa ajira kwa vijana na hivyo kuingizia Serikali mapato.

- **Kukuza biashara za ndani na za nje**

Mhe. Naibu Spika, moja katika jambo ambalo ni kichocheo kikubwa katika kukuza biashara ikiwa za ndani au za nje ni kuwepo na maonesho ya biashara. Biashara ni lazima itangazwe. Haya yanawezekana kwa wafanyabiashara wetu kupatiwa fursa ya

kwenda kwenye maonesho ya biashara nchi za nje (kama *Dubai Export).* Halikadhalika, nasi pia kutengeneza maeneo ya maonesho yetu.

Mhe. Naibu Spika, hapo zamani tulikuwa na mabanda ya maonesho ambayo awali yalikuwepo Mwanakwerekwe na hatimae tukayahamishia eneo la Tunguu. Kwa kiasi fulani tuliweza kufanikiwa sana katika kuitangaza Zanzíbar kibiashara. Cha ajabu maeneo hayo tumeyabadilisha matumizi yake na sasa hatuna eneo la aina hiyo lililo tayari. Tumeelekeza macho yetu huko kijiji cha Dimani, Unguja ambapo wizara imetenga eneo la hekta 60 (1.6 sq km) kwa ajili ya kujenga uwanja wa maonesho ya Biashara. Tunaiomba Serikali kuliona suala hili ni muhimu na kurahisisha ujenzi wake. Ni eneo kubwa na linaweza kuwa lenye kuvutia isipokuwa ni lazima lijengwe kwa mpango mzuri. Ramani yake ioneshe mwelekeo wa matumizi yatakayokidhi haja iliyo endelevu ili liweko kwenye matumizi ya muda mrefu.

Mhe. Naibu Spika, Kamati inaomba sasa hili liwe ni kipaumbele na mara hii liwe eneo la kudumu. Maadam tumeamua isiwe ni kuhama hama kama ambavyo tumewahi kufanya hapo awali. Hii itatutia hasara zisizo na sababu za lazima.

- **Kufanya utafiti**

Mhe. Naibu Spika, utafiti ni muhimu sana katika sekta ya Biashara kwani itasaidia katika kutoa maamuzi makini kuhusu mikakati mbali mbali ya kibiashara na hivyo kuishauri vizuri Serikali katika uimarishaji uchumi na uendelezaji viwanda ambao utatoa fursa za ajira kwa wananchi.

Pia, utafiti unakusudia kuigeuza Zanzibar kuwa eneo tengefu la Uchumi *(SEZ)* na kutayarisha mpango kazi kwa ajili ya utekelezaji wa mapendekezo ya taarifa ya utafiti kuhusu kuogeza

thamani ya mazao (*value chain study*). Hili ni jambo zuri na kamati inasisitiza kuwa tafiti hizo zifanywe kwa lengo la kuifanya Zanzibar kuwa sehemu nzuri ya biashara na hivyo kuimarisha ushindani ndani ya soko la Afrika Mashariki na nchi za jumuiya ya *SADC*.

- **Kuimarisha mazingira ya uwekezaji katika sekta ya viwanda**

Mhe. Naibu Spika, uwekezaji katika sekta ya viwanda ni jambo la msingi na la kuzingatiwa. Ili kuwavutia wawekezaji lazima mazingira bora yaandaliwe ikiwa ni pamoja na kufanya mapitio ya sera za viwanda, kuchunguza vikwazo vinavyokwamisha maendeleo ya viwanda Zanzibar, na kuwekwa mfumo mpya wa vivutio kwa ajili ya kuendeleza sekta ya viwanda hapa Zanzibar. Hivyo, kamati inasisitiza katika jambo hili pamoja kuhakikisha kuwa maendeleo ya viwanda vichache vilivyopo yanasimamiwa ili kuelewa matatizo yaliyopo pamoja na kutoa usaidizi wa kitaalamu ili viweze kuendesha shughuli za uzalishaji kwa ufanisi. Pia tunasisitiza kuwepo kwa *One Stop Centre* kwa ajili ya wawekezaji hii itasaidia katika kuimarisha mazingira bora ya uwekezaji.

- **Kuimarisha mashirikiano baina ya sekta binafsi na Serikali**

Mhe. Naibu Spika, kuwepo mashirikiano kwa sekta binafsi na Serikali kutatoa fursa kubwa zaidi katika kuendeleza uchumi na maendeleo ya nchi. Serikali haiwezi kutoa huduma zote pekee, lazima sekta binafsi isaidie katika kufikia mikakati na malengo mbali mbali yaliyowekwa na Serikali. Hivyo, kamati inapendekeza kuwepo kwa mashirikiano ya karibu kwa sekta hizo. Serikali pia itashirikiana na sekta binafsi katika kutoa ajira kwa wananchi. Katika kulishajihisha hilo ni lazima Baraza la Taifa la Biashara liwe linakutana mara kwa mara ili liweze

kukutanisha wafanyabiashara na Serikali kwa dhamira ya ufanisi wa sekta hii.

Mhe. Naibu Spika, kuna malalamiko mengi ambayo yamedumu kwa muda mrefu sasa yanayohusu ulipaji wa kodi kwa bidhaa za Zanzíbar zinazopelekwa Tanzania Bara. Hasa zile bidhaa ambazo tayari zimeshalipiwa kodi hapa Zanzibar. Madai ya kulipa tofauti ya ziada ni kitendawili ambacho kinahitaji nguvu zetu ili kukitegua. Kwa vile suala hili ni kilio kikubwa sana kwa wananchi wetu, tunaiomba Serikali isikae kitako tena bali isimame kidete kulipatia ufumbuzi wa kudumu tatizo hili.

- **Kuimarisha usafirishaji bidhaa**

Mhe. Naibu Spika, usafirishaji bidhaa nje ya nchi ni jambo ambalo linaiingizia nchi mapato na kunyanyua uchumi wake. Katika kuimarisha usafirishaji wa bidhaa Wizara imeratibu utekelezaji wa Mkakati wa kuimarisha usafirishaji bidhaa *(Export strategy)* ikiwa ni pamoja na uendelezaji wa mazao ya viungo. Hili ni jambo zuri na Kamati inasisitiza suala hili lifanyiwe kazi ipasavyo kwani tunazo rasilimali za kutosha ambazo tunaweza kutumia wenyewe na nyengine kusafirisha kwa ajili ya kutuingizia mapato.

- **Kuimarisha Shirika la Biashara la Taifa *(ZSTC)***

Mhe. Naibu Spika, suala la kuimarisha shirika ni muhimu kwani lina kazi kubwa la kulisimamia zao la karafuu ili liweze kushindana katika soko. Ili kufikia malengo hayo shirika linafanyiwa mageuzi makubwa ya kisheria na muundo wa kibiashara ili liweze kusimamia vizuri uendelezaji wa zao la karafuu na kuweza kushindana katika soko. Mfuko maalum wa kuendeleza karafuu *(Clove Development Fund)* utaanzishwa kwa madhumuni hayo. Kwa hivyo, kamati inasisitiza kusimamiwa

vizuri muundo huo wa shirika ili tufanikiwe katika kuliimarisha zao letu hili tukufu la karafuu.

Mhe. Naibu Spika, tunaishukuru Serikali kwa kuliangalia suala la bei ya karafuu anayopewa mkulima. Kamati ingependa kushauri kwamba kila mara ni vyema kuiangalia bei hiyo. Kila inapobidi kupandisha bei, ni vyema Serikali ikafanya hivyo ili kuwapa motisha wananchi na kuwaamsha ari ya kulithamini zao hilo na pengine nafasi ya kufanyika kwa magendo inaweza kupungua.

- **Eneo la Bwawani**

Mhe. Naibu Spika, kuandaa mapendekezo ya matumizi mbadala ya kibiashara ya eneo la Bwawani na mpango wa uendelezaji wake, ni suala la busara sana. Haipendezi eneo hilo lilivyo hivi sasa linaondoa haiba ya mji, sura iliyopo haileti taswira ya kuonesha kwamba hapa ni mjini. Ile nia ya Rais wetu wa Kwanza Marehemu Abeid Amani Karume ya kulipendezesha eneo lile imepotea kabisa.

Hivyo basi, Kamati inashauri matumizi yanayokusudiwa yawe yenye kuzingatia fursa zilizopo katika eneo hilo ikiwa ni pamoja na kuandaa biashara ambazo zinaendana na uhalisia wa eneo lilivyo.
Mhe. Naibu Spika, tunaiomba Wizara kuchukua jitihada ya utekelezaji katika maeneo hayo mapya ili kutatua changamoto mbali mbali inayoikabili Wizara hiyo.

Mhe. Naibu Spika, Kamati yetu imekubaliana na mapendekezo ya makadirio ya Bajeti ya Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko kwa mwaka wa fedha wa 2011/2012 ambapo Wizara imekadiria kutumia jumla ya Tsh. 2,662,000,000. Kati ya hizo Tsh. 300,000,000 kwa ajili ya kazi za maendeleo, Tsh. 1,462,000,000 kwa ajili ya kazi za matumizi ya kawaida na Tsh. 900,000,000 kwa ajili ya ruzuku kwa Taasisi mbali mbali zilizo chini yake.

Aidha, kwa kipindi hicho cha 2011/2012 Wizara imekadiria kukusanya mapato ya Tsh. 30,000,000.

Mhe. Naibu Spika, kwa niaba ya Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo naunga mkono hoja hiyo na nawaomba Wajumbe wenzangu wamuunge mkono Mhe. Waziri ili Wizara itekeleze majukumu yake ipasavyo.

Mhe. Naibu Spika, nawashukuru wote kwa kunisikiliza na naomba kuwasilisha.

Mhe. Makame MshimbaMbarouk: Mhe. Naibu Spika, nakushukuru na mimi kunipa fursa hii asubuhi ya leo kwanza kutia *fat-ha*. *Inshaallah* kwa uwezo wa Mwenyezi Mungu *fat-ha* hii na sisi masharifu itakwenda vizuri bila ya wasi wasi wowote.

Mhe. Naibu Spika, nimshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia uhai na uzima wetu. Nimpongeze sana Mhe. Waziri pamoja na Naibu wake hasa wanavyokaa pamoja na wakianza kutafsiri hapa na pale ili kuleta mafanikio ya majibu yetu yakawa mazuri.

Mhe. Spika, pia nimshukuru sana Katibu Mkuu wake akiongozana na Naibu Katibu Mkuu pamoja na Wakurugenzi wote wa Wizara hii kwa kutupangia kitabu hichi kizuri chenye sura ya mwelekeo wa uvunaji mzuri wa karafuu hapa Zanzíbar.

Mhe. Naibu Spika, niende katika ukurasa wa 9. Katika mchango wangu Mhe. Naibu Spika, jana hapa nilikuwa nazungumza suala la vijana ili kukua kibiashara kwa kupitia njia ya utalii. Lakini kwa kuweka *hansard* yangu vizuri nimshukuru sana Mhe. Waziri wa Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika, nilipiga kelele sana Jana kuhusu suala la utalii kwa ajira zetu Wazanzibari ambazo tunapaswa tuzifanye basi wanafanya wao wenyewe wazungu kwenye mahoteli. Kwa kweli aliniahidi niende ofisini

kwake asubuhi na nimefika pale na utekelezaji nimeuona haraka haraka na nimeridhika na hivi ndivyo tunavyotaka.

Mhe. Naibu Spika, hatupendi sisi kuwasakama Mawaziri lakini tatizo linatokana na kuwa wananchi wetu huko nje wanadhalilishwa sana. Sasa na sisi ndio wapiga debe wao wa kuwasemea hapa kunako chombo cha sheria na ni lazima tuwe wakali na mtusikilize hatuna chuki na mtu.

Mhe. Naibu Spika, niliona niweze kutoa sifa hizo ili kuweza kuweka *hansard* yangu vizuri na kuonesha kuwa Mawaziri tukikwambieni mnatekeleza. Hilo ni suala ambalo ndio changamoto ya mwanzo.

Mhe. Naibu Spika, nikija ukurasa wa 10 kuna suala la malalamiko. Mhe. Naibu Spika, hapa mimi nitakuwa mkali kidogo, hili suala kila siku tunalizungumza mwisho hapa kuna kifungu kinasema hivi: "Hivyo, Wizara inafuatilia utekelezaji wa utaratibu huo mpya ili kuweza kutoa taarifa hapo baadae."

Mhe. Naibu Spika, kwa kweli hili suala lina muda mwingi sana, wafanyabiashara wetu wanalalamika sana wameshachoka katika kulalamika kwao. Serikali inasema tunalifuatilia tumeshaliamua katika kikao cha pamoja kati ya Tanzania Bara na Tanzania Visiwani. Wameshakaa pamoja wanasema wanatwambia kuwa tayari hili suala limeshaamuliwa lakini bado. Kusema kwa mdomo jamani ni kutokufuatilia bado wanadhalilika hawa wafanyabiashara wetu.

Mhe. Naibu Spika, wakati ule wa Dk. Salmin Amour Juma hebu iangalieni biashara ilivyokuwa imeshamiri Zanzíbar hakuna asiyejua hapa, mahoteli, ma-*guest house,* wachukuaji, wafungaji, wauzaji, watu wanakesha pale usiku, mataifa mbali mbali mpaka *Comorian* watu wanakuja leo wako wapi. Ilikuwa hapa wenzetu hawa wa Tanzania Bara wakija kuchukua bidhaa hapa watu

wanajaa biashara ilikuwa nzuri tu sasa yote imepigwa bao. Biashara wenzetu wameichukua wao sisi tumebakia tuna nyimbo tu sasa hivi nenda katazame pale sasa hivi *wallahi* aibu tupu.

Kwa hivyo Mhe. Naibu Spika, mimi kifungu hichi sijakubaliana nacho kwa sababu naona hakitakuwa na mwelekeo wa kusema kuwa hili suala sasa limemalizika kiuhalali kabisa na sasa hivi wafanyabiashara wanaendelea vizuri.

Mhe. Naibu Spika, kila siku wafanyabiashara wanalalamika, kwani kuna tatizo gani, hebu tuamueni tuseme kuwa *TRA* sasa basi kwani itakuwa nini. Jamani kwa Mungu kunataka ujasiri, sheria wapangaji ndio sisi, sheria wapanguaji ndio sisi, tena kuna ugumu gani.

Mhe. Naibu Spika, biashara Zanzíbar imekufa, yalikuwa yanaletwa magari mengi sana hapa kwa kupitia hapa kuelekea kule Bara, sasa yako wapi hakuna kabisa. Sasa leo itakuwaje Mwakilishi kama mimi nifumbie macho kila siku ninyamaze kwa kumuogopa Mhe. Nassor Ahmed Mazrui nisimwambie nitamwambia, ni lazima nimwambie kwa sababu ndio wajibu wake. Yeye Mhe. Mazrui anajua wapi pakulipeleka hili suala akasema jamani kule hatari sasa hivi shimoni hakuna mchezo watu wamechoka kupiga mabao.

Mhe. Naibu Spika, wananchi wetu wanatwambia kule msifikirie kuwa masihara tunakwenda tu kule kusema kuwa nipeni kura, wanakupa kura kwa masharti sasa hivi. Wanataka kuona jinsi gani unavyowatetea katika chombo hichi. Kwa kweli hili suala Mhe. Naibu Spika, bado hatujalizingatia hatujataka kuwasaidia Wazanzibari kufanya biashara tukubaliane hapo. Tutoe kauli tunaogopa nini kusema kuwa Wazanzibari hatutaki kuwasaidia kufanya biashara kupeleka Tanzania Bara.

Si tatizo wala si aibu, kama tunaogopa aibu basi tuseme kuwa tumeshafuatilia na sasa hebu pelekeni, hebu twende siku moja Mhe. Waziri tulifuatilie hili tuone wafanyabiashara wetu wanavyopeleka zile gari na sisi tufuatilie nyuma halafu tuone. Unasimamia pale pale mhusika jinsi gani anavyolipa au jinsi gani wanavyoachiwa, pale nitasema kweli sasa tumedhamiria Mawaziri kuliondoa hili tatizo. Lakini kwa nyimbo tu hili tutahangaika sana Mhe. Naibu Spika, tunadidimia kiuchumi na kibiashara.

Lakini wenzetu wanapotaka lao mlango wetu upo wazi hichi ndio kitu kinachoniuma. Iweje sisi mlango wetu uwe wazi kwa wanalotaka wao, kuna sheria za maajabu ajabu hapa bahari kuu zimeingizwa sisi tumeshtukizia, mambo ya anga wenzetu walivyokuwa *sharp* imeingizwa sisi tumebakia kutazama macho.

Sasa Mhe. Naibu Spika, kifungu hichi kwa kweli mimi bado kinaniumiza kichwa sijakubaliana nacho. Wazanzibari bado tunateseka sana katika upelekaji biashara kule Bara. Mhe. Naibu Spika, namuomba Mhe. Waziri tujitahidi sana kwa sababu wananchi wetu wanakosa ajira.

Mhe. Naibu Spika, hapo zamani walikuwa wanajaa wafanyabiashara Darajani utawakuta wengi sana pale mpaka saa nane za usiku wana-*pack* mizigo yao. Mhe. Naibu Spika, kwa kweli hili suala linaumiza tena linaniumiza sana.

Mhe. Naibu Spika, niende katika ukurasa huu wa 12, kifungu cha 23 kwa upande wa Zanzibar upatikanaji wa chakula. Mhe. Naibu Spika, ni kweli vyakula vinakuja *Alhamdulillah* tuseme ukweli ulivyo, lakini bado bei zake hazijaweza kuridhisha kwa waletaji wetu.

Mhe. Naibu Spika, katika ukurasa wa 17 tuangalie katika kifungu cha 29, kama tunavyoeleza kuwa maendeleo, inavyoeleza hapa kwenye kitabu, kwamba baada ya Mapinduzi matukufu Serikali ya Zanzibar ilivitaifisha viwanda mbali mbali na kujenga viwanda vipya vikiwemo viwanda vya maziwa.

Mhe. Naibu Spika, kiwanda cha maziwa. Kwanza mimi nataka niulize nani aliyejenga pembeni pale. Katika kiwanda cha maziwa kile tunakijua halafu utaona pembeni pale pamepita uzio mwingine. Hebu Mhe. Waziri nisaidie, kesho wewe ukitaka kufanya *modern* kiwanda kipya cha kisasa unataka kutanua utapeleka wapi na umesharuhusu pale mtu keshajenga uzio, keshajenga nyumba. Mhe. Naibu Spika, mimi nataka niambiwe nani aliyejenga kwa hati gani iliyotoka pale.

Mhe. Naibu Spika, haya mambo mengine tuyafikirie. Mhe. Waziri wewe unataaluma ya kisasa na kwa sababu wewe ni mfanyabiashara, unakwenda nchi za mbali mbali. Leo badala kiwanda kile kukifanya *modified* kidogo kiwe cha *model* ya kisasa unatoa eneo, sasa utakwenda wapi, una eneo tena wewe, huna eneo. Eneo lile zamani limeshatolewa. Mhe. Waziri nataka uniambie lile eneo kapewa nani kusema ukweli.

Mhe. Waziri bora hao watowaji wangesema hivi, maana siwajui ni kina nani, kuwa bora tungewajengea wale wajasiriamali, tungewajengea pale. Mimi ningesema *yes*, viongozi wetu sasa wameamua kuwasaidia wafanyabiashara wadogo wadogo, kwangu mimi lisingekuwa tatizo. Lakini unampa mtu atajirike kuwacha wengi. Hapa ndiko kwenye shida yetu na tutakuwa wakali mpaka dakika ya mwisho na tusemwe potelea mbali. Kwa sababu ndio kazi tulioletewa hapa, tumekula kiapo kwa kushika msahafu mkono na wakati huo tuna udhu. Hatutorudi nyuma *kuntu* tumesema, tutasema ukweli tu. Tunauogopa msahafu mheshimiwa sio masihara.

Mhe. Naibu Spika, ndio maana utakuta aidha, mawaziri au waheshimiwa wanapoanguka katika miaka mitano, ndio yale maneno ya Mhe. Hamza Hassan kwamba utamkuta mtu anafunga susu, nyinyi hamjui tunadhurika kwa nini. Kwa sababu hatuukubali ukweli na hatuusemi kwa kuwatetea wananchi, kutokana na kile kiapo cha msahafu tunakisahau. *Wallah Laadhimu* pale katibu anakukamatisha hivi tunakamata, hatari hiyo na pengine umetoka nyumbani umetia udhu, ni lazima utie udhu kwa siku ile, kwa sababu huwezi kuushika msahafu bila udhu, sheria inakataa.

Kwa hivyo, Mhe. Naibu Spika, naomba hili tuelewe kuwa jamani katika viwanda kama vile kesi zile ziwachwe vile vile. Inaweza kutokezea mtu yeyote anaweza kusema aongeze. Kiwanda cha Sukari Mhe. Waziri usema hapa kuwa imeundwa tume, lakini hiyo tume imeanza kazi yake sasa hivi inatimia muda mwingi sana. Mhe. Naibu Spika, bado ripoti sijaipata, tena nataka ripoti kweli. Mhe. Waziri hebu tunaomba tuletewe mikataba yake, tunaomba utuombee kwenye Baraza hili Mhe. Naibu Spika, tuletewe mkataba wa kiwanda cha sukari, ili tuangalie mapungufu.

Mhe. Naibu Spika, wanasheria tunao. Kina Mhe. Abubakar Khamis Bakary na Mwanasheria Mkuu na mimi mwenyewe mwanasheria nipo, tuangalie mkataba ule pengine una mapungufu ya hali ya juu, pengine hata kodi sijui kama analipa mwekezaji na ndio jambo kubwa katika kosa la mkataba.

Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri wangu mpiganaji mzuri wa biashara utuletee mkataba wa kiwanda cha sukari unasemaje, tutawasaidieni kazi sisi. Kwa sababu tume toka ilipoundwa mpaka leo imeshaota uyoga haijaletwa ripoti, wataalamu wapo hapa Barazani, wataangalia na watasema. Kwa hivyo, mimi naomba Mhe. Naibu Spika, huo mkataba uletwe ili kuweza kufanikisha suala hilo.

Mhe. Naibu Spika, jengine nije kwenye suala la Kiwanda cha Kuku, mheshimiwa hiki kiwanda kina madhumuni ya kutengeneza chakula cha kuku na kuzalisha kuku. Leo vipi inapelekwa saruji, hatari hii. Mhe. Naibu Spika, katika kiwanda kile nasikia hivi sasa kimekuwa ni ghala ya saruji, mashine imeshakufa ile. Kwa sababu vumbi la saruji ni baya kwenye mashine. Kwa hvyo, naomba suala hili kama kweli huyu mwekezaji amefanya hivyo kuweka saruji kwenye kiwanda kile, basi Mhe. Waziri mara moja chukuwa sheria ili afutiwe, kwa sababu lengo letu kuwekeza ili kupata vifaranga, leo tunanunua Bara, wakati sisi wenyewe tunacho kiwanda hapa. Mhe. Naibu Spika, kwa kweli ni kitu cha kuchekesha ni sawa sawa na kiwanda cha sukari, tumemwambia atengeneze sukari yeye anatengeneza spiriti, anataka kutumaliza, maana yake spiriti ni ulevi. Spiriti mheshimiwa wenyewe wakiichanganya wanapata ulevi.

Mhe. Naibu Spika, unafikiria konyagi inatengenezwa na nini kama sio spiriti. Spiriti ile inafanywa konyagi bwana, kwenye picha ya nje kuna mzee kaweka mikono juu. Sasa na sisi tunataka kulewa hapa, sisi hatutaki kulewa bwana. Mhe. Naibu Spika, je mkataba unasema hivyo. Mhe. Naibu Spika, jibu rasmi utaniletea wewe kama ni kweli au sio kweli. Lakini ukweli ni huo. Hicho kiwanda cha kufanyia chakula cha kuku na kuzalisha kuku, tunasikia hiyo ni hali halisi, tuwatafute wawekezaji wenye mantiki hiyo, iambie serikali kuu na sisi tutakusaidia.

Jengine Mhe. Naibu Spika, nije kwenye ukurasa wa 52 kwenye zao letu la karafuu. Mhe. Naibu Spika, ilani yangu ya Chama cha Mapinduzi ni kuendeleza zao hili la karafuu ili kuleta tija kwenye serikali kuu pamoja na wakulima kuweza kujiondolea umaskini. Mhe. Waziri kwanza mimi nikupe pole, kwa sababu bajeti yako haikidhi haja kabisa. Mhe. Mazurui utafanya nini wewe. Jamani kuna wizara ni lazima tuwape fedha za kuweza kuwasaidia hawa wananchi. Leo tunachukua pesa tunakwenda kuwapa fungu la

kuondoa mbwa kichaa. Hizo fedha za fungu la mbwa vichaa mpeni Mhe. Waziri huyu wa Bishara, Viwanda na Masoko, ili atuletee neema hapa.

Yuko wapi Mhe. Waziri wa Fedha, hayupo. Kwa sababu fedha zile akipewa ataweza kufanya viwanda vidogo vidogo. Viwanda vidogo vidogo vipo *SIDO* kule, lakini hana ubawa yule na viwanda vidogo vidogo tutizame wenzetu Bara kule viko chungu nzima, vimetandaa kama uyoga, leo tunashindwa sisi kufanya hivyo. Kuna mafungu yanapelekwa sehemu ambazo hata akilini hayaingii, hao mbwa vichaa wenyewe kwa nadra. Miaka nenda inawezekana mbwa mmoja tu. Mimi nitalipa marisau, kama haja yenyewe ni marisau, ili hilo fungu liondolewe na uletewe wewe Mhe. Mazrui ili tuweze kufanya kazi. Lakini vyengine vyovyote huna bajeti, tutakulaumu siku zote. Mhe. Naibu Spika, kwa kweli inasikitisha mno ni lazima mambo mengine bwana tuwasaidie.

Mhe. Spika, kunatakiwa vitalu vitengenezwe ili zao lile liimarishwe. Mhe. Naibu Spika, mikarafuu sasa hivi imekatwa, hakuna huduma kiasi hicho. Hivi kweli sasa hivi tutapata kama zile tani za kizamani, hakuna tusidanganyane.

Mhe. Spika, kuhusu magendo wamejitahidi kusema ukweli. Niliwaona Mhe. Mazrui na Mhe. Dk. Mwinyi, juzi kwenye televisheni pamoja na Mhe. Makamo wa Kwanza. Lakini jitihada zao zitakuwa hazifai kitu, hakuna mjiti wa kulinda watazipata zile karafuu ndogo tu. Lakini mara hii, kwa asilimia kubwa zitapatikana kwa watu hao niliowaona. Dk. Mwinyi pembeni na mwenyewe Mhe. Mazrui sidhani kama itapenya karafuu. Wameanza vizuri tu kwa kushirikiana na Mhe. Makamo wa Kwanza. Lakini je, hiyo miti yenyewe tunayo. Nalo hili tunaomba Mhe. Waziri kufanywe fungu kwa makusudi na wao wapewe fungu lao la kuimarisha karafuu. Kama maji tulivyofanya, si tumeshakusanya milioni tumezipeleka kule, kwa nini na wao tushindwe kuwatafutia fedha kama hizo.

Kwa hivyo, tuwatafutie tu tuwape hapo ndipo nitakapojua kwamba kweli Zanzibar au serikali yetu inakusudia zao hili kulipa nguvu. Lakini kwa kumuambia tu kwenye karatasi aseme na akishasema keshamaliza kazi yake imekwisha, akifika hapa tumpigie makofi ameondoka na mchezo umekwisha. Tumeokoa nini na tumeleta maendeleo gani. Lakini nimefurahi sana kusikia bei imepandishwa, sasa hapo zitachumwa. Kuna mambo mawili zitachumwa karafuu au mkarafuu utakuja chini, maana yake mtu atataka lazima aipate ile. Mhe. Naibu Spika, lakini turudie na sisi ile ya kizamani kwamba tuwatafutie magunia, majamvi na zile karabai, basi kazi itakwenda vizuri hapo. Najua serikali haina pesa kakope Mhe. Waziri kwa ujanja wako, ili tuliweke sawa hili ili mwananchi yule baada ya kumuongeza bei na kazi hii ya kutafuta magunia na mambo mengine pia uwapatie ili ile *quality* ya karafuu tuweze kuipata, kwa sababu watu wanaanika karafuu ovyo ovyo kwenye barabara, tusidanyanye ulimwengu

Mhe. Naibu Spika: Mhe. Mjumbe bado dakika tano.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Ahsante Mhe. Naibu Spika. Kwa kumalizia Mhe. Naibu Spika, nije kwenye zao la mwani. Zao la mwani ni zuri sana, lakini bado hatujatafuta njia ya kuwasaidia wakulima wetu. Njia rahisi ya kuwasaidia ni kwamba tuwatafutie mashine ya kukaushia. Wale wenyewe wakaushe, basi wale wanunuzi waje pale ndio watapata kuuza vizuri, kuliko hivi sasa wanavyouza varange varange. Kwa hivyo, mimi namuomba Mhe. Waziri awasaidie kwa njia hiyo ya kuwatafutia mashine.

Mhe. Naibu Spika, kwa kumalizia katika kifungu cha 58 kwenye Shirika la Biashara. Shirika la Biashara na Magari *MTC*, mimi niwapongeze sana na hii ndio roho yako. Mhe. Waziri kwa kweli mmewakopesha fedha na wanafanya biashara vizuri sana. Mhe. Naibu Spika, tuwaongezee *fund*, ili waendelee na biashara yao, kwa kweli wanafanyakazi vizuri sana. Mhe. Waziri, Mkurugenzi

wako nampa sifa sana na hivi ndivyo inavyotakiwa ukipewa fedha na serikali kwa kuwatafutia vitu vya umma wananchi basi na wewe uzilinde na uzitekeleze vile inavyotakiwa.

La mwisho sasa la kuagia. Mhe. Naibu Spika, ningemuomba Mhe. Waziri akae na Dk. Mwinyihaji ili pale Darajani mtengeneze kitu kimoja kizuri sana, badala ya kutaka kuyabomoa na yale makotena basi lijengwe jumba la ghorofa la *model* ya kisasa, ili wafanyabiashara wote wawemo mule, ile haiba ya Kizanzibari basi lile jengo liwe zuri kabisa mheshimiwa. Kwa kweli hii itatusaidia sana, wale wafanyabiashara wote mnawaweka mule ndani katika sehemu moja. Hata na ile itakuwa ni *center* nzuri kwa biashara.

Kwa hivyo, Mhe. Waziri kaa na Dk. Mwinyi, fedha anazo, mukae pale ili muweze kutoa *style* ya kupata jengo zuri kabisa ili wafanyabiashara wetu tusiwahangaishe tena huku na huko. Siku hizi ndivyo wanavyofanya wenzetu Bara. Utakuta maghorofa makubwa kabisa, unaanzia chini mpaka juu au chini zaidi unakuta maduka tu. Sasa na ile sehemu pale ni *designer*, mkishakumaliza, mnaanza kugawa wewe ulikuwa na kontena lako nambari fulani, chumba chako hiki na wewe chako hiki. Wallah tutakwenda vizuri sana na tutakwenda na wakati tunaoutaka.

Mhe. Naibu Spika, kwa kuujali wakati wako, kwa sababu kwenye hotuba hii mimi sina buti kubwa kabisa. Sina buti na hasa maneno yangu niliyoyasema kuwa naomba vile vitu nilivyovitaja, naamini Mhe. Waziri utaniletea.

Kwa hayo machache naunga mkono kwa asilimia mia kwa mia, ahsante sana.

Mhe. Rashid Seif Suleiman: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, kwa kunipa fursa hii yakuchangia machache kuhusu bajeti hii ya Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko.

Kwanza namshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa kutupa uhai, uzima na kutupa tawfiq ya kuzungumza katika Baraza hili tukufu. Kwanza mchango wangu wa mwanzo ni juu ya serikali. Moja katika vigezo vizuri vya bajeti ni ile bajeti ya serikali kutoa kipaumbele kwa yale mambo ambayo ni muhimu.

Mhe. Naibu Spika, bajeti hii waliopewa Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko haionekani kwamba kulitumika utaratibu mzuri wa kutoa kipaumbele kwa wizara hii. Kwa hivyo, kama mambo yataendelea kwenda hivi basi kuna wasi wasi wa kufika pale tunapokwenda. Majukumu yaliyokabidhiwa wizara hii na changamoto ambazo ziko katika Zanzibar, Tanzania na ulimwengu kwa jumla yanaonesha kwamba bajeti hii waliyopewa ni ndogo mno, ya kuweza kufikia malengo ambayo kama Waswahili wanavyosema, kwamba ‘mwanzo ni mgumu’. Sasa hapa mwanzo ndio ilikuwa wapewe bajeti nzuri ili baadae mambo yaweze kujiseti.

Mhe. Naibu Spika, baada ya hapo, kabla sijaendelea mbele, labda siku ya Wizara ya Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo naanza kutanguliza swali kabisa. Katika bajeti zilizopita ile ya serikali tuliambiwa na mapema kila wizara na asilimia inayopewa. Sasa hadaa hiyo iliyofanywa ilitupunguzia uwezo wa kujadili katika bajeti ya serikali. Kwa hivyo, mimi nawalaumu sana wale waliotayarisha bajeti hizi za serikali kuwa wamefanya hadaa ya kutokutoa hasa mchanganua wa asilimia za bajeti zilivyotawanywa katika wizara mbali mbali. Naomba suala hili lizingatiwe sana, kwa sababu tunapokuja kuzungumza wizara hii ya biashara halafu ukaambiwa bajeti yake ni tupu *and something billion* kwa kweli inavunja moyo.

Suala la pili ambalo nataka kuzungumza Mhe. Naibu Spika, ni suala la kero kwa wananchi wetu. Tatizo kubwa linalotukabili ni mfumko wa bei hasa bei za vyakula. Mimi nafikiria kwamba

lingepewa uzito mkubwa zaidi wa namna gani ya kushughulikia huu mfumko wa bei, pamoja na yale ya mwanzo niliyosema bajeti ndogo, lakini tulikuwa na mjadala mkubwa kuhusu kuanzishwa kwa ghala ya akiba ya chakula. Mhe. Naibu Spika, wataalamu wanaoizungumza kuhusu ghala ya akiba ya chakula inakuwa na malengo mawili makubwa.

Lengo la kwanza kwa bahati liko kule, ghala hii ya chakula ilikopelekwa. Lengo la kusaidia juhudi za wakulipa wakati yanapotokezea majanga ya kimaumbile, yaani *natural disasters*, kama wakati wa kuja kwa ukame au kuja kwa mafuriko mazao yakaharibika. Pia ni sehemu moja ya matumizi ya ghala ya akiba ya chakula.

Mhe. Naibu Spika, madhumuni ya pili ya ghala ya akiba ni kusawazisha bei za vyakula wakati yanapotokezea mabadiliko katika soko la kiulimwengu. Kweli sisi hatuna *control* ya soko la ulimwengu, lakini tukiwa na chakula ndani ambacho kilinunuliwa katika hali nafuu, wakati ulimwengu unapotikisika katika bei za vyakula basi wahusika wa ghala ile kwa mujibu wa sheria inavyosema, wanatoa chakula kile na kukiuza kwa bei ambayo wananchi itakuwa ni nafuu kwao. Ndio maana mimi katika michango yangu mingi ninasema sana, kwamba wizara mbili hizi ni lazima zishirikiane kuanzisha na kuendeleza ghala ya akiba kwa sababu madhumuni ni mawili makubwa. Wizara ya Kilimo na Maliasili na Wizara hii ya Biashara, Viwanda na Masoko.

Mhe. Naibu Spika, lakini wakati wenzetu Tanzania tayari wanayo ghala ya akiba nah ii mara kwa mara Mhe. Rais wa Jamhuri ya Muungano anapohutubia huwa anatoa mpaka takwimu ya kiasi gani chakula walichonacho. Sisi tunasua sua hatuna, hii ni hatari na huku kusema kwamba tuta-*stabilize* bei za vitu bila ya kuwa na ghala ya akiba, tutawashughulikia wakulima bila ya kuwa na ghala ya akiba, haiwezekani. Sasa bajeti hii niliifikiria mimi kwamba kutakuwa na fungu fulani ya kuanzisha kununua hiyo

ghala ya akiba, kwa ajili ya chakula ambacho kitawekwa katika ghala kwa ajili ya mambo mawili yanapotokezea.

Sasa tukisema tumo katika ya matayarisho ni lini kitanunuliwa chakula hicho, lini ghala litawekwa, hatuwezi kufikia kabla hatujaanza na tunaweza tukaanza na tani tano tu. Lakini tukishaanza inajulikana kwamba sasa huu mpango umeshaanza. Kwa hivyo, napenda nimuulize Mhe. Waziri je yazungumze katika kiwango gani huko serikalini hili suala la ghala ya akiba ndio imeachiwa Wizara ya Kilimo na Maliasili na Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko haimo katika hili lengo la pili au vipi, naomba aje atueleze. Kwa sababu inawezekana sisi tunafahamu vyengine na serikalini nako kuna jambo jengine. Kwa hivyo, bora ate atueleze ili tukubaliane mambo mawili, kwa sababu hayo ni mambo ambayo yamo katika sheria za kimataifa.

Halafu Mhe. Naibu Spika, suala la tatu ni juu ya huu urari wa bidhaa zinazoagizwa na zinazosafirisha na Zanzibar. Hili ni suala la changamoto kubwa ni lazima tufike wakati tuwe na mkakati japo mdogo, lakini tuweze kuimarisha katika hali ya usafirishaji ili kupunguza huu urari mkubwa wa tunavyoagiza na tunavyosafirisha.

Mhe. Naibu Spika, juzi katika mchango wangu kwenye Wizara ya Kilimo na Maliasili, nilisema kule sokoni tunakokwenda hizi bidhaa zetu za matunda tusiwe na *fector* za kujidanganya lazima takwimu zetu ziwe sahihi. Nilitoa mfano kwamba hivi viazi vitamu nilikwenda sokoni nikaviona vipo vinatoka Iringa. Sasa tukiendelea na hali hii tunaweza tukajikuta sio kwa tunachosafirisha tu, hata hiki tunachokula karibu chote kinatoka nje ya Zanzibar. Ni lazima tufike wakati tukubaliane kwamba tunaendesha vipi hayo mambo. Hii ni wizara ya tatu ambapo wakishirikiana ingekuwa na jukumu la kuanzisha mezani kubwa za barabarani. Wizara ya mwanzo ni wizara ya fedha tutakuja tuiambie nayo, wizara ya kilimo nimeshaiambia juzi na leo

naiambia wizara ya biashara kwamba ipo haja kubwa ya wizara tatu hizi kuzungumzwa na kupata mwelekeo wa kuanzisha mezani zile kubwa za barabarani ili kuona ni namna gani nchi yetu inavyokwenda katika mambo hayo.

Mhe. Naibu Spika, katika suala langu moja la hapa Barazani niliuliza katika mchango wangu nilioutoa kwamba tayari imeshaonekana *potential* ya kuwa sisi tunaweza kuzalisha chumvi. Sijui ni kitu gani tunachosubiri ili waje watuambie wataalamu gani kwamba huu mpango tuuendeleze. Hatuwezi kuanza kila kitu tukazalisha siku moja, ni lazima tutaanza na *item* moja moja, tunaongeza katika idadi yetu. Sasa chumvi imeshaonesha kwamba iko *potential* na liko soko katika *SADEC contries*, ni sababu zipi za msingi zilizoonesha kwamba wizara hii bado haijaitilia mkazo suala la uzalishaji chumvi na kuona kwamba sisi tunaanza kusafirisha chumvi kwenda katika maeneo mengine.

Mhe. Naibu Spika, suala la viwanda au maendeleo ya viwanda. Kuna mambo mengi ambayo mimi nimeyaona yanahitaji kuangaliwa. Sera iliyoandikwa haisemi chochote utekelezaji wa sera yenyewe, kwa kuendelea kuandika sera tukazitawanya basi hazifahamishi kitu chochote ulimwengu, bali ni lazima sera ile itafsiriwe kivitendo ndio itakuwa ni sera. Sasa kuna changamoto nyingi kuhusu viwanda.

Mhe. Naibu Spika, changamoto ya kwanza, tulikuwa navyo viwanda vidogo vidogo karibu vyote vimekufa. Je, ni utafiti gani uliofanywa ambao unaonesha kwamba viwanda vile vilikufa kwa sababu moja, mbili, tatu au nne. Ikiwa viwanda vya aina ile vinatufaa tufanye nini ili tufufuwe ari ya viwanda vile au wawekezaji wa viwanda vile.

Lakini na msemaji wa mwanzo alizungumza katika kitu ghali hapa Zanzibar ni ardhi pamoja na kote ulimwenguni. Mhe. Naibu

Spika, maeneo haya ya viwanda ambavyo vingi vikimilikiwa na serikali yapo, sasa kwa nini hayapewi udhibiti na wizara hii na ikawa na udhibiti kamili kuhusu maeneo haya tena bila ya kuyaachia.

Kwa hivyo, kama wizara haijachukua udhibiti na kiwanda kimefungwa, yaani hakipo na wala hakifanyikazi tena, basi wako wajanja wataingia. Kwa kutokana na hali hiyo, wapeleke waraka serikali kwa ajili ya kupewa udhibiti wa maeneo yote ambayo yalikuwa na viwanda na hivi sasa vimekufa, ndio itaonekana kwamba kweli wako *serious*. Lakini watu wengine wataanza kuja kuchukua nafasi na kutumia njia mbali mbali.

Suala jengine ni kupitia sheria za nchi. Je, sheria za nchi zilizopo zinatoa kipaumbele cha wawekezaji kuwekeza katika viwanda? Hivi kweli mwelekeo wa nchi unatoa nafasi ya uwekezaji katika viwanda, kwa sababu viwanda vinataka mambo mengi.

Vile vile jengine je matatizo yaliomo ndani ya muungano yanatoa changamoto gani kwa wawekezaji ndani ya viwanda? *(Makofi)*

Hivi sasa Mhe. Naibu Spika, tungetegemea kwamba Zanzibar kwa sababu inanunua umeme kwa pamoja, yaani *bulk purchase* ya umeme ingenunua umeme *TANESCO*, kwa sababu *TANESCO* ndio mwenye umeme.

Kwa mfano, juzi Mhe. Naibu Spika kutokana na matatizo ya umeme ambayo yako Tanzania Bara, alikuja mwekezaji kutoka Marekani na kusema yeye umeme wake anazungumza na *TANESCO* na wakikubaliana basi atawasha majanareta yake, kwa sababu yeye anataka kumuuzia *TANESCO* na wala hakuiuzia *EWURA*.

Sasa hili tatizo la Zanzibar kwamba sisi tunanunua umeme *TANESCO* lakini bei wanatupangia *EWURA* kama kwamba

wanatupa wanatuungia *line*. Kwa kweli *EWURA* ni Jumuia ambayo inaunga *line* na wala hauzi umeme kwa jumla isipokuwa inauza na kuunga ule umeme mdogo mdogo.

Kwa hivyo, Zanzibar kukubali kununua umeme *EWURA*, halafu *ZECO* wamuuzie kiwanda wakati kwa Bara itakuwa sivyo hivyo, itakuwa ama wananunua *TANESCO* au *EWURA*, lakini huyu mtu wa tatu itakuwa hayupo.

Mhe. Naibu Spika, moja kwa moja haiwezekani kabisa kusema kwamba bei ya umeme inayouziwa kiwanda cha hapa cha Zanzibar ni sawa na bei ya umeme inayouziwa kiwanda cha Tanzania Bara, mimi sikubali hata siku moja kwa *process* hii. Je, hii si sababu kwamba watu hawataki kuwekeza hapa kwa sababu ya bei kubwa ya umeme?

Sasa yote tuyatizame, ndio maana tukawa tunasema kwa kelele kwamba tutafute nyanzo vyetu vya umeme, ili tuweze kutoa umeme kwa viwanda ambavyo viko tayari kuwekeza hapa Zanzibar. Lakini *process* hii tunayokwenda nayo hii ni sawa na mimi nakwenda kuuza mchele kwa *packet*, lakini nakwenda kununua kwenye duka la reja reja haielekei.

Kwa mfano, ikiwa ninazo fedha za kununua *packet* 100 au 200 nende tena nikanunue kwenye duka la reja reja na yule aniambie ngojea kidogo kumbe yeye amekwenda kununua na kuniletea kwa nyuma.

Mhe. Naibu Spika, siku hizi Dar-es-Salaam kuna utaratibu mmoja, ukenda kununua kitu na akeshakujua kitu kile kipo pahala fulani, basi anakwambia kiko *store* subiri kidogo baada ya nusu saa pita itakuwa tayari tumeshakileta kumbe vile amekwenda kununulia duka jengine na baadaye akubandike, sasa kama hivi ndivyo tunavyobandikwa kuhusu umeme hapa Zanzibar.

Kwa kweli sisi tunanunua umeme 60 *Mega Watts* za umeme zinatumika hapa Zanzibar hivi sasa, tunanunua kwa *EWURA* na halafu mwenye kiwanda aje hapa kwa ajili ya kuwekeza. Mhe. Naibu Spika, naomba mlitizame sana suala hili. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, wataalamu wa uwekezaji wanasema mwekezaji anapokuja anatizama mambo matano. Kwanza anatizama elimu za watu waliopo pale, halafu anatizama ujuzi walionao, je sisi hivi viwanda ambavyo tunataka kuviekeza hapa tayari tumeshawatayarisha watu katika ujuzi wa ngazi au fani hizo.

Vile vile suala la uaminifu unatizamwa, uchapaji kazi ambapo humu Mhe. Waziri ameyataka baadhi ya mambo hayo namshukuru sana ameyaona, namna gani watu wanachapa kazi. Pia suala la utamaduni wao vipi na ile mali.

Mhe. Naibu Spika, moja tatizo ambalo linapigiwa kelele Mahonda na pengine watakaokwenda wataliona, kwamba hakuna staha ya ile mali iliopo pale. Kwa hivyo, uwekezaji wa kilimo una matatizo, kwa sababu huwezi kulinda ile mipaka yake kwa kikamilifu na tofauti na viwanda ambapo kutajengwa kuta pamoja na walinzi.

Kwa maana hiyo, utamaduni wa watu wetu lazima tutizame, pia *culture* ilivyobadilika, watu wanavyostahi mali za watu wengine.

Mhe. Naibu Spika: Mhe. Mjumbe, dakika 20 zimemalizika nakuongeza na dakika tano. *(Makofi)*

Mhe. Rashid Seif Suleiman: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, kwa heshima ulionipa.

Kwa hivyo, baada ya kuzungumza suala la viwanda nataka nizungumzie Shirika la *ZSTC*. Mhe. Naibu Spika, *ZSTC* ni shirika

linalofanyakazi vizuri tunashukuru kwamba wameona kupitia wizara yao kuongeza bei ya karafuu. Kwa kweli jambo la kujitahidi wao ni kupunguza urasimu, yaani watu wanaokwenda kuuza karafuu wasisumbuliwe, pia kama inavyowezekana kuzidisha vituo kwa pale ambapo kuna umuhimu wa kuzidisha vituo.

Lakini kuna changamoto ndani ya hili shirika. Kwanza ni idadi ya wafanyakazi waliomo, ili kufanyakazi kwa ufanisi inabidi wawe na wafanyakazi kiasi. Kwa hivyo, serikali haina budi kuona kwamba kuna changamoto hiyo katika shirika hili.

Pili ambapo humu sikuiona au sikusikia ni kuhusu Tawi la Shirika liliopo pale Dar-es-Salaam. Kwa kweli mara nyingi tulipopita na ziara za kamati tulishauri tawi hili kwa sababu ya kukua harakati za kibiashara pale Dar-es-Salaam, waingie sasa kikamilifu katika harakati za kibiashara bila ya kuogopa sasa, ili waweze kulitononosha hili shirika.

Sasa sijui hali hii Mhe. Waziri imefikia wapi, yaani namna gani Tawi la Dar-es-Salaam linavyotumiwa na *ZSTC*, ili kuweza kuliendeleza hili shirika, kwa sababu hali ya biashara ya Dar-es-Salaam imekua sana na matumaini makubwa yapo.

Kwa mfano, juzi tumesikia hapa *PBZ* imeanzisha Tawi lake Dar-es-Salaam kuonesha zile harakati za kibiashara na mambo mengine zimekua. Kwa hivyo, hebu tupe Mhe. Waziri ni vipi Shirika letu la *ZSTC* litajiimarisha katika Tawi lake la Dar-es-Salaam.

Mhe. Naibu Spika, suala jengine Mhe. Waziri hakutueleza ni lini na wao watajenga ofisi, kwa sababu kwa hapo walipo haipendezi kuitwa Ofisi mpya ya Biashara, hivi akija mwekezaji basi atauliza hii ndio ofisi yenyewe basi atarudi. Kwa hivyo, naomba atueleza

na yeye amepangiwa lini kupata jengo la ofisi kama kiwanja anacho au vipi?

Mhe. Naibu Spika, naomba univumilie nitoe la mwisho kabisa pale uliponiambia unazo dakika tano nilikuwa katika viwanda na nililisahau moja, lakini hili litakuwa la mwisho kabisa.

Mhe. Waziri ameeleza kwenye hotuba yake kuhudu *Processing Industries* za mambo ya matunda. Mhe. Naibu Spika, napenda kumuuliza tu kwamba hii ni *idea* nzuri sana na ndio inayotufaa sisi.

Kwa hivyo, kwa kupitia wizara yake tutegemee mchango kiasi gani atakaoutoa kupambana na hawa nzi wa embe pamoja na wadudu waharibifu wa matunda, ili na yeye imuwezeshe pamoja na wajasiriamali kuweza kuyatumia haya matunda, kwa sababu hivi sasa hayakamuliki, matunda yote yameharibika na wala hayakamuliki. Lakini tukifanya juhudi ya pamoja, basi naamini kwamba tutafikia.

Kwa hiyo, namuomba atueleze Mhe. Waziri amechukua juhudi ya kiasi gani, kwa sababu yeye anatafuta nini, ile *product* ya matunda.

Mhe. Naibu Spika, baada ya hayo, naomba kuunga mkono hoja. Lakini namuomba Mhe. Waziri asijeakaliacha hata neno langu moja swali yangu kunijibu kama ni hivyo, basi buti lipo. Ahsante sana. *(Kicheko/Makofi)*

Mhe. Subeit Khamis Faki: Nakushukuru sana Mhe. Naibu Spika, kwa kunipa fursa ya kuchangia hotuba ilioko mbele yetu ya Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko.

Mhe. Naibu Spika, mchango wangu nataka nianze kwenye biashara ya taifa ya karafuu. Kwa kweli naishukuru sana Serikali

ya Mapinduzi ya Zanzibar kuona kwamba kuna haja ya kuongeza bei ya zao letu hili la karafuu, ambalo kwa muda mrefu wananchi wa Zanzibar walikuwa wameshakata tamaa kwa biashara hii. Lakini hivi sasa naona kuwa serikali imekusudia wakulima wa zao hili la karafuu wafanyekazi ya kulihuwisha zao hili la karafuu.

Mhe. Naibu Spika, baada ya kutangazwa bei mpya ya karafuu, basi wananchi wengi wa Zanzibar hivi sasa wanajiandaa. Kwa hivyo, naiomba Wizara hii ya Biashara, Viwanda na Masoko, kwa sababu siku za nyuma ilikuwa ikikaribia zao la karafuu, basi waliokuwa na harusi walikuwa wakikopa vitu vya harusi, wanataka nguo kwa sababu ya zao hili, yaani kabla ya kuchuma zao hili pamoja na mambo mengine kama hayo.

Vile vile kulikuwa na utaratibu kupitia shirika hili kama wale wafanyabiashara wa karafuu walikuwa wakikopeshwa fedha pamoja na kupewa zana za kuendeshea kambi zao. Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri aone kama kuna haja ya kufanya hivyo, ili kuwapa kipaumbele zaidi na kupata hili zao vizuri zaidi.

Mhe. Naibu Spika, pamoja na bei kubwa iliyotangazwa na serikali, lakini namuomba Mhe. Waziri ajue kwamba walanguzi na wao tayari wameshaongeza bei. Hivyo, serikali ikae na ione ifanye jitihadi, ili wasiweze kulipata tena walanguzi zao letu hili la karafuu, kwa sababu wakiongeza basi na serikali ikiona kuna haja ya kuongeza nayo iongeze. Kutokana na hali kama hiyo, nadhani itafikia pahala walanguzi watatua silaha chini. *(Makofi)*

Jambo jengine ninalomuomba Mhe. Waziri, ili kudhibiti zao letu hili la karafuu, yaani watu waweze kulichuma kwa haraka na kuweza kulipata kwa ajili ya kukuza biashara yetu. Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano wakati anapotangaza bei za gari za abiria huwa anatangaza kwa ajili ya vituo vyote vya magari ya abiria.

Mhe. Naibu Spika, namuomba Mhe. Waziri aone kuna haja baada ya kutangaza bei ya karafuu, sasa kusimamia na bei ya vibarua, yaani wale wachumaji wa karafuu. *(Makofi)*

Kwa hivyo, kwa sababu gani nasema hivyo. Mhe. Naibu Spika, matajiri wa karafuu wana ila moja, ila yao karafuu zikiwa juu anahimiza na kutaka haraka zije chini. Sasa kuna baadhi ya mataji wa karafuu kwa sababu sote tumeshafanyakazi hiyo, zikeshachumwa zile karafuu sasa wale vibarua anawaona hawana thamani na kuwadharau pamoja na kuwakejeli. *(Makofi)*

Kwa maana hiyo, ikitangazwa bei ya vibarua basi tajiri yeyote atakayekiuka ile bei iliyotangazwa na serikali atakuwa yumo kwenye hatia. Sasa yule tajiri atakayeona mimi karafuu zangu nataka zichumwe haraka na kuongeza bei zaidi basi serikali imruhusu aweze kuongeza bei, kwa sababu karafuu zake anazitaka haraka watu wazichume, hiyo ikiwa ataongeza bei zaidi kuliko ile iliyowekwa na serikali basi ni ruhusu. *(Makofi)*

Lakini hapa *target* iwe yule anayeshuka zaidi kwa ajili ya kuwatesa wale vibarua, sheria iweze kumnasa. Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri aone kwamba kuna haja ya kutangaza bei ya vibarua, yaani wale wachumaji wa karafuu na iwe ni bei ya taifa, nadhani hapo itakuwa tumefikia lile lengo.

Mhe. Naibu Spika, suala jengine ambalo nataka nilizungumze katika ukuzaji wa biashara. Hivi sasa tumeshaingia katika Soko la Afrika ya Mashariki. Kwa kweli namshukuru sana Mhe. Waziri kwamba kuna changamoto nyingi sana amezionesha zinazotukabili. Sasa biashara hii tunayoingia katika Soko la Afrika Masharika sisi Zanzibar kama alivyosema Mhe. Waziri inaonesha kwamba tuko chini katika usafirishaji wa biashara.

Kwa hivyo, ni vyema Mhe. Waziri aone kama kuna haja ya kila njia kufanya kila utaratibu, yaani yeye awe mbunifu wa kufanya

utaratibu wa kila aina kwa ajili ya kukuza hii biashara na kupata kuongeza usafirishaji wa biashara nje.

Mhe. Naibu Spika, juzi nilipokuwa nikichangia kwenye Wizara ya Kilimo na Maliasili kwenye mazao nilizungumza suala la chumvi kama alivyozungumza Mhe. Rashid Seif Suleiman, kwa bahati nzuri Mhe. Waziri alinijibu kwamba nisubiri atakapokuja Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko.

Kwa kweli nilizungumza kwamba ukanda wa Mashariki wa Pemba, yaani karibu hivi sasa sehemu zote wanazalisha chumvi na bahati nzuri chumvi inapatikana kwa wingi. Lakini wafanyabiashara wetu masoko yao wanauza mule ndani tu, wakati mwengine chumvi inakuwa inakaa na kuwa nyingi sana.

Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri aone kama kuna haja ya hawa wazalishaji wa chumvi, kwanza kupewa elimu zaidi na halafu kuwezeshwa, ili wazalishe zao hili kwa wingi zaidi na iwe ni biashara moja tunayouza nje. Mhe. Naibu Spika, biashara ya chumvi si lazima tukauza China, Marekani na sehemu nyengine za mbali, lakini wenzetu wa Congo, Rwanda, Malawi hawana bahari, kwa hiyo sisi itakuwa tunawauzia ni sawa na kuwa tunauza kwa bei ya nje. Hivyo, ni vyema kuna kwamba kuna haja ya kufanya kila njia ya kupata kiwanda cha ku-*pack* ile chumvi na kufungwa vizuri na halafu watafutiwe soko kwa ajili ya kuuza. Kutokana na hali kama hii itakuwa tunakuza zaidi biashara. *(Makofi)*

Nikiendelea na mchango wangu sasa naomba nizungumzie kuhusu suala la viwanda. Mhe. Naibu Spika, sote ni mashahidi na tunajua kama kuna maeneo ambayo yalitengwa maalum kwa sababu ya kuwekeza viwanda. Kwa mfano, ilikuwa ni sehemu yangu ya Micheweni kwa Pemba na Fumba kwa Unguja ilikuwa ni maeneo ya uwekezaji na hasa ukizingatia ukanda wa Micheweni upande wa mashariki ya kusini ya Micheweni katika

ule ukanda uliowekwa wa kuekeza, yaani ulitengwa kwa ajili ya kuweka viwanda.

Mhe. Naibu spika, nasema lengo la serikali ni kuwekeza. Lakini bado serikali haijaweka mkazo katika suala zima la kuwekeza. Kwa nini niseme hivyo, kwa sababu Mhe. Waziri mwenyewe ameonesha changamoto zinazotukabili kuwa wawekezaji wanakuja, lakini bado hawajawekeza. Kwa kweli sababu alizoziweka kwamba hakuna miundombinu kama vile barabara, umeme, maji, yaani hakuna chochote.

Kutokana na hali hiyo, mwekezaji atakwenda kuekeza maporini ambako hakuna chochote, yaani hivyo anavyotaka kwenda kuekeza atajenga vipi hivyo viwanda vyake wakati hakuna *facilities* zozote. Kwa hivyo, naiomba serikali ione kwamba kama imekusudia kuekeza kwa ukweli, basi ione kuwa kuna haja ya kuweka miundombinu yote ambayo inahitajika kuwepo kule, sasa mwekezaji atakapokuja atakuwa hana sababu ya kwamba asiwekeze.

Mhe. Naibu Spika, wakati atakapokuja mwekezaji akapekewa na kuona hiyo barabara ya kufika kule Maeneo Huru basi ni shida kufika, hawezi kukubali kuwekeza. Kwa maana hiyo, serikali ione kama kuna haja ya kufanya hivi sasa kila mbinu ya kuwa sasa wale wawekezaji atakayekuja asirudi tena, kwa sababu wanakuja lakini wanarudi kutokana na kuona kwamba hakuna hiyo miundombinu.

Suala jengine kama alivyozungumza Mhe. Rashid Seif Suleiman. Kwa kweli moja miongoni mwa sababu tosha ni umeme, jamani kila siku tunapiga kelele katika Baraza hili kwamba wakati umefika sasa wa kuwa na umeme wetu mbadala, pia kila wakati nawaeleze kwamba mtutegemea cha ndugu hufa masikini.

Mhe. Naibu Spika, hivi tutakuwa tunasubiri umeme wa kugaiwa mpaka lini, wakati kila siku tunaambiwa kwamba wanakuja watu na kufanya utafiti na kuona kwamba Zanzibar upo uwezekano wa kupata umeme wetu mbadala. Kwa mfano, tumenunua majanareta 32, lakini majanareta haya yanakwenda kwa fedha nyingi sana kwa sababu mafuta yake ni ya aina yake, hivi kiasi gani cha fedha zinazoteketea kwa majanareta haya. Sasa kama tungekuwa tayari tumeshaweka umeme wetu kiasi gani cha fedha tungekiongoa.

Kwa hivyo, naomba Mhe. Waziri aone kwamba hivi sasa wanapokaa kwenye *Cabinet* wazungumze suala hili na kuona kuwa ipo njia ya kupata umeme wetu na wala tusitegemee umeme ule tu, kwa sababu wawekezaji watakuja na kuondoka, kwani wanajua umeme wa kugaiwa haina muamana, kwa sababu leo upo na kesho haupo. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, hili ni moja ambapo serikali bado haijawa tayari, ndio maana nikasema hivyo na kama serikali itakuwa tayari basi wawekezaji wakija hawataondoka. *(Makofi)*

Kwa kweli Zanzibar ni njema atakaye aje kila siku tunasema na kila mtu anaipenda Zanzibar hii, kwa sababu watu wako tayari kuwekeza. Kwa hiyo, tuwekeni miundombinu watakapokuja wawekezaji wasiondoke. Kwa mfano, kila siku mimi nakuja kuzungumza kwamba Micheweni inaongoza kwa umasikini *Wallahi* kule kukiwekwa viwanda viwili tu basi watu wa Micheweni tayari ule unyonge waliokuwa nao utawapungua.

Mhe. Naibu Spika, naomba kwamba muone kuwa ipo haja ya kukuza viwanda, kwa sababu Afrika ya Mashariki kama hatuna cha kuuza basi sisi tutadumaa, yaani wenzetu watatupita na sisi tukae. Kwa kweli kwa bahati nzuri masiki Wazanzibari ni wabunifu sana, lakini suala hili bado, kwa sababu mimi nataka mtu aniambie ni sehemu gani ya nchi hii iliko ulimwenguni

asimkute Mzanzibari tena hamkuti amekaa tu, yaani anamkuta ni mfanyabiashara au taji mkubwa.

Kwa hivyo, kuna haja ya kutumia rasilimali aliyotupa Mwenyezi Mungu ya mbinu zetu tulizonazo, ili Zanzibar hivi sasa iondokane na tulipo na tusogee mbele.

Mhe. Naibu Spika, suala jengine ambalo nataka kulizungumza ni kuhusu suala la biashara la wafanyabiashara wetu watoto. Mhe. Naibu Spika, namuomba Mhe. Waziri aone kwamba hivi sasa tumefika pahala ya kuwajali wafanyabiashara wadogo, kwa sababu na wao ni wachangiaji wa kodi zilizopo Zanzibar na hawa ndio rasilimali zetu. Vile vile ni moja ya kupunguza umasikini na kuleta ajira, kwa sababu wale wafanyabiashara wadogo wanazoajira ambazo wamejiajiri wao wenyewe binafsi.

Kwa mfano, wenzetu kule Tanzania Bara walipokuwa wanataka kuwatoa Wamachinga pale Kariakoo walikwenda kuwajengea nyumba za ghorofa na kwenda kuwaeka pamoja na kwamba baadhi yao wanakaa na wengine hawakai. Mhe. Naibu Spika, juzi niliona vurugu iliyotokea Mwanza na kusababisha watu kufa.

Kwa hivyo, na sisi Mhe. Naibu Spika, siku za nyuma tulikuwa na tatizo la wafanyabiashara wadogo waliopo pale Juakali, hali hiyo ilisababisha sisi kutumia fedha nyingi sana, kwa sababu Baraza la Mji lilikuwa likiweka askari ambao wakilala pale kutwa kucha, yaani asubuhi, jioni, usiku na mchana. Kwa kweli askari wale walikuwa wakilipwa pamoja na kula, sasa kazi ngapi ambazo walikuwa wakizifanya waliziacha na kwenda kukaa pale kwa ajili ya kwenda kuwalinda wafanyabiashara.

Mhe. Naibu Spika, namuomba Mhe. Waziri tusiende kwa kuvurugana na vyema ashirikiane na Mhe. Waziri wa Nchi (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kuona kwamba Manispaa

hivi sasa wale watu wetu isiwe kila mara wanakwenda kuvurugana pamoja na kupokonywa vitu.

Kwa kweli wafanyabiashara wale ni masikini tena wanakuwa wamekwenda kukopa fedha za watu na amekwenda pale kwa sababu amejiajiri na Manispaa wanakwenda pale na kuvuruga vitu vyote na kuchukua na inapelekea kukosa hata kile cha kuanzia msingi na mtu amekwenda kukopa fedha za watu.

Sasa namuomba Mhe. Waziri aandae utaratibu mzuri akaae na wafanyabiashara wale wadogo, kwa ajili ya kupanga na kukubaliana na kuwakweka sehemu ambayo itakuwa na maslahi, ili waendelee kufanya biashara zao bila kubughudhiwa na kupata tabu katika nchi yetu.

Mhe. Naibu Spika, hivi sasa nchi yetu tunamshukuru Mwenyezi Mungu hapa alipotufikisha tupo katika hali nzuri, sasa yale mambo ya kuhangaishana, kunyang'nyana pamoja na kupokonyana vitu yafe na wala si tabia nzuri. *(Makofi)*

Kwa hiyo, namuomba Mhe. Waziri akae nao vijana kwa ajili ya kuwapa elimu nzuri, wakubaliane na utaratibu ili twende kiutaratibu kama Zanzibar ilivyokuwa ina wastaarabu basi twende kistaarabu.

Mhe. Naibu Spika, suala jengine ninalotaka kuzungumza ni suala la wafanyabiashara wakubwa ambao wanauza vyakula. Mhe. Waziri katueleza hapa sababu za upandaji wa vyakula, kwa sababu wananchi wetu walio wengi suala la vyakula linawagusa na linawaumiza walio wengi, mpaka sisi tuliokuwemo humu. Suala hili umetueleza sababu zilioko duniani mpaka kupanda vyakula bei tunakubali sisi.

Lakini tunachokiomba ni kwamba na wafanya biashara na wao wawahurumie wananchi wetu wasijue kupandisha tu lakini wajue

kuteremsha, bei zinavyopanda duniani sawa nawapandishe lakini bei zinavyoteremka nao wateremshe, lakini wao wanajua kupandisha tu kuteremsha hawajui, kupandisha ni haraka sana lakini kuteremsha hawaji. Kwa hivyo naiomba serikali kupitia wizara hii ya biashara iwe wasimamizi wazuri wa kuwasimamia hawa wafanya biashara na kuona kwamba bei ikipanda tupande, lakini ikiteremka tuteremke nayo, isiwe wanajua kupandisha lakini kuteremsha hawajui.

Kwa hivyo hili pamoja na kwamba umetwambia mmepanga kamati maalum ya kusimamia lakini naomba hii kamati ya kusimamia pamoja na kuwa mnasema mmekaa vizuri na wafanya biashara mkipanga, lakini mpange na hili nalo mlione. Biashara ya mafuta inapanda na kushuka lakini kushuka haishuki inapanda tu lakini vyakula vinapanda tu lakini kushuka haijui hata hiyo bei ikija ikianza basi ndio moja kwa moja haiteremki tena, sasa huko duniani hivi vyakula vinapanda tu havirudi ninavyoelewa mimi ni kwamba kuna kupanda na kushuka. Kwa hivyo ikishuka tushuke nayo tuone bei inatangazwa mpya na ikipanda tuone inatangazwa bei mpya.

Mhe. Waziri mimi kutokana na bajeti yako ilivyo naona sina buti mimi nakuunga mkono na nakutakia uyarekebishe hayo niliyoyasema ishaalla naunga mkono hoja. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika: Naomba niwatambulishe kwamba katika bajeti yetu hiyo amehudhuria Rais wa Jumiya ya wafanya biashara pamoja na makamo wake, naomba wasimame ili waheshimiwa wawajue. Ahsanteni sana.

Mhe. Hassan Hamad Omar: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, na mimi nashukuru sana kunipa fursa hii kuchangia hotuba ya Waziri wa Biashara Viwanda na Masoko nakushukuru sana.

Kama ulivyoelezea muda wetu ni mfupi na kuna wachangiaji wangine wanataka kuchangia naenda moja kwa moja katika mchangio wangu, kwanza kabisa nachukua fursa hii kuipongeza serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar pamoja na wizara husika ya Biashara Viwanda na Masoko, hivi karibuni kuweza kutangaza bei ya wakulima wa zao la karafuu tunaipongeza sana Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kupitia wizara husika kwa bei hiyo, wananchi sasa hivi wamefarajika vya kutosha na tayari wamejipanga kukabiliana na kulichuma zao hilo. Wananchi wa Zanzibar wana matumaini makubwa katika serikali hii ya umoja wa kitaifa na dalili njema sasa hivi tunaziona, mojawapo ni hiyo kupandishwa kwa bei za karafuu.

Mhe. Naibu Spika, pamoja na kupanda kwa bei ya karafuu lakini zao hili linateketezwa sana kwa kusafirishwa magendo pamoja na kupanda bei, lakini kama alivyozungumzia Mhe. Subeit Khamis Faki muwakilishi wa Micheweni basi na walanguzi nao wameshajipanga vizuri sana, wanashindana na serikali tunaomba kwa kuliokoa zao hili serikali kupitia wizara husika ijipange vizuri kwa sababu bei zilizotangazwa ni bei za matumaini kabisa hakuna sababu zao hili kusafirishwa kwa magendo. Ndio maana takwimu zikawa ndogo hazipatikani kwa sababu hiyo.

Mhe. Naibu Spika, kwa kweli zao hili la karafuu sasa hivi watu wameshaanza kudondoa na baadae litakuwa limeshamiri Zanzibar nzima, lakini kuna watu wanaolinunua zao hili yaani karafuu mbichi pia na kuikata mikarafuu hili liko wazi naomba kwa nguvu zetu zote ili mikarafuu isipotee tudhibiti mambo haya.

Mhe. Spika, pamoja na kupandishwa kwa bei ya karafuu lakini na mfumko wa bei wa vyakula unaendelea siku hadi siku na baada ya kupandisha bei hii ya karafuu, wenye vyakula nao watapandisha zaidi na zaidi hasa kwa mwezi huu mtukufu wa ramadhani, isiwe huku tumepandisha bei kuokoa wananchi na huku bei ikawa zinafumka zaidi itakuwa tuko pale pale hatujafanya kitu chochote,

kwa hivyo Mhe. Waziri wa Biashara Viwanda na Masoko ukabiliane nalo jambo hili kwa kina kabisa. Yaani nakuomba ukae na wafanya biashara wawaonee huruma wananchi wetu kila siku isiwe bei zinafumka tu zinakuja juu hazirudi chini, hii ni kuwatia wasi wasi wananchi wetu wenye matumaini makubwa na serikali hii ya umoja wa kitaifa ambao shughuli zake tunaziona zina matumaini makubwa sana kwa wananchi wetu.

Mhe. Naibu Spika, jambo jengine ni kuongezwa vituo hivi vya ununuzi wa karafuu shirika liongeze vituo kwa sababu wananchi wengi wanapata usumbufu kwa kwenda kuuza mazao haya sehemu mbali mbali, kwa hivyo mule mwenye upungufu muongezwe vituo.

Mhe. Naibu Spika, jambo jengine tunaomba ulinzi uimarishwe kweli kweli bila ya kuimarishwa na kusimia vizuri basi bado tupo pale pale, kwa sababu wizara hii ni ya biashara na nazani tuna wafanya biashara wadogo wadogo ambao wanapata usumbufu pale jua kali, kama tumekubali katika kuinyanyua Zanzibar basi wafanya biashara wale tusiwaone maadui, tuwaone ni watu wenye kuisaidia Zanzibar. Kwa sababu za msingi kuna wafanya biashara kule Tanzania Bara wanaitwa machinga wapo, na hata hawa machinga wengine walio sehemu mbali mbali hata Ulaya wapo sijui wanaitwa vipi, sisi hapa Zanzibar tunaita watu wa jua kali, lakini hata ulaya wafanya biashara kama vile. Kwa hivyo tunaomba hawa wasionekane maadui na tuwape kipaumbele kuwaboresha ili waweze kufanya kazi zao vizuri na kwa ufanisi na kuwasaidia wananchi wetu.

Mhe. Naibu Spika, imezuangumziwa habari ya viwanda katika kitabu hiki kama palikuwa na viwanda vingi lakini viwanda vyote vimekufa, na kama nchi haina viwanda basi umasikini hapo hauondoki hatuna uwezo wa viwanda vikubwa, lakini hata hivi viwanda vidogo vidogo kama vya mafuta ya nazi, palikuwa na viwanda vya sabuni na viwanda vya aina mbali mbali hapa

vilikuwa vinasaidia kama ilivyoelezwa katika kitabu hiki basi kulikuwa na ajira mbali mbali za viwanda hivi. Lakini bado viwanda hivi vimekufa tunamuomba waziri wakati huu tunaona kwa nyie watu wa miundombinu vifufuke ili wananchi wetu wapate ajira.

Mhe. Naibu Spika, nikiendelea na michango yetu hii kama ilivyoelezwa alizungumza mwenzangu hapa Mheshimiwa wa Micheweni, imetajwa bei ya wakulima wa karafuu lakini bei ya wachumaji haikutajwa hili ni tatizo tunakuomba Mhe. Waziri ulichukue na kwa muda mfupi tupate tangazo lako kama wachumaji wa karafuu nao wamesikia bei yao ya kuchumia karafuu ili nao wahamasishike, bihairi ya hivyo wakulima watakuwa wanawaumiza sana hawa wachumaji au vibarua wao.

Mhe. Naibu Spika, baada ya mchango wangu huu mfupi mimi na wananchi wangu wa Jimbo la Kojani naunga mkono hotuba hii ya bajeti mia juu ya mia. Ahsante sana *(Makofi)*

Mhe. Asaa Othman Hamad: Nakushukuru Mhe. Naibu Spika, na mimi kupata fursa ya kuweza kusema machache kwenye bajeti hii ya Mhe. waziri wa Biashara Viwanda na Masoko, kwanza namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia kufika jioni hii ya leo tukiwa wazima wa afya, lakini pia kwa fursa maalum ambayo tumeipata nimpongeze sana Mhe. Waziri kwa hotuba yake nzuri kutokana na watendaji walioko kule juu wameipanga kiasi kwamba waheshimiwa wajumbe wa Baraza hili waweze kushawishika kwa namna moja pamoja na mapungufu mengi wanayokabiliana nayo.

Mhe. Naibu Spika, nimpongeze tena Mhe. Waziri kwa kuwa muwazi na sifa yake nyengine ni mkweli, ndani ya kitabu ameyaeleza mapungufu anayokabiliana nayo katika utendaji wa siku hadi siku lakini nimshukuru tu pamoja na watendaji wake wakuu yale mapungufu makubwa ambayo yanamtatiza yeye na

wenzake amepanga kuyachukulia hatua, kama vile sheria ya biashara ya mwaka 1989, sheria ya mizani, sheria ya ushindani na mengineyo. Kwa sababu tuna tatizo hatujui mipaka ya Wizara hii ya Biashara yeye na Manispaa ukiliuliza hili kwa nini Manispaa hamuchukui hatua anakwambia aa, ukiuliza watu wa Biashara wanakwambia sio letu ni la Manispaa, watu wa manispaa nao wana maduka yao hayana leseni wala hayana lolote ni yao wao kwa namna wanavyojua.

Mhe. Naibu Spika, kunakosekana mapato kwenye maduka maduka yetu mengi yapo hayana leseni na hayana kwa sababu yamefichwa na wenzetu, ni imani yangu sheria hii itasaidia kufafanua utatahuu. Mhe. Waziri tulimbebesha lawama hata juzi aliposema mapembe basi yakafufurisha bei mpaka ikawa kizaa zaa kwa nini basi hatoi kauli wafanya biashara wanapandisha wanavyotaka wao, lakini kumbe hana meno anaweza kupiga kelele lakini hawezi kukamata. Sheria hizi zitamsaidia watendaji watapata ari lakini sasa niende ndani ya kitabu.

Mhe. Naibu Spika, mimi nitaanza na changamoto Mhe. Waziri kasema huko changamoto zinazomkabili ni pamoja na uwezo mdogo wa uzalishaji wa ndani, wazalishaji wa ndani na wale wajasilia mali kawaida hawa huwa wanawezeshwa, wenzetu duniani Mhe. Waziri ni mambo anayoyafahamu vizuri kuna hata wale wa biashara za kutwa wanakopeshwa na taasisi za fedha wanarejesha kwa kutwa, wako wa mwezi na wako wa mwaka. Kwa hali za watu wetu ni lazima wasaidiwe katika mfumo ambao utawezesha wao kufanya kazi hizi na kupunguza hili wimbi hususan la vijana na mtihani uliotukumba hapa visiwani.

Mhe. Naibu Spika, kina mama tumewaona Wazanzibari wana uwezo mkubwa wa kibiashara lakini tatizo tumelikuta kwenye fedha hii ya mamilioni ya JK na AK namna yalivyokuwa, hatimae malalamiko sasa wengine wanashindwa kurejesha wamepewa wale ambao hawana sifa za kupewa, lakini wizara hii kwa ilivyo

jipanga sasa wakipewa fedha hii na wakipewa fursa ya kutembea juu na chini atasaidia. Chini kwa kupita ndani juu na angani sio chini ya bahari atakuwa na uwezo na safu aliyopangiwa kule juu ya kuwasaidia Wazanzibari kwa sekta hii ya biashara.

Mhe. Naibu Spika, kuna mwitikio mdogo wa masuala ya viwanda nashukuru kwamba sasa tumetanabahi kwamba ilikuwa ni ndoto za alinacha kuzungumza uchumi kumbe hatuna viwanda, hatutoweza kukuza hali hii tuliyonayo kiuchumi kama hatukuwa na viwanda pengine viwanda vilivyoanzishwa miaka ya sitini hatukujipanga ndio maana ni magofu matupu hii leo, leo Mhe. Mazrui kajipanga na safu yake. Lakini naomba sana Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar hebu t umpingueni hizi pingu za mashaka ya kule kwenye muungano, kwasababu atapanga vizuri ataandaa sera safi wafanyabiashara bado watakuja kukwamishwa pahala padogo tena sehemu ndogo tu bandarini Dar es Salaam kwa kweli mutatudhoofisha kwa hiyo, tunaomba haya mazungumzo yafike pahali yaishe sio yasite mazungumzo yanazungumzwa kuhusu kero hata sisi mzitwambie mambo ya kero nendeni wenyewe tu, lakini tunataka wafanya biashara wetu wawe wanafanya shughuli zao kwa raha mustarehe.

Viwanda pia vina mkono wa wawekezaji kuwekewa vikwazo, hapa kwa sababu kwenye bajeti hii pia tumesema kwamba tunataka wazalendo kipaumbele, wawekezaji wa nje namba mbili. Lakini bado tuna tatizo anakuja muwekezaji mifano mingi ipo anaomba mzunguruko unamchukua miaka, tulisema kwamba tutakuwa na *one stop centre* lakini hii haitatusaidia katika vita vya uchumi jamani, akija mtu wa *ZIPA* mtu wa Uhamiaji hayupo, akija Uhamisaji mtu wa Ardhi hayupo. Kuna watu hadi leo wameomba lakini *release* haijatoka mzalendo wa hapa hapa sasa haya ni matatizo, naomba sana katika suala hili Mhe. waziri pale utakapoona aah niambiwe baraza wenzako ndio sisi tunataka tupungue na lawama zisizokuwa za lazima kwako, tupambane na wale vikwazo kwa sababu ardhi ni ya serikali watendaji

wanalipwa na serikali, mimi sioni sababu kwa nini wakwamishe watu.

Mhe. Naibu Spika, zikiwa shughuli zake ni biashara sasa zitakuwepo kwa njia ya bahari na angani, hili hatuna mjadala nalo kazi yetu sasa ni kuboresha maeneo haya mawili yawavutie wawekezaji wetu, marafiki zetu na mabalozi wetu kama tunao hao watatu kutoka Zanzibar wafanye hiyo kazi watusaidie. Serikali ikitaka itawaongeza wengine lakini kwa hivi sasa nasikia wako watatu katika sitini na ngapi sijui, sasa serikali tunaiambia tuna suala la uchumi Zanzibar titamie balozi hizo za Tanzania Wazanzibar nao waongezeke, mabalozi wako kule kazi moja ni kuwavuta wawekezaji kwenye nchi zao sasa balozi anayetoka pembe yoyote ya Tanzania anavutia Tanzania ya huko kwao, Zanzibar wako watatu sasa hivi serikali tunaiomba izitizame. Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Makamo wa Pili wa Rais ananisikia.

Mhe. Naibu Spika, tumeuza nje hapa inaonyesha dola 2.08 za Marekani tatizo letu hatuna viwanda tuna ardhi ni finyu lakini tuna bahari, nazungumza tena kwamba mgodi wetu ni bahari hivi ni visiwa ni vipi tutaitumia bahari kuzalisha vilivyomo ndani ya bahari tutaweza kusafirisha na kufaidika ndani, lakini kama bado bahari ile tunaiona ipo kupita kwenda Pemba na Dar es Salaam na Tanga kilichomo ndani ya bahari bado na kama tunavyosema tutavitumia wee lakini bado, bado hadi lini hii bado haina mwisho.

Mhe. Naibu Spika hivyo hivyo vilivyomo kuna wazalishaji wenzangu tuseme wazalishaji wa chumvi Pemba mashariki, Mhe. Waziri nitakuomba uje kutoa kauli lini watapata kiwanda cha kuisarifu chunvi yao itusaidie sisi na wao kwenye haya masoko yetu ya kikanda ipo nyingi, umasikini wao wote wala hawakipeshwi benki zatu bado hazijawasaidia lakini kwa juhudi zao hizo hizo na wajumbe hawa waliomo humu ndani ndio

wanaofanya kazi hiyo, lakini sasa ameshafanya kazi mpaka karundika humo ndani na juzi nilisema kuna mzalishaji ana paketi mia mbili ndani hana vya kufanya, lakini lazima kujengwe utaratibu wasaidiwe hawa. Hili nitamuomba Mhe. Waziri aje na jibu.

Lakini jengine Mhe. Naibu Spika, karafuu zimetwaja lakini nimekuja kutishwa na kushangaa kwamba kushuka kwake ni pamoja na uhaba wa ardhi, ningekuwa kule kwetu ningesema taireni lakini hapa nasema sikubali sio kweli ardhi hii hii ambayo ni kweli inapungua lakini miaka ya sitini inatoa tani sitini elfu ikizalishwa hapa karafuu, leo imefika tani 2. mnakuja kutaja ardhi kwa nini hamsemi tulilidharau zao na wakulima wakulima wakaliacha, wachaga kule Mhe. Naibu Spika, baada ya kahawa kushushwa bei waliikata wakapanda tungule kwa sababu ni nipe nikupe wanauza wanapata. Leo sisi tuliiwacha mikarafuu ikafa wakati ni zao ambalo tulikuwa tunalitegemea katika nchi hii maisha yetu yote yalikuwa ni karafuu, lakini tukabweteka tumetulia izaliwayo inatiwa kenye gunia inapelekwa Indonesia hakuna utafiti unaofanywa hakuna lolote haya ndio matatizo na maradhi makubwa ya hapa kwetu.

Mhe. Waziri utafifi sasa hivi kwenye zao la karafuu ni lazima ufanywe kwa sababu ile ni miti kama binaadamu anavyoumwa na kwenda hospitali na kufa na yenyewe sasa imesibiwa na ilichokisibu, mkarafuu ukiupanda hauoti iliyopo inakufa kwa ari kubwa ati unakuja kusema ardhi, ardhi imefanya nini kwani. Hilo lilikuwa ni wajibu wetu wenyewe kuuchunga mkarafuu kuhakikisha uhai wake ni endelevu kwa maslahi yetu.

Mhe. Naibu Spika, la mwisho mwisho muda haupo tena sasa nivumilie tu nimalizie ni huu usanifu wa bidhaa umegawika kama nilivyosema kwenye kitabu, wandani chini ya APZ na wa soko la ndani uwekezaji huu bado uko pale pale kwenye viwanda na viwanda vyetu Mhe. Waziri, sisi ni viwanda vidogo vidogo na

viwanda vya kati ndivyo tutakavyomudu hapa visiwani hatuna viwanda vyengine, lakini Mheshimiwa anasema sababu kubwa ya kukosekana hiyo mambo ya usanifu kwa kwetu yale maaneo maalum yaliyotengwa na miundo mbinu hafifu ya umeme, barabara, maji na kule Fumba na Micheweni hakukutumiwa suala la Fumbe na Micheweni sitaki nilirudie. Sisi tunachosema jamani suala la maji Mungu katupa yapo suala la umeme una matatizo hata huko kwa wenzetu tunakochukua, tumetia mkataba na *TANESCO* lakini msemaji ni *EURA* mambo haya mmeyaona wapi isipokuwa hapa, hatuwezi sisi kulipa *EURA* sio mkataba wetu.

Mimi nimemuomba Mhe. Shamhuna kwa kweli kuja kutoa pesa ukamlipa *EURA* tutakushitaki, sisi hatuna mkataba na yule tuna mkataba na *TANESCO* mikataba yetu na makubaliano yapo kaja mtu kati sasa hivi ndio msemaji hatukubaliani nae kwa hilo. Tunasema kwamba hizi mambo ya Micheweni na Fumba tunaitaka Zanzibar serikali itangaze eneo lote ni huru, Zanzibar ni yetu Wazanzibari wanataka kauli hiyo wafanye shughuli zao, hakuna sababu ya kurudi nyuma kwa suala hili.

Mwisho Mhe. Naibu Spika, Mhe. Waziri namuomba sana wafanya biashara Pemba wanasumbuka mno wanasumbuka miundombinu ya bandari hawana, leo unapotaja kwamba kwa sababu meli hazifiki na shehena zao kwa sababu ya bandari kwa Zanzibar kauli hii ni aibu maumbile yetu sisi ni bahari, bandari Mkumbuu ipo hamutaki kuiboresha. Bandari ya Malindi hamutaki kuikuza, Bandari Wete mnasema kuna mwamba mnataka Mungu awape nini hata museme mmepewa. Mimi nataka ukija uje na jibu lini bandari ya Wete itakuwa na heshima ya kuwa bandari kwa watu wa Mkoa ule wa Kaskazini, iweze kuwaletea manufaa. Bandari ile inategemewa na watu wa Kaskazini wote na kisiwa chote, watu wa Mombasa, Pemba, Tanga lakini leo hata jahazi maji yakipwa halifiki ukutani halafu mnakuja kulalamika na bandari tutawaelewa sisi hatukubali kwa hilo.

Meli hizi muwawezeshe wafanya biashara mimi nasema hii ni makusudi sijui kama Waziri ana mpango na kule Bara ivi kwa nini meli isiweze kuja hapa, tulisema tupanue bandari Malindi hatuna pesa mimi nakubali hatuna uwezo huo, naheshimu sana muda wako Mheshimi Naibu Spika, lakini leo unanikata kasi kwa hapa pagumu sana. *(Makofi)*

Mhe. Rufai Said Rufai: Mhe. Mwenyekiti, nashukuru kupewa dakika hizi tano zilizopo awali ya yote nimshukuru Mwenyezi Mungu kutujaalia mchana hii kupata nafasi fupi ya kutoa mawazo yangu mawili matatu na kuipongeza Wizara hii ya Biashara Viwanda na Masoko kwa umahiri wake na kuleta tija kwa kazi zake na wananchi wetu.

Mhe. Naibu Spika, Mimi nianze katika ukurasa wa 57 kwa biashara hii ya mwani, biashara hii ya mwani kwa hapa kwetu Zanzibar imeanza muda mrefu sana lakini kwa kipindi hiki pia niipongeze Wizara ya Biashara Viwana na Masoko kuona kwamba katika biashara hii ya mwani ina tija na pato kubwa la nchi, kutokana na wafanya biashara walivyoibuka kuupandisha mwani bei na wao kuona kwamba sasa tathmini iliyopo ili kufanya utafiti wao ili mwaka unaokuja wa bajeti kuingizwa katiba suala la biashara. Kwa hivyo naipongeza sana Wizara hii ya biashara kuona kwamba wananchi wetu wanaozalisha zao hili la mwani na wao watakaposhindana na hawa wafanya biashara wanaweza kupata tija haraka wananchi wetu ili kuweza kupata maendeleo haraka.

Mhe. Naibu Spika, lakini pia tuzungumze suala zima ambalo juzi tu serikali imetangaza kwamba zao la karafuu wanalipa kipaumbele ili kumnyanyua mwananchi wetu na kuweka mifuko mbali mbali ya kuwezesha suala hili, lakini Mhe. Naibu Spika, kuna tatizo la haya mashamba ya karafuu tulipofanya ziara kwenda kuangalia shamba la karafuu pale Makuwe ni shamba moja kubwa adhimu ambalo la serikali ambalo linaipatisha

serikali tija kutokana na shamba lile. Lakini tatizo lililopo shamba lile lina wafanyakazi saba na shamba hili bado lipo porini linasafishwa hapa machoni tu pa watu wanapokwenda wakiona lile shamba na pale serikali inapata mapato mengi sana.

Kwa hivyo ningeliiomba sana Wizara lile shamba ni lao walihuwishe ili lilete mazao kwa wingi, kwa sababu mkarafuu uliopo pale kila mkarafuu mmoja una uwezo wa kuzalisha pishi katibuni mia na kitu, lakini ndio shamba limetupa liko porini. Kwa hivyo ningeliishauri sana serikali kwamba hili shamba walidumishe na walihuwishe. Lakini pia kuna mashamba ya serikali yale yaliyokatwa eka wale waliopewa yale mashamba wameyaua, mimi nasema kwamba wameyaua kwa makusudi pengine ni shamba ambalo halimhusu wala halimkeri asubiri lizae apewe kama ngawa aweze kulichuma lile zao.

Kwa hivyo ningeliishauri serikali mashamba yale yakaangaliwa kwa kina na wananchi waloyabeza yale mashamba waweze kuondoshwa na kupewa watu wengine ambao watayahusisha na kuanzisha miti miti ya mikarafuu, lakini pia ningeliiomba wizara kuwashughulikia wafuaji wa nyuki hawa wanaitekeleza mikarafuu kwa wingi kwa hivyo wangelifuatiliwa ili waweze kuwa wafugaji wa kisasa, wasiwe wale wafugaji wanaokwenda kuziua nyuki kwa kutumia moto, kwa hivyo suala la moto ni suala moja linaloangamiza mikarafuu yetu.

Lakini pia Mhe. Naibu Spika, sasa hivi watu wanachuma karafuu lakini tayari wameshaanza kupokea matatizo kwa upimaji wa mizani, wananchi wetu wanaanza kulalamika kwamba mizani wanayopimiwa aidha mpimaji au mizani yenyewe zinaanza kufifiliza watu wetu wanaouza karafuu. Nahisi kwamba ima mizani tunazozitumia ni za muda mrefu au wapimaji wanaanza kuwanyang'anya wazalishaji wetu, kwa hivyo ningelimuomba sana Mhe. Waziri watu suala linalowarudisha nyuma wakawa hawaiuzii sana serikali ni kuona kwamba ameshapima pishi zake

kumi ana uhakika kwamba atapata laki moja, lakini akifika anapata thamanini elfu. Kwa hivyo akija kwa mtu wa pembeni huku anachukua laki yake moja na ishirini haina mashaka kwa hivyo hawa watu hawa wanunuzi hebu washughulikie ili wananchi wetu wasipate matatizo.

Kwa hivyo Mhe. Naibu Spika, kwa kweli muda hautoshi na nilikuwa nina mengi lakini ishaalla tutaonana jioni.

(Saa 7.00 Mchana Baraza liliahirishwa mpaka Saa 11.00 Jioni)

(Saa 11:00 jioni Baraza lilirudia)
(Majadiliano yanaendelea)

Mhe. Rufai Said Rufai: Ahsante Mhe. Naibu Spika, kama nilivyosema mchana katika kitabu hiki cha hotuba ya Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko imejieleza kwamba ina mpango wa kutaka kuanzisha biashara katika eneo la Hoteli ya Bwawani. Mhe. Naibu Spika, ni muda mrefu sana eneo lile limekaa wazi. Kwa kweli uwazi ule hauna tija na faida yoyote inayopatikana Zanzibar.

Naipongeza sana Wizara hii ya biashara kuliona lile eneo kwamba lina uwezo wa kuweza kuibadilisha Zanzibar kwanza kutokana na ile hali iliyopo. Kwa kweli ile hali iliyopo hairidhishi, ni hali mbaya duni. Lakini wenzetu hawa wa Wizara hii ya Biashara wameliona lile eneo kwamba linaweza kuleta tija na faida kwa kizazi kilichopo na kijacho baadae. Kwa hivyo, niwapongeze sana Mhe. Waziri, Naibu Waziri na watendaji wake wote kwamba ubunifu wao huu waliouwona Mungu awajaalie uwezo lile eneo liweze kutusaidia Wazanzibari ili tuweze kubadilika na biashara hii tuliyonayo.

Mhe. Naibu spika, niseme kwamba kuna maeneo haya, Maeneo Huru. Tunasema kwamba ni muda mrefu toka kutangazwa

Maeneo Huru. Lakini faida ya yale Maeneo Huru hadi kufikia sasa haijaonekana faida yake. Mimi nahisi kutangaza tu sio kufanya. Kwa hivyo, tokea kutangazwa basi muda umekuwa mrefu. Ningeliomba sana Wizara hii ya Biashara ili kuikuza biashara Zanzibar. Basi ni vyema eneo lile la Fumba wakati tayari limeshapimwa, wakaliandaa wakapeleka miundombinu, anayehusika na maji akapeleka maji, anayehusika na umeme akapeleka umeme kule, ile wawekezaji wetu waweze kuja kuekeza katika maeneo yale ya Fumba.

Biashara ni mashindano, biashara ni kubadilishana mawazo baina ya mtu kwa mtu, baina ya nchi na nchi. Kwa hivyo tunapoweka mabanda ya biashara pale inawezekana Zanzibar iakabadilika kwa muda mfupi kutokana na hali ya sasa tuliyonayo. Ningelikushauri sana Mhe. Waziri hili alifumbulie macho yote, pamoja na wizara yake. Ili lile eneo wananchi waweze kufaidika haraka iwezekanavyo.

Mheshimiwa pia kuna hizi biashara ndogo ndogo. Wanapiga kelele sana wafanyabiashara wetu wadogo wadogo. Imekuwa kana ni ujanja kwa wafanyabiashara wakubwa. Tunajua kwamba wafanyabiashara wadogo wadogo wengi wanachukua biashara zao kwa wafanyabiashara wakubwa. Tatizo linalojitokeza ni vipi Mhe. Naibu Spika. Wafanyabiashara wetu wanakwenda kuchukua biashara leo kwa wafanyabiashara wakubwa, lakini kesho bei aliyomuuzia mfanyabiashara mdogo ndiyo anayouza *cell* kwa mwananchi wa kawaida. Hili naona ni njia moja ya kuwakwamisha wafanyabiashara wetu wadogo wadogo. Sasa kama kweli una malengo ya kupunguza bei bidhaa zako kwa nini huanzi kumpunguzia mfanyabiashara huyu mdogo bidhaa hii akaweza kumudu ili na yeye akaweza kupata maslahi ya kufaidika yeye pamoja na familia nyengine. Kwa hivyo nahisi huu mpango unaoendelea sasa hivi ni mpango wa kuwarudisha nyuma na kuwakatisha tamaa wafanyabiashara wetu wadogo wadogo ambao

wanachukua mizigo hii hapa hapa Zanzibar kwa wafanyabiashara wakubwa.

Ningeiyomba sana serikali iangalie sana. Kwa sababu unapokwenda kwa wafanyabiashara wakubwa wanapoweka zile leseni zao, unaweza ukachukua siku tatu au nne bado hujafika pale unapokusudia kupata ile bidhaa. Kwa maana hiyo utasabisha wezi waporaji, wanyang'anyaji, watatokea kwa sababu msongamano wa watu umekuwa mkubwa. Kwa hivyo kama na hawa wafanyabiashara wadogo kama *cell* yao waliyoweka na yeye atapata faida kidogo huku, basi tayari watu wale wangelikuwa wanaenea maeneo mbali mbali na biashara ingelikuwa inakwenda vizuri na vibaka wasingekuwa rahisi kuweza kuvamia maeneo kama yale.

Mhe. Naibu Spika, hili ni tatizo. Kwa hivyo ni vyema serikali ikae macho sana na kudhibiti masuala kama haya ili wafanyabiashara wetu wadogo wadogo waweze kuimarika na wao. Kwa sababu wafanyabiashara wadogo hawa ndio wanaotupatishia pato zaidi, kwa sababu kila mara wananchi wananunua. Ni vyema serikali ikafumbua macho kwa wafanyabiashara wetu wakubwa ili na wao kuwaenzi wafanyabiashara wadogo.

Mhe. Naibu Spika, nataka nimalizie kwa kuwesema suala hili lifuatalo. Kikao kilichopita tulipitisha sheria. Kwa bahati nzuri juzi Spika, ametutangazia kwamba Mhe. Rais tayari sheria hizi ameshazipa OK, mambo ya kudhibiti vitu vilivyobora. Lakini mpaka hivi sasa Mhe. Naibu Spika, Zanzibar bado tunaingiziwa vitu ambavyo havifai. Tunaingiziwa biashara kama mafriza mabovu, makongwe kabisa, maredio, matelevishen, magari na mambo mengine mbali mbali. Nahisi kwamba kama Wizara hii haitajipanga vizuri bado Zanzibar itakuwa ni jaa la kutupia takataka za nchi nyengine.

Ningelimuomba sana Waziri suala hili kulisimamia kwa hali na mali ili kuhakikisha kwamba tumeondoka pale tulipo na tumepiga hatua nyengine mbele. Ili kuinusuru Zanzibar ni kama tunavyoona sasa hivi maradhi ya aina kwa aina yameibuka katika nchi yetu ya Zanzibar. Tatizo ni nini? Tatizo ni kuingiziwa vitu ambavyo vimekwisha wakati. Vitu hivi vinasababisha maradhi na mambo mengine mbali mbali. Kwa hivyo unapopita katika maeneo ya barabara kuna maeneo mengine ukiyakuta hivyo vyombo ambavyo bado vinatafuta wateja basi haviwezi tena kuondoka pale vilipo vikafika eneo jengine, kwa hivyo ndio vimeshaganda, havijulikani wapi vipelekwe.

Ningelimuomba sana Mhe. Waziri, masuala ya kuletea takataka ya vitu ambavyo vimepitwa na wakati ajaribu sana kulisimamia suala hili ili tuweze kuwa na Zanzibar mpya. Na hizi sheria tulizoziweka ziweze kufuatwa.

Mhe. Naibu Spika, kwa hayo machache na yale niliyoyasema mchana mimi pamoja na wananchi wangu wa jimbo la Tumbe, tunaiyunga mkono hotuba hii ya Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko mia fil mia. Ahsante.

Mhe: Abdalla Juma Abdalla: Mhe. Naibu Spika, na mimi nakushukuru kwa kunipatia fursa hii ya kusema angalau maneno machache katika Wizara hii muhimu kwa uchumi wa nchi yetu.

Mhe. Naibu Spika, mimi kwanza nataka nianze katika masuala ya bei za bidhaa. Bidhaa hizi tunazoagizia nimezigawa katika mafungu mawili. Fungu moja nimeziita bidhaa muhimu, zile ambazo *sensitive* vinazogusa maisha ya watu moja kwa moja. Humu nimeangalia bei za chakula na bei za mafuta ya petroli.

Mhe. Naibu Spika, wananchi wetu wamekuwa wakinung'unika sana, tulifika pahali kwa kweli walikuwa wamevunjwa moyo sana na bei za chakula. Ingawa baada ya serikali kujieleza vizuri

hatimaye wananchi walifahamu nini kilichotokea mpaka bei zikawa katika mripuko wa namna ile.

Pamoja na hayo Mhe. Naibu Spika, bado tunatatizo la wafanyabiashara wetu. Hili mara nyengine mimi nathubutu kusema wafanyabiashara wetu hawana imani na wananchi. Kwa sababu mara nyengine unatokea mripuko wa bei, wakiangalia tu kwenye mtandao wanaona bei zimebadilika kule duniani lakini wao kwenye magodauni yao kumejaa bidhaa ambazo hazihusiki na bei ile kule duniani, lakini chakula kinapandishwa bei ndani ya magodauni wakati kimeshaingizwa nchini, kimeshalipiwa ushuru na kila kitu. Huu kwa kweli ni uhalifu. Nilikuwa nafikiri sana Mhe. Waziri moja katika changamoto alizonao ni hiyo.

Mhe. Naibu Spika, nimeona kuna kanuni hapa ya 6 mambo ya uagiziaji inahusu muundo wa bei. Kanuni hii imempa fursa Mhe. Waziri kwa kushirikiana na hao waagiziaji kuangalia miundo ya bei kulingana na mabadiliko ya dola, mabadiliko ya pesa zetu katika nchi, mabadiliko ya bei katika soko la dunia. Lakini nilikuwa namuomba sana Mhe. Waziri awe *serious* katika hili. Kwa sababu wafanyabiashara wengini ni wanyambi.

Pia jambo jengine ambalo na mimi nathubutu kusema wafanyabiashara wetu wengine nafikiri wana kibri. Kwa sababu lilipotokea sakata la bei nakumbuka Mhe. Waziri aliwahi kutoa maelezo ya kubhibiti bei. Mitaani kukawa kumezagaa maneno ya kwamba wafanyabiashara kwa sababu wanajaribu kudhibitiwa kibei basi wanajaribu kuzuia uagiziaji waone kama wananchi watafika wapi, mpaka ukawa mtafaruku mkubwa. Wengine tukawa na wasi wasi kwamba Zanzibar mchele utaadimika kwa sababu wafanyabiashara wameambiwa wauze bei wasiyotaka na wao watajizuia kuleta mchele. Hii inatokana na ile *monopoly* iliyopo ya kuwa muagiziaji mchele ni fulani na fulani tu.

Nilikuwa naomba sana, kama hiyo ni kweli maanaake mimi sina uhakika nayo. Kama hiyo ni kweli waliopewa kibali ni watu fulani tu katika nchi hii, hiyo naomba sana iondolewe. Kila mtu mwenye uwezo wa kuagiza mchele aagize mchele.

Jambo jengine ambalo lipo ambalo pia linafanya niseme kwamba wafanyabiashara hawana imani na wananchi wana ile falsafa ya kuwa nakioze. Wakishaamua tunauza bei hii wakitaka watanunua bei ndio hii, hawataki bei ni hii, hakuna kupunguza bei. Tena hata ukenda wapi utakuta bei ndio hiyo hiyo. Ule ushindani wa kuwashindania soko katika nchi yetu hakuna. Maana yake mfanyabiashara mzuri ni yule ambaye kuwa anaangalia mwenzangu anauza bei gani? Anauza Shs 25,000/- kwa dumu la mafuta ya kupikia, hebu acha na mimi niuze Shs. 24,000/-.

Mhe. Naibu Spika, mimi nina mfano mzuri sana. Yuko mfanyabiashara mmoja chipukizi aliyekuwa hayumo. katika ile *hierarchy* aliagiza mafuta ya kula, akaleta nchini. Kwa kuwa yeye ni masikini ya Mungu anataka auze haraka arudi akachukue mengine, akashusha bei kidogo, aliposhusha bei wakubwa wakajiuliza alah! Mbona leo kutwa hawajaja watu hapa. Aaaa kumbe ni fulani haya ngojea. Wakamtia adabu, kwa sababu wao hawafilisiki, walishusha bei mara kumi ya ile aliyeshusha yeye. Sasa akawa hakuuza, mwisho alikwenda kuwapigia magoti jamani nisameheni. Akaambiwa basi ukome siku ya pili.

Sasa katika hali kama hiyo Mhe. Naibu Spika, mimi nafikiri si nzuri. Nilikuwa naomba sasa hii kanuni ya bei basi Mhe. Waziri aifanyie kazi vizuri. Hapa nataka niunganishe jambo jengine. Hizi kanuni Mhe. Waziri zisimalizie kwenye bidhaa za chakula tu. Kwa sababu huu utaratibu wa wafanyabiashara kutupandishia bei mimi nafikiri hata Uislamu unaweka asilimia fulani ya faida. Kama kalamu hii nimeinunua Sh. 5/- huko ilikoundwa basi mimi siruhusiwi kutoa faida 100% ya ile Sh. 5/- nikaiyuza Sh. 10/-.

Mhe. Naibu Spika, sikumoja nilikuwa nimekaa dukani mfanyabiashara mmoja anayejua mambo ya watu ikawa simu yake imepata ajali imeharibika. Akamtuma kijana wake nenda kanunulie simu ya aina hii dukani. Sasa kwa sababu yeye bei anaijua huko inapoundwa alikokwenda kununua yule mwenzake anaijua ile bei na bei aliyoletewa pale kuwa nimeinunua kiasi fulani alishangaa sana hiii! Hivi ndivyo wanavyofanya hawa, yani mtu anatia faida bila ya huruma.

Mhe. Waziri kama sheria itaruhusu mimi nilikuwa nadhani tunapoangalia bei ya vyakula katika soko la dunia, tusiangalie bidhaa hizi muhimu petroli na chakula tu lakini tuangalie na bidhaa nyengine. Kwa sababu watu wetu ni wanyonge mno. Huwezi kuamini bei utakayopewa Zanzibar ukenda pale Dar-es-Salaamu tofauti, sikwambii ukenda sehemu nyengine. Sasa lazima tuone huruma, wao wanaendesha maisha yao kupitia migongo ya wanyonge hawa. Unaweka bei mpaka maana yake mtu anajilazimisha na hapa pengine atajilazimisha atakwenda hapo hapo, kama hatujamuonea huruma sisi tutamuuwa. Kwa hivyo nilikuwa naomba sana juu ya hili.

Mhe. Naibu Spika, hivi majuzi serikali ya Tanzania ilikuwa inatangaza punguzo la bei ya petroli, mimi nikadhania nikifika sheli leo kwa kuwa bei itakuwa imepungua maana ilikuwe pale penye 2,000 kwa lita. Lakini nilipofika Sheli badala ya kupungua imeongezeka, nikauziwa lita moja Shs. 255/- na mpaka leo ndivyo inavyouzwa. Tena kinyemela maana yake hiyo wala haikutangazwa Zanzibar. Nilikuwa naomba sana Mhe. Waziri mambo haya ayafuatilie. Kwa sababu petroli ni moja katika bidhaa muhimu ambazo zinagusa maisha ya watu sana. Kuna ujanja hapa wa kupandishwa bei kinyemela nyemela sijui kwa sababu gani. Nilikuwa naomba hayo yashughulikiwe.

Mhe. Naibu Spika, nataka niipongeze sana serikali kwa kupandisha bei ya karafuu. Karafuu ni uti wa mgongo wa uchumi,

tena sio wa serikali tu, ni uti wa mgongo wa uchumi mpaka wa wananchi mmoja mmoja. Kule kwetu Pemba mtu akiwa na harusi yake anasubiri msimu wa karafuu, akiwa na shughuli yake ya kujenga nyumba, kile kitu ambacho kina gharama kubwa kidogo basi anasubiri msimu huu. Sasa hapo kati kati tulikuwa tukisema sisi ni afadhali mtu apande shamba la mibungo kuliko la mikarafuu. Lakini kwa bei ile ya juzi kwa kweli nataka niipongeze sana serikali kwa kufanya vile. Sasa hakuna sababu ya kuuza karafuu magendo. Naunga mkono sana, mimi binafsi nitakuwa askari mzuri sana wa kuhakikisha kila penye harufu ya mtu anayenunua karafuu za magendo basi tunamshughulikia ipasavyo.

Lakini kuna jambo moja Mhe. Waziri kalisahau, kapanga bei ya tajiri tu atakavyouza karafuu. Sisi kule Pemba anayechumisha mikarafuu akauza tunamwita tajiri. Lakini tajiri anakuwa ana vibarua wake wanaemchumia zile karafuu kutoka kule kwenye miti na wale ni watu muhimu kweli kweli. Ni watu wambao mara nyengine wanapata hasara kubwa, wanaanguka, wanavunjika wengine wanakufa na wengine wanakuwa walemavu. Hatukusikia bei ya pishi moja ya karafuu kuchumi ni shilingi ngapi. Sasa mimi nipo hapa nimepigiwa simu mbona bwana kibarua hajatajwa. Kwa hivyo naomba sana Mhe. Waziri na hili atafute namna ya kulitolea tamko.

Halafu Mhe. Naibu Spika, mimi nasikitishwa sana na wale wenzetu waliopwa heka tatu tatu za mikarafuu, hawakuilimia ile mikarafuu sasa imekufa. Ukenda kule Pemba maeneo makubwa utakuta kuna pori, ukiuliza unaambiwa hii ilikuwa heka ya fulani bwana, wameziwacha sijui kwa sababu wamepewa bure. Lakini kwa kweli hawakuwa wakiyatunza yale mashamba na sasa hivi mikarafuu mingi imepotea imebakia pori.

Mhe. Naibu Spika, jambo jengine sijui litakuwa la mwisho kutokana na wakati au vipi. naomba nizungumzie kidogo ukanda

wa Mashariki wa kisiwa cha Pemba. Mhe. Naibu Spika, ule ukanda sasa hivi mvua zimepungua mno, hata ikifika kule huwanda ikawa mwaka mvima tunapata msimu wa mvua za mwaka mara moja tu. Kwa sababu hiyo wananchi wamejiajiri katika masuala ya chumvi. Wengi wao wametengeneza maeneo ya kutengeneza chumvi, kuanzia kusini ya kisiwa cha Pemba Chambani, Pujini, Vitongoji, mpaka utafika Kojani, ukanda ule wote, Kangagani huko kwa Mhe. Hamadi Masoud, kote kuna mashamba ya chumvi megi na wananchi wanavuna chumvi sana.

Kinachosikitisha serikali inaonekana haijatoa umuhimu wa kuwasaidia wale wakulima wa chumbi. Kwa sababu chumvi yao mara nyengine inakuwa haifikii kiwango. Ili chumvi ifikie kiwango wataalamu wanasema mpaka kuwe na kiwanda cha. kufanyia *process* na kuchanganya madini fulani ndio ifike kiwango kinachotakiwa kuuzwa. mimi nafikiri kuna haja ya serikali katika hili suala la kutilia maanani viwanda. Wajenge kiwanda kimoja kizuri kule Pemba ili ile chumvi wanayoivuna iwe inapelekwa kule, wale wakulima wawe wanauza pale kiwandani, halafu kiwanda kiwe kina *process*, kinaifanya iwe katika *standard* halafu wawe wanasafirisha nje.

Sasa kwa vile walivyo inakuwa hawapati bidhaa nzuri, mara nyengine chumvi yao inakosa soko kabisa. Kwa hivyo, nilikuwa naomba sana Mhe. Naibu Spika, Mhe. Waziri aangalie uwezekano wa kutayarisha kiwanda kizuri sana cha chumvi kule Pemba hasa ukanda wa Mashariki ili kuwasaidia wenzetu ambao sasa hivi wanajiajiri sana sasa hivi.\

Baada ya kusema hayo Mhe. Naibu Spika, kwa sababu wakati ni mfupi sana mimi naunga mkono hoja mia kwa mia.

Mhe. Panya Ali Abdalla: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika. Nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu, kutujaalia jioni hii tukawa katika Baraza lako hili tukufu tukiwa katika hali ya uzima

na afya. Lakini pia nichukue fursa hii kukushukuru wewe kwa kunipatia nafasi hii na mimi niweze kutoa mchango angalau mdogo katika kuichangia bajeti hii.

Tatu namshukuru sana waziri na nampongeza sana yeye na Naibu Waziri kwa juhudi zao kubwa pamoja na watendaji wao wote ambao wametuandalia kitabu hiki. Kusema kweli hata lile la kuuliza humu unalitafuta kwa tabu, kwa sababu kila swali tayari limeshajibiwa kabisa. Lakini tutajitahidi hivyo hivyo angalau tuweze kupata japo mawili matatu tuweze kuichangia bajeti hii.

Mhe. Naibu Spika, nianze ukurasa wa 17 penye maendeleo ya viwanda. Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kweli ilianzisha viwanda ikiwa ina lengo zuri la kuweza kuwapatia fursa wananchi wake kwa ajili ya kupata ajira. Lakini pia kuweza kupunguza uagiziaji kutoka nje. Tatu kuiingizia serikali mapato ili kuweza kuendesha nchi vizuri.

Mhe. Naibu Spika, katika uwanjishwaji wa viwanda huu, inaonekana tulishindwa na viwanda vingi vikafa na hatimaye tukakumbana na wimbi zito la ajira na mpaka hivi sasa bado tunasumbuka na vijana wetu kwa ajiri ya ajira. Lakini tulianza kupata matumaini mazuri baada ya kusikia kiwanda cha Sukari kimepata muwekezaji. Hili lilileta faraja kwa wananchi na kuona tayari tutakwamukwa kiuchumi ili tuweze kupata ajira na kujiendeleza na familia zetu.

Kwa masikitiko makubwa bado kiwanda hiki hakijawa mkombozi kwa wananchi wa Zanzibar. Bado muwekezaji aliyewekeza pale hajaweza kukidhi mahitaji yetu. Maana ni muda mrefu tangu amewekeza pale lakini hatuoni kinachoendelea. Ile ajira bado ni usumbufu, hao walioajiriwa bado na wao wapo katika mashaka makubwa ya kuadhibika juu ya pesa zao wanazozifanyia kazi.

Mhe. Naibu Spika, pale tuna hasara mbili kwa mpigo. Hasara ya mwanzo ni kukosa ile ajira ambayo ilikuwa serikali ndio lengo lake kuu kuweza kuwakomboa wananchi wake. Lakini pia hasara ya pili tunaipata muwekezaji huyu mabonde yale sisi wananchi wa Mkoa wa Kaskazini tulikuwa tukiyatumia sana kwa kilimo. Lakini hasara zimekwua mbili kwa wakati mmoja, imekuwa kulima hatulimi na wala sukari hatusagi.

Mhe. Naibu Spika, mimi nimuombe Mhe. Waziri takapokuja hapa pamoja na kuwa ametueleza humu lakini nilitaka kupata nyongeza ya kuona ni lini tunaweza tukapata majibu mazuri au tukaweza tukapata ukombozi mzuri wa kuona Kiwanda cha Sukari kinafanya kazi ili wananchi wapate tija au kiwanda cha Sukari kinafungwa ili tuweke *irrigation* pale tuweze kupata mpunga tukala na familia zetu.

Mhe. Naibu Spika, nadhani muwekezaji anapokuja kuwekeza huwa kunamikataba. Mimi hapa ninachoshangaa muwekezaji huyu, hivi mkataba mimi si mtaalamu wa kujua mambo ya mikataba lakini najua lazina kunaweza kukawa na masharti yoyote kati ya muwekezaji na serikali. Ni lazima kutakuwa kuna mkataba na vipengele vinavyomtaka muwekezaji huyu akishindwa kuwekeza basi takuwa ni lazima wamekatibiana kitu chochote. Ninachoshangaa hapa mpaka hii leo Kamati ndio hizi zinaundwa lakini jawabu ya kututosheleza sisi bado hatujaipata. Kwa hivyo Mhe. Waziri atakapokuja atueleze huu mkataba kweli unaweza kukidhi mahitaji yetu sisi na tukaendelea kuwa na muwekezaji huyu.

Mhe. Naibu Spika, nikiondoka hapo niende kwenye ukuzaji wa masoko. Mhe. Naibu Spika, Mhe. Waziri amejitahidi hapa kutaka kutonesha juhudi zake za kutaka kukuza masoko yetu haya ili wafanyabiashara wetu waweze kufanya biashara vizuri na kupata sehemu za kuziuza. Nampongeza kwa hilo lakini nataka nimuombe sana Mhe. Waziri juu ya hili maana hiki ndio kilio

chetu kikubwa wafanyakazi wetu, wajasiri amali wetu, wafanyabiashara ndogo ndogo hiki ndio kilio chetu cha kuwa biashara zinafanywa lakini bado hatuna soko la kuweza kutukidhia mahitaji yetu.

Mhe. Naibu Spika, wajasiri amali wanajitahidi kufanya biashara, wapo wanavikundi wanawake wanaosuka mikoba, lakini bado utakuta mikoba hii bado hawana sehemu ya kuviuza au kuweza kupata mtu madhubuti wa kuweza kusimamia soko lao kwa sababu tukipata umadhubuti hapa wa kusimamiwa soko hili, basi mikopa hii na vikapu tunaweza tukaviuza. Kwa sababu nakumbuka serikali imepiga marufuku mifuko ya pastiki hivyo tutakapochukua juhudi kudhibiti mifuko ile kweli isitumike, basi kina mama hawa wanaweza wakapata ajira ya kutosha wakaweza kuuza mikoba yao na vikapu na hapo hapo tukaweza kuutunza mji wetu katika mazingira mazuri.

Mhe. Naibu Spika, ndani ya Mkoa wangu kuna kina mama ambao wanajishughulisha sana na biashara ya kutanda dagaa, kina mama hawa kusema kweli wanajitahidi hasa katika kufanya biashara na kuziendeleza familia zao. Lakini tatizo kubwa linawapata kufanya biashara yao hii wakati wa mvua, biashara inakuwa ni ngumu kwa hiyo haya maelekezo yako uliyotoa kusema kweli kitabu kimeeleza lakini haya maelekezo mimi nataka niyape nguvu ili Mhe. Waziri uweze kuyasimamia kuhakikisha kina mama wale wanapata vifaa vile vya kukaushia dagaa wakati mvua zinapokuwa nyingi waweze kujikwamua na tatizo hili.

Mhe. Naibu Spika, baada ya kusema hayo niende katika upandaji wa bei ya karafuu ambapo hapa karafuu kama tunavyoelewa ndio uti wetu mkubwa wa mgongo wa nchi yetu kwa sasa umesaidiwa kidogo na utalii, lakini hapo mwanzo hili lilikuwa ndio zao letu kubwa ambalo tunajivunia. Hapa Mhe. Naibu Spika, niruhusu nimpongeze kwa dhati Mhe. Rais Dk. Ali Mohammed Shein ambaye katika ziara zake tumekuwa tukimsikia kwa juhudi zake

kubwa ambazo alikuwa akituahidi kuhakikisha zao hili atalipandisha bei ili wananchi wa visiwa hivi waweze kufaidika. Na si hilo tu Mhe. Naibu Spika, Mhe. Rais hata mishahara alipokuwa akifanya ziara yake alisema atahakikisha wananchi wa nchi hii basi viwango vya mishahara vinapanda hatua kwa hatua ili tuweze kufikia malengo.

Mhe. Naibu Spika, zao la karafuu limepanda na tunashukuru na tunaipongeza sana wizara hii kwa kazi nzuri, lakini nimuombe Mhe. Waziri karafuu imepanda bei lakini nyuma tuna watu ambao wana rudisha nyuma sana vitendo vya serikali. Tuna watu kwanza ni wezi ambao watataka kuliandama zao hili kwa kuona limepanda bei, watataka kuiba karafuu hizi pia wezi hao wapo wa aina mbili. Kuna wezi ambao wataona waziondoshe karafuu hizi ambazo sisi ndio tunazitegemea na zitatuinua sana kiuchumi waende wakaziuze katika nchi nyengine kwa kutumia njia ya magendo na kupunguza maendeleo katika nchi yetu. Kwa hivyo, nimuombe Mhe. Waziri juu ya hili amejipanga vipi kukabiliana na watu hawa au adhabu gani watapangiwa watu hawa ambao watakamatwa na karafuu za magendo wakizisafirisha kurejesha nyuma juhudi za serikali ambap serikali imeshajitahidi kupandisha karafuu hizi.

Mhe. Naibu Spika, katika karafuu nakumbuka tulikuwa na vituo mbali mbali ambavyo vinawasaidia wauzaji wa karafuu, lakini kwa sasa inaonekana vituo hivi vingi vimekufa hili nimuombe Mhe. Waziri avikague vituo vya karafuu na pale anapoona masafa yamekuwa mbali basi ni muhimu kuweka kituo ili kuzuia mianya ya wale watu ambao watapita mle kufuatilia na kuzinunua karafuu zetu katika njia ya magendo.

Mhe. Naibu Spika, vituo vimekuwa mbali mbali, mimi niseme nilipokuwepo Pemba tulipokuwa katika Mkoa wa Kaskazini tuliwahi kukifufua kituo kimoja kuna sehemu inaitwa Ng'omeni, kituo hiki tulikisimamia sisi kwa kukijenga kwa kuona masafa

makubwa ambayo wanayapata wananchi kwenda kuuza karafuu zao mbali hata wakirudi wameshachoka na ile faida ambayo wametegemea kuipata basi ilikuwa inapungua kwa kiasi kikubwa. Hivyo, serikali ilichukua hatua hiyo ya kukijenga kituo kile cha Ng'omeni sijui mpaka sasa hivi bado kama nacho kipo kama hakipo nimuombe Mhe. Waziri masafa ya kule ni makubwa kituo kile kiwepo.

Mhe. Naibu Spika, hata Mtambwe katika ziara yangu nilipokwenda katika kamati pia tuliweza kuona pale kulikuwa na kituo lakini kwa sasa hakipo. Kwa hivyo, Mhe. Waziri nikuombe hivi vituo vifufue ili wananchi wapunguze kwenda masafa ya mbali kwenda kuuza karafuu.

Mhe. Naibu Spika, mimi leo hapa niseme sina mchango mkubwa kwa sababu kitabu chako kama nilivyoeleza mwanzo, kitabu hiki tunasubiri mambo mazuri kwa sababu kitabu umekiandaa vizuri badala ya maswali kimeleta na majibu yake. Kwa hivyo, mimi nikushukuru na niwapongeze sana na nawatakia kila la heri ili bajeti hii iweze kupita kwa vizuri na muweze kutekeleza yale majukumu yote ambayo mmejipangia ambayo yatakuwa ni ufanisi kwa wizara, lakini ufanisi mkubwa utakuwa kwa wananchi wanaoitegemea serikali yao hii kuona wanapata mafanikio. Mhe Naibu Spika, baada ya kusema hayo mimi kwa niaba yangu na kwa niaba ya wanawake wa Mkoa wa Kaskazini naunga mkono hotuba hii kwa asilimia mia moja.

Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi: Ahsante Mhe. Naibu Spika, kunipa nafasi hii na mimi kuchangia hotuba hii ya Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko. Kwanza Mhe. Naibu Spika, nampongeza Mhe. Waziri kwa kuteuliwa kushika nafasi hii ya Uwaziri wa Biashara na pia nimpongeze Mhe. Naibu Waziri Mhe. Thuwayba kuwa msaidizi wake wa wizara hii.

Mhe. Naibu Spika, lakini pili nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kumpa kauli njema Mhe. Waziri kwa kusikiliza kilio cha wananchi kwa kulipandisha bei zao hili la karafuu. Mhe. Naibu Spika, zao hili ambalo sasa hivi lilikuwa limeshapoteza mwelekeo wake kwa wananchi, wananchi wengi tayari ilikuwa zao wameshalisusa kutokana na bei, lakini na mimi vile vile nawaambia wananchi kupandishwa kwa bei ya zao la karafuu na wao wao wasikilize kilio cha serikali kwamba zao hili na wao waweze kulihifadhi vizuri ili kuacha kulisafirisha kwa magendo kwa kupitia njia zisizohusika.

Mhe. Naibu Spika, kwa kuwa wakulima tuwashukuru sana hivi sasa wamerudisha imani zao kuhusu zao hili, lakini cha kusikitisha Mhe. Naibu Spika, ni kwamba Shirika la *ZSTC* limeshindwa kupanga mikakati ya kuongeza ubora wa zao hili. Mhe. Naibu Spika,l zao hili kwani hadi hii leo bado ukaushaji wake wa karafuu unategemea jua, jambo ambalo Mhe. Naibu Spika, siku nyengine hutokezea mvua na karafuu hizi zikashindwa kukauka na hatimae kugeuka mpeta.

Mhe. Naibu Spika, kwa hiyo basi niombe serikali kutafuta mashine maalum ya ukaushaji wa zao hili ili kupata ubora wa karafuu zetu na kuwa nzuri. Aidha, kwa wakulima hao wa karafuu katika hatua za awali za uvunaji wa zao hili la karafuu hawana uwezo lakini naiomba serikali iwasaidie vitendea kazi kama vile majamvi, kamba pamoja na taa za karabai ili waweze kuliendesha zao hili. Kwa hivyo, naiomba serikali iwakopeshe vifaa hivyo kwa masharti na bei nafuu.

Mhe. Naibu Spika, nije katika zao la minazi. Mhe. Naibu Spika, katika awamu zilizopita kilimo cha minazi tuliambiwa kinaboreshwa kutoka minazi mikubwa na kuja minazi midogo. Kwa maana hiyo kuongeza usafirishaji wa pato la taifa je, mpango ule umefika wapi na je, sasa hivi zao hili halimo katika orodha ya mazao ya biashara kwa hapa Zanzibar. Mhe. Naibu Spika, vile

vile kuhusu zao la mipira ambalo Mhe. Waziri katika kitabu chake hiki hakulitaja kabisa kwa hiyo Mhe. Waziri hakusema lolote kuhusu zao hili. Je, Mhe. Waziri dhamira ya zao hili serikali ni kuendeleza kilimo au halina soko katika ulimwengu huu hili zao la mpira. Mhe. Waziri naomba aje anijuilishe kuhusu hilo.

Mhe. Naibu Spika, nije katika zao la mwani pamoja na kupandishwa zao hili la mwani, lakini bado wapo wakulima wa mwani wanashindwa kulima zao hili kutokana na kutokuwa na vifaa. Mhe. Naibu Spika, namuomba Mhe. Waziri awasaidie wananchi hawa vifaa vya kutendea kazi ili waweze kuzalisha zao hili kwa wingi na kuweza kuliendeleza hapa Zanzibar.

Mhe. Naibu Spika, mwisho nije katika vipodozi ni kwamba Zanzibar takriban watu wote sasa hivi wanatumia madawa ya kujichubua ukiangalia takriban ni watu wengi sasa hivi. Mhe. Naibu Spika, hivi sasa ukiangalia hali ya wa Zanzibar wote sura zao zimebadilika, lakini nimuombe Mhe. Waziri aliangalie sana kwa sababu hawa wanaonunua hivi vipodozi vinaandikwa kwa maandishi ya Kiengereza ambayo wengine hawakusoma hawajui nini wakitumie vipi. Kwa hivyo, hununua dawa zile mtu akajipaka na hatimae akageuka sura ikawa kama alivyosema Khadija Kopa uso wa paka.

Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri aliangalie sana suala hili la uingizaji wa vipodozi kwanza apige vita vipodozi vilivyokwisha muda wake halafu aliangalie sana kwa maandishi yanayoletwa kwa Kiengereza wananchi ambao hawafahamu dawa zile wazitumie vipi. Kwa hivyo, Mhe. Waziri nakuomba hili ulizingatie kwa sana ukiangalia hatimae wa Zanzibar wote tutakuwa na nyuso zilizokuwa na mabaka.

Mhe. Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ahsante.

Mhe. Abdi Mosi Kombo: Ahsante Mhe. Naibu Spika, kwa imani yako kwa kunipa nafasi hii na mimi ya kuchangia hotuba ya Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko. Kwanza namshukuru Mwenyezi Mungu kwa uwezo wake kutufikisha hapa leo na kutufanya tukiwa wazima. Vile vile namshukuru Mhe. Rais wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa mfumo wa Serikali ya Umoja wa Kitaifa.

Mhe. Naibu Spika, mimi nitakwenda kidogo katika maendeleo ya viwanda. Mhe. Naibu Spika, katika ulimwengu mzima inasemekana kwamba maendeleo yanaletwa na viwanda, na sisi Mhe. Waziri wetu katika kitabu chake hiki kinazungumzia viwanda. Kwa hivyo, Zanzibar tulikuwa na viwanda lakini kama vimekufa au vimeuzwa hatujui na kama tunajua basi tumeuza wenyewe, lakini hivi sasa iko haja kutokana na maendeleo ya kiulimwengu kufungua viwanda aidha vipya au kama vile vikuukuu kama vipo basi vifunguliwe.

Mhe. Naibu Spika, katika nchi yetu tuna vijana wengi sana na wananchi wengi sana wana viwanda vidogo vidogo, vilivyokuwa vya binafsi vipo vina wananchi wanaviendesha lakini kutokana na uwezo wao mfupi viwanda vile vinakosa maendeleo. Mhe. Naibu Spika, tukichukua kwa hapa Unguja Mjini kuna sehemu pale Mlandege pale pana wananchi wengi sana wana viwanda. Kwa hivyo, serikali pamoja na wizara wananchi wale kama watawapa huduma na kuwajengea sehemu nzuri yakuweza kujiendesha basi sehemu hiyo inaweza ikatupa msukumo sana kwa viwanda vile vilivyokuwepo pale.

Lakini serikali bado haijawaona vijana wale pale wanatengeneza kila kitu na vitu vile vile tunaviagizia Bara. Kwa hivyo, naiomba serikali pamoja na Wizara hii ya Biashara inayoongozwa na Mhe. Mazrui wale wananchi wale waangaliwe ili waweze kupewa mikopo. Mhe. Naibu Spika, wananchi wale wakipewa mikopo wataendelea vizuri.

Mhe. Naibu Spika, tunakwenda katika sehemu za viwanda vya serikali vikubwa vikubwa, sasa hivi iko haja ya hivi sasa serikali pamoja na wizara hii kutujengea viwanda. Kwa mfano, upande wa Kaskazini hivi sasa kuna wananchi wengi sana wana nyanja za kibiashara lakini hawana msaada wa viwanda. Mhe. Naibu Spika, Kaskazini tunahitaji kiwanda cha madagaa hivi sasa, tunahitaji kiwanda cha samaki, tunahitaji kiwanda cha matunda, tunahitaji kiwanda cha kukaushia mwani. Mhe. Naibu Spika, hivi vitu vyote Kaskazini vipo lakini sasa hakuna msaada unaopelekwa kwa wananchi wale ili wakaweza kujiendesha.

Mhe. Naibu Spika, Kaskazini tunakosa ajira, tunakosa kila kitu na tunakosa utaalamu kwa ukosefu wa viwanda. Mhe. Naibu Spika, Mjini viwanda viko vingi sana, lakini vimeuliwa tu. Mimi nakumbuka viwanda vidogo vidogo pale pana viwanda vyote, pana viwanda vinafika 25 pale lakini bado serikali viwanda vile imevitupa. Mhe. Naibu Spika, pale pana kiwanda cha mananasi, pana kiwanda cha mipira ya baiskeli, pana kiwanda cha kutengenezea nguo. Hivyo kwa nini serikali haivichukui viwanda vile vikafanya huduma na kama kuna watu wameuziwa kwa nini wale watu hawaambiwi wakaleta huduma katika viwanda vile.

Mhe. Naibu Spika, tunamuomba Mhe. Waziri wakati utakapoleta majumuisho uje utueleze viwanda vidogo vidogo vimekufa au vimeuzwa. Viwanda vile ingelikuwa vinafanya kazi wananchi wa Zanzibar wote wangelipata ajira pale, lakini viwanda havipo.

Mhe. Naibu Spika, serikali yetu ya Umoja wa Kitaifa makusudio yake makubwa kuwataka wananchi wake kufanya biashara ili kupata maendeleo, lakini ukosefu wa nyanja za biashara, ukosefu wa huduma za biashara, ukosefu wa mitaji wanakuwa wanaanguka sana. Kwa hivyo, Mhe. Naibu Spika, namuomba Mhe. Waziri awaangalie wafanyabiashara wa Zanzibar kuwapa mikopo ili wapate kujiendeleza.

Mhe. Naibu Spika, kuna kina mama wanawake wanaitwa mama ntilie hao, hivi sasa wanaweza kufanya biashara lakini hawana fedha za kufanyia biashara na wakipata mitaji wafanyabiashara kidogo wakiuza biashara zao pale hasa wale wanaouza wali wanakuja Manispaa wanauchukua ule wali aidha wanakwenda kuumwaga au wanakwenda kugawana. Mhe. Naibu Spika, watu kama wale wameshauza wali, wameshanunua mchele, wameshagharamika lakini bado Manispaa wakifika pale wanawanyanganya. Kwa hivyo, Mhe. Naibu Spika, ikiwa Manispaa wameshaona kwamba hawa wafanyabiashara hawana mazingira mazuri basi wawatafutie sehemu wawajengee pazuri ili wajiendeshe sio kuwanyanganya. Mhe. Naibu Spika, ikiwa tutawanyanganya wafanyabiashara biashara zao huu utawala bora itakuwa hatuna na sisi tunataka utawala bora.

Mhe. Naibu Spika, utawala bora mwananchi unamuwezesha, unamjengea sehemu unamuweka sehemu ile kama inatakiwa na serikali kujengwa basi inachukuliwa inajengwa, lakini mwananchi wako umeshamuwekea mahala pazuri. Lakini mwananchi ameshagharamika biashara yake kwa mfano ndio mfuko wake wote halafu baada ya kuuza anakwenda kunyanganywa hivi itakuwa wananchi tunawanyanyasa. Kwa hivyo, naomba wizara hii iwaangalie wananchi kwa jicho la huruma. Pia naiomba tena serikali isiwanyanganye wananchi biashara zao wakati wanapouza iwatafutie sehemu iwajengee ili wapate kujiendesha sio kuwanyanganya hiyo sio suluhu.

Mhe. Naibu Spika, tunatembea katika nchi za watu tunaona mambo yanavyokwenda, lakini unakwenda danedane pale mtu ameshaweka biashara yake na ndio mfuko wake wote anakwenda Manispaa anamnyanganya. Baada ya kwishakumnyanganya haitambulikani kesi mimi siku moja nilipita nikawakuta wanaambizana akenda kunyanganya yule anarudi anakwenda mwengine mpaka wanamaliza. Kwa hivyo, kama tunataka

wananchi wetu waende vizuri na wawe na maisha mazuri basi tusipende kuwanyanganya biashara zao, kwanza kumnyanganya mtu biashara yake ni dhambi. Mhe. Naibu Spika, utamnyanganya vipi mtu biashara yake wakati wewe ni Muislamu, muelekeze na muwekee nafasi mahala pazuri halafu umtizame yeye atafanya nini.

Mhe. Naibu Spika, hapa pana hali ya chakula na mwenendo wa bei. Mhe. Naibu Spika, sasa hivi tunanunua vyakula kwa bei ya juu kabisa na sababu yake hatujui kweli ulimwenguni bei imezidi, lakini na ushuru wanaolipa wafanyabiashara unazidisha bei kuwa juu. Mhe. Naibu Spika, tunasikia wafanyabiashara makontena yao yakiwa Dar es Salaam wanalipa, wakija Unguja wanalipa sasa inakuwa ushukuru unazidi. Kwa hivyo, mfanyabiashara huyu huyu analipa ushuru mara mbili. Kwa hivyo, Mhe. Naibu Spika, namuomba Mhe. Waziri hili aliangalie kwa makini sana, ushuru mara mbili ndio inazidisha kuuzwa biashara ghali katika nchi yetu ya Zanzibar.

Mhe. Naibu Spika, ili nisipoteze muda wako mimi naomba kwamba kama nilivyozungumza kuwa Mkoa wetu wa Kaskazini tunahitaji tupatiwe viwanda hivyo nilivyovitaja na vitaja tena ili Mhe. Waziri avitambue, Kaskazini tunahitaji kiwanda cha kukaushia madagaa, tunahitaji kiwanda cha kusarifia mwani, tunahitaji kiwanda cha samaki, samaki ni wengi sana lakini hatujui tuwafanye vipi. Kwa hivyo, kama tutapata kiwanda cha samaki Kaskazini watoto wetu watapa ajira nzuri na maendeleo yatakuwa mazuri, na hata yale matatizo makubwa ya watoto wetu kuja Mjini wakaa bure yatapungua. Kwa hivyo, serikali tunaiomba viwanda pia Kaskazini hivi sasa inalima matunda mengi sana, inalima ndimu sana, embe nyingi sana kwa hiyo tunahitaji kiwanda cha matunda kiletwe Kaskazini.

Mhe. Naibu Spika, kwa kuheshimu muda wako mimi pamoja na wananchi wangu wa Jimbo la Matemwe kama tutaletewa viwanda hivyo basi naunga mkono hotuba hii mia kwa mia.

Mhe. Suleiman Hemed Khamis: Mhe. Naibu Spika, nakushukuru na mimi kwa kunipatia nafasi ya kuweza kuchangia katika hotuba ya Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko. Mhe. Naibu Spika, mimi nataka niseme kwamba tunahitaji kuimarisha biashara zetu, ni lazima biashara kwa wakati tulionao kwa sababu Zanzibar tumejielekeza sana katika suala la biashara. Kwa hivyo, ni lazima hatuna budi tuimarishe biashara zetu kwa hivyo namwambia Mhe. Waziri biashara tunazihitaji kuimarishwa zaidi kuliko hivi sasa. Bidhaa zetu ambazo tunazileta katika nchi hii tuhakikishe kwamba ni bidhaa zenye viwango vizuri.

Jengine ambalo Mhe. Waziri nataka nimwambie ni kwamba tunahitaji tupate usimamizi mzuri wa bidhaa zetu ambazo tunaziingiza katika maduka yetu. Nataka nimwambie Mhe. Waziri katika bidhaa za biashara tulizonazo hapa za vyakula na vitu vyengine ni kwamba biashara zetu nyingi zilizomo madukani zinapita muda ambao wakati wake sio mzuri, (*expire*). Bidhaa zinamalizika zimo madukani na hii Mhe. Waziri nataka nimwambie kwamba, kama ikiwa bidhaa hizi ambazo zina muda maalum zinakaa ndani ya maduka bila ya kupitiwa wakati ambao unaotakiwa, uwezekano wa watu wetu kupata maradhi uko karibu sana.

Kwa hivyo, ningelimuomba Mhe. Waziri asiachilie vyakula vya makopo na vyakula vyengine ambavyo kwenye maduka vinaachwa kwa muda mrefu bila ya kupitiwa. Nchi imejaa maradhi ya namna kwa namna, kwa hivyo tujitahidi sana Mhe. Waziri kuhakikisha kuwa vyakula vinapitiwa na vinaangaliwa kwa vizuri.

Mhe. Naibu Spika, katika kuinua kiwango chetu cha kibiashara ndani yake tukiinua tunapata kipato sisi wenyewe na tunaongeza pato la taifa. Kwa hivyo, ni muhimu tuhakikishe kwamba tunainua biashara zetu kwa kipato cha mtu mmoja mmoja na pato la taifa.

Lakini katika kuangalia mambo mawili ambayo Mhe. Waziri anayo biashara pamoja na viwanda. Mimi ningelimuomba Mhe. Waziri kwamba katika suala la biashara na suala la viwanda aweze kushirikiana na Mhe. Waziri wa Mifugo na Uvuvi. Kwa sababu naamini bila ya kufanya mashirikiano mazuri basi viwanda kwa upande wa bahari vitakosekana ni lazima yapatikane mashirikiano mawili.

Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko na Waziri wa Mifugo na Uvuvi washirikiane kwa sababu hapa tunahitaji tuwe na viwanda vya kusindikia samaki, sasa tunataka kunyanyua hali za wananchi wetu. Bahari inayo rasilimali nyingi sana za uvuvi, inaweza kututoa katika hali mbaya za kimaisha na tunazo aina zote za samaki kwa hivyo tunaweza kusindika samaki kwa wingi na hawa samaki tutakaopata tutaweza kuuza nje, tukiuza nje tutapata fedha za kigeni, tukipata fedha za kigeni fedha hizi zitaweza kutusaidia kununua mahitaji yetu ndani ya nchi.

Kwa hivyo, hapa ningelimuomba Mhe. Waziri akashirikiana na Mhe. Waziri wa Uvuvi ili tukapata hivi viwanda kwa haraka na kuweza kusindika na sisi wananchi wetu wakafaidika.

Mhe. Naibu Spika, pia nataka nizungumzie juu ya suala la matunda. Nchi yetu ina matunda ya kutosha, matunda mengi sana tuliyonayo ndani ya nchi yetu na inafika wakati matunda haya yanaharibika. Kwa hivyo, ningelimuomba Mhe. Waziri tunayo nafasi ya kuweka viwanda vya ziada katika nchi yetu, lakini katika hivi viwanda tunabaini kitu kimoja, viwanda vidogo vidogo

tunavyo vingi ndani ya Zanzibar, lakini hali ya kiwango katika viwanda vyetu havijafikia.

Halafu matunda kama ni matunda hatujafikia matunda yetu ya kupea, kwa sababu Unguja tuna tabia ya kitu kimoja, matunda tunapiga moto, tunauza marikiti ndizi za moto na matunda mengine yanapigwa moto. Sasa kama tunataka kusafirisha nje hali hii tuliyoizowea haitoweza kufaa, kuchuma matunda yaliyokuwa machanga hayajapea hatuwezi kufanya biashara ya namna hiyo, kama tunataka kujikita ndani ya biashara ya matunda ni lazika wakulima wetu wajikite katika kuhakikisha kwamba matunda yanayovunwa yamepea, yako katika hali ya usafi, *packing* zake ni nzuri na ziko *standard*. Hiyo itaweza kutusaidia. Kwa hivyo, ningemuomba Mhe. Waziri au watu walio chini yake vile vile ajitahidi na kuhakikisha kwamba hali hii inajitokeza kwa vizuri.

Mhe. Naibu Spika, katika nchi yetu vile vile tunavyo viwanda vidogo vidogo kama vya *aluminium industry* tunavyo hapa Zanzibar. Lakini viwanda hivi tunahitaji kupata malighafi, tunahitaji kusarifu bidhaa zetu vizuri, tunahitaji kuwa na *quality* nzuri ya bidhaa zetu na tunahitaji soko la kuuzia bidhaa zetu. Sasa ningelimuomba Mhe. Waziri katika jitihada zake zote hapa tunavyo viwanda hivyo, lakini bado watu hao wanahitaji kupitiwa na kuangaliwa kwa sababu ndani yake wana mapungufu makubwa sana. Kwa hivyo, kuweka hali hii ya kupata malighafi, kusarifu bidhaa zao na hali ya bidhaa zikawa nzuri na kupata soko ni jambo muhimu na hilo serikali inahitaji kutilia mkono.

Wafanyabiashara hao jambo jengine ambalo ninaliomba ni kwamba hali za watu wetu wamekuwa duni sana katika biashara na biashara zetu za viwanda zinakuwa chini kwa sababu uwezo wetu wa kuzalisha ni mdogo hatujafikia kiwango kikubwa sana cha uzalishaji kwa sababu uwezo wetu ni mdogo. Kwa hivyo, ningelimuomba mawili katika hayo asaidie watu hawa, ama kwa kupewa mikopo wakaweza kujiendeleza au ikiwa mikopo

haikupatikana katika wizara hii watafute mabenki wakope ili waweze kujiendeshea biashara zao kwa njia ya benki. Kwa hivyo, tutaweza kukuza kiwango cha uzalishaji na tukifanya hivyo tutaweza kunyanyua hali za wananchi wetu.

Halafu bidhaa hizi tutakazozipata ni muhimu ambapo na sisi tunaweza tukauza nje tukapata pesa za kigeni zikaweza kutusaidia. Ningemuomba Mhe. Waziri kama kutoa ushauri kwa wafanyabiashara waweze kuwekeza ndani. Kwa sababu kuna wafanyabiashara wengi bado wanashindwa kuwekeza. Kwa hivyo, waweze kuwekeza katika viwanda ili hao wawekezaji wa ndani.

Vile vile Mhe. Waziri tumuombe aweze kututafutia watu wengine ambao wanaweza kuja kuwekeza wanaotoka nje. Kwa hivyo, tuwe nao wawekezaji wa ndani na wa nje katika kusaidia viwanda vyetu. Tukiwa na viwanda vingi bila shaka vijana wetu wataweza kupata ajira, hicho ni kitu muhimu kuwasaidia vijana wetu.

Pia niweze kupongeza Mhe. Waziri kwa kujitayarisha na sera za viwanda ambapo safari hii tumepata sera mpya za viwanda kwa sababu sera zimeonekana kuwa ni kongwe, kwa hivyo, nampongeza kwa suala hilo. Lakini vile vile namuomba katika *master plan* ya visiwa hivikuna kitu ambacho hakijaweza kuonekana, nchi bado *master plan* yake haijajulikana ndio maana tunajenga majumba ovyo hakuna utaratibu wa kupitisha magari wakati *incase of fire*, matatizo chungunzima, masuala ya kupeleka magari makubwa kupeleka bidhaa inakuwa ni tatizo kubwa sana.

Lakini kubwa zaidi katika upande wake Mhe. Waziri ni kuwa tunataka tuone *location*, hatujaambiwa kwamba viwanda vya Zanzibar *location* yake itakuwa mahala fulani. Kwa hivyo, ningemuomba Mhe. Waziri ikiwa bado haijafanyika katika *master plan* yake na hii tujue *location* ya viwanda vyetu wapi itakuwa na

Zanzibar inazidi kumezwa kila wakati mambo mengi yanajitokeza.

Mhe. Naibu Spika, nataka vile vile nimwambie Mhe. Waziri kwamba tunao hawa wajasiriamali ambao wanajitahidi sana kubuni mambo mbali mbali kama haya masuala ya madawa ya kienyeji (*herbal*). Tuangalie katika dawa za misuaki unakuta madawa ya siku hizi mengi yanatengenezwa yawe ni *herbal*, yaani ni ya miti vile vile. Kwa hivyo, mimi ningemshauri Mhe. Waziri vijana wetu wamekuwa *very creative*, wana madawa mengi sana, lakini utakuta matatizo wanayo kwamba katika kutayarisha madawa yetu hayo ya kienyeji wana matatizo ya kifedha, viwango vya madawa hayo hayajafikia sawa sawa, matatizo ya kutafuta soko, matatizo ya hata kuuza biashara. Sasa ningelimuomba Mhe. Waziri kwa kuwa anao watendaji wa kutosha waweze kuwafuatilia hawa na kuwasaidia kila namna ili waweze kujisaidia.

Mhe. Naibu Spika, katika suala hili zima tumejiona kwamba katika kufanya masuala haya ili kufikia kiwango bora cha mambo yetu yote ya viwanda vyetu ni kwamba tunakosa wataalamu wa kutosha. Kwa hivyo, elimu inahitajika kidogo katika kusaidiwa saidiwa ili waweze kufikia mahala pazuri kabisa na waweze kupeleka vifaa vyao soko la nje kwa mahitaji madogo madogo na uzalishaji wao huo huo utaweza kuwapa maendeleo mazuri.

Jengine ambalo nataka nimwambie Mhe. Waziri. Kwa kweli ni muda mrefu sasa hivi katika nchi yetu kumekuwa na kilio, kilio hiki ni lazima tukitafutie ufumbuzi. Ni malalamiko sisi ndio tunaopewa malalamiko, mimi nilifikiria baada ya matatizo yaliyojitokeza katika biashara ya chakula mchele, sukari na unga nilifikiri labda serikali itabeba mzigo huu angalau kuwanusuru wananchi. Wananchi bado wanalalamika bei ya mchele na sukari pamoja na matatizo tuliyoambiwa kuwa yametokezea nje. Bei za bidhaa ziko pale pale au zimeendelea zaidi kuwa juu na hili

ningelimwambia Mhe. Waziri angejitahidi, serikali angalau iwaonee huruma imege sehemu ili kuwapunguzia hii bei, bei iko *constant* shilingi 1,200/- ni ile ile ya zamani mpaka leo wananchi bado hawajaona serikali yao imewafanyia nini.

Kwa hivyo, ningemuomba Mhe. Waziri kama itawezekana hili suala walizungumze angalau bei ya mchele na sukari ipunguzwe. Hii bei serikali ibebe kam aitawezekana.

Jambo jengine Mhe. Naibu Spika, ambalo nataka nilizungumze hapa kwamba kuna tabia ya wafanyabiashara, unajua wanapoagizia mali kutoka nje wanaleta ndani ya nchi yetu, mali hii inakaa katika maghala kwa muda mrefu sana, wanaleta mchele kwa wingi, sukari kwa wingi kila kitu kinaletwa hata vifaa vingine vidogo vidogo vinabakia ndani ya maghala kwa muda mrefu. Sasa mara moja utakuta bei zime *shoot* wakati bado ile mali aliayokuja nayo iliyomo ndani ya ghala haijamaliza kama bei iliyopangiwa ni ile wanaanza kutia bei mpya kutokana na mali ile iliyomo ndani ya maghala yao. Hayo yanatendeka utaambiwa dola imepanda juu, lakini hafikirii kwamba bidhaa ile aliichukua wakati gani. Sasa ni utaratibu maalum nafikiri mngeliufanya kuona kwamba bidhaa kongwe ambazo zimeingia muda mrefu ndani ya maduka isiwe ni sababu ya kupandisha bei za bidhaa zile. Kwa hivyo, ningekuomba Mhe. Waziri hilo suala ukaliona na ukalifanyia kazi. Mhe. Waziri hilo nakuachia ili uweze kutusaidia hapo.

Mhe. Naibu Spika, nina suali zima la habari ya karafuu. Kwana namshukuru Mhe. Waziri kwa kuongeza bei ya karafuu, wnanchi wetu wamefurahi lakini ninachotaka kumwambia Mhe. Waziri pamoja na wizara kuwa imejikita katika kuongeza bei ya karafuu, wewe ukifanya hivi na wenzako wanafanya vingine, tunapoona *some set of competition* baina ya sisi serikali na wananchi, sisi tunaongeza bei na wale wanaongeza bei.

Lakini mimi nataka niseme hili suala katika biashara hii ya karafuu hii *ZSTC* inanunua karafuu moja katika kazi yake, lakini kazi nyengine vile vile tunaona katika shirika hili au wizara hii ina kiwanda chake cha kuweza kuzalishia kutokana na zao lile la karafuu ambacho tunazalisha mafuta ya aina kwa aina kama vile ya makonyo, ya karafuu yanatokana katika bidhaa ile ile, majani ya mkarafuu na makonyo yake na karafuu yenyewe yote inazalishwa.

Mbali ya hivyo katika kiwanda chake vile vile kinazalisha mkaratusi, mchaichai, mrehani yote yanatengenezwa mafuta. Lakini sasa Mhe. Waziri suala hili ningelisema mimi wananchi wakapewa motisha zaidi juu ya suala hili, kwamba uzalishaji umekuwa hali yake kidogo iko duni. Kwa sababu mimi nafikiri watu labda hawajaelimishwa nini umuhimu wa makonyo kupatikana, umihimu wa yale majani katika kuzalisha mafuta na mambo mengine. Lakini zaidi mimi naona katika hawa watu wanaokodi mikarafuu, hilo ndio tatizo kubwa sana, anayekodi mikarafuu anakodi kwa maslahi yake yeye haangalii maslahi ya taifa, anapokodi shamba yeye haidhuru hata kama mtu kenda na panga au shoka akaikata ile mikarafuu *so long* yeye anaangalia mahitaji yake yeye kuwa apate fedha nyingi zaidi. *Regardless* kwamba mikarafuu ile itakatwa au itakuwa vipi yeye anaona apate faida zaidi.

Kwa hivyo, Mhe. Waziri kama hali hii ya biashara zetu imekucwa na mmejitahidi kuongeza bei na wao wanaongeza bei, lakini vile vile mikarafuu itakatwa kwa wingi. Hali ya mikarafuu Pemba sasa hivi kwa upande wa Kaskazini ni mbaya, mikarafuu imebakia Kusini. Kwa hivyo, ningekuomba Mhe. Waziri hilo suala.

Suala la mwisho Mhe. Naibu Spika, Mhe. Waziri aangalie zaidi suala la *competition*. Inavyoonekana sasa hivi Kenya wanakuwa wao ndio watu wakubwa sana, wanaonekana wao ndio wazalishaji wa karafuu Zanzibar wakati sio kweli. Kwa hivyo, ningekuomba

Mhe. Waziri ujitahidi katika kurekebisha suala zima la kufanya *branding*, yaani ijulikane kimataifa. Hicho ni kitu cha kwanza ufanye haraka ili tuhakikishe kwamba karafuu zetu zinatoka Zanzibar *not from* Kenya. Kwa sababu sasa hivi karafuu zinatoka Kenya, wao ndio wanaojulikana kuwa karafuu wanazo wao wakati hata mkarafuu hawana. Sasa ningemuomba suala la *branding.*

Suala jengine ningesema Mhe. Waziri hii mikarafuu idhibitiwe vile vile, tujitahidi sana katika kuidhibi katika kukatwa wakati mwengine mikarafuu inakatwa mibichi. Nafikiri hilo ni suala muhimu sana.

Jambo la mwisho kwa sababu muda umemalizika ningemuomba angezungumza kidigo Mhe. Waziri habari ya maonyesho. Mimi ningeomba katika suala la maonyesho tujitahidi kwa sababu tunajua katika suala hili fedha inapatikana kwa wingi wakati huo na biashara mbali mbali zitakuja, *Sunday Market* tufanye ili tuweze kuwakaribisha watu wetu na wao angalau waone nini *Sunday Market* na faida zake na maonesho mengine kwa wananchi wetu. Nafikiri mambo haya yatakuwa ni muhimu ningemuomba Mhe. Waziri ajitahidi kuyaangalia na kuyapigia jicho hasa wakati wa maonesho ya nchi yetu kama nchi nyengine zinavyofanya maonyesho.

Mhe. Naibu Spika, kwa mujibu wa wakati wako kuwa ni mdodo nachukua nafasi hii ya kukushukuru wewe na vile vile kwa niaba ya wananchi wangu naunga mkono hotuba hii kwa silimia mia moja. Ahsante.

Mhe. Mbarouk Wadi Mussa (Mtando): Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, nakushukuru na mimi kunipa nafasi ili niweze kuchangia hotuba hii ya Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko. Mhe. Naibu Spika, nianze kwa kumshukuru Mhe. Waziri pamoja na watendaji wake wote wa wizara yake kwa

kutuwasilishia hotuba hii nzuri yenye mambao matamu kabisa humu. Hotuba hii kwa kweli imekidhi haja kiasi cha wananchi wetu kule wanakotusikiliza.

Mhe. Naibu Spika, nisipoteze muda wako kama unavyotuhimiza twende kwa haraka haraka ili tupate kuchangia wengi. Mimi nina machache sana katika hotuba hii. Nianze ukurasa wa 11 hapa Hali ya Chakula na Mwenendo wa Bei.

Mhe. Naibu Spika, kwa kweli upandaji wa bei za vyakula umekua kwa kasi sana, bei za vyakula hasa vile vinavyotumika kila siku kama alivyovionesha Mhe. Waziri kwenye hotuba yake kuwa ni mchele, sukari, unga na mafuta vinapanda kwa nguvu mno, kiasi kwamba vinapishana kwa kasi mno na kipato cha mwananchi wetu.

Ukiangalia kwa mfano bei za mchele kwenye mwaka 2005/2006 kilo ya mchele ilikuwa kati ya shilingi 450 – 480 lakini leo hii tuko kwenye shilingi 1,200. Ni kiwango kikubwa mno ukilinganisha na kipato cha wananchi wetu. Sasa mimi namuomba sana Mhe. Waziri atakapokuja hapa atupe maelezo ya ziada kabisa katika kuweza kusaidia huu upandaji ovyo wa bei kiasi hiki. Ametoa maelezo kwenye kitabu lakini naona hayajatosheleza, hivyo aje atupe ya ziada kidogo ili tuone mkakati wa wizara yake katika kuhakikisha kwamba tatizo hili linapungua. Nina hakika halitokwisha lakini litapungua lisiwe kwa kasi kiasi hiki.

Mhe. Naibu Spika, katika kitabu chake Mhe. Waziri alitueleza upandaji wa bei hizi, lakini akaseama unga wa ngano haukupanda katika soko la ndani. Sasa mimi najiuliza kwa nini haukupanda? Ingawa katika kitabu chake katoa maelezo kwamba labda kwa sababu Bara wanalima, lakini mimi nimwambie mchele nao unalimwa sehemu nyingi zaidi kuliko hiyo ngano kule Bara. Sasa hizi sababu nyengine mimi nahisi si sahihi.

Lakini nikumbushie hapo nyuma serikali ilikuwa inatoa misamaha kwa wafanyabiashara ili kupunguza ile kasi ya upandaji wa bei hasa katika kipindi hiki tunachokwenda nacho cha Mwezi wa Ramadhani, sasa sijui mara hii kama ipo au vipi. Lakini mimi nilikuwa naitilia shaka misamaha ile sasa Mhe. Waziri atapokuja naomba aje atueleze namna gani atafanya ili angalau kwa mwezi huu wa Ramadhani basi bidhaa hizi zisipande na ikiwezekana ziteremke kidogo ili ziweze kuwapa nafuu wananchi wetu. (*Makofi)*

Mhe. Naibu Spika: Waheshimiwa Wajumbe tunaahirisha kikao kwa muda mpaka umeme utaporejea.

(Saa 12:20 Baraza liliahirishwa kwa muda kutokana na hitilafu ya umeme hadi umeme utaporejea)

(Saa 12:25 Baraza lilirudia)

Mhe. Mbarouk Wadi Mussa: Mhe. Naibu Spika, nizungumzie ukurasa wa 46 Kiwanda cha Sukari ambacho zamani kiliitwa Kiwanda cha Sukari na Manukato na sasa hivi itabidi tukiite Kiwanda cha Sukari na Spiriti. Kwa sababu hapa kwa mujibu wa maelezo yake Mhe. Waziri anatwambia kiwanda hiki kinazalisha spiriti.

Mhe. Naibu Spika, tukiangalia maudhui ya kujenga kiwanda hichi ni kusaidia katika uzalishaji wa upatikanaji wa sukari kwa wingi ili tuweze kujitosheleza sisi wenyewe humu na nyengine kusafirisha. Lakini bahati mbaya kiwanda hichi kina muda mrefu hakijazalisha sukari. Hata katika maelezo yake hapa Mhe. Waziri ameeleza wazi kwamba kiwanda hichi anajua kimekodishwa lakini hakijazalisha sukari. Sasa sijui tumemkodisha kwa niaba ipi kwa sababu kuna tatizo hapa kwenye kiwanda hichi.

Mhe. Naibu Spika, kiwanda hichi kilikuwa kinachukua ajira kubwa sana ya watu katika Mkoa wa Kaskazini. Lakini vile vile kilikuwa kinasaidia sana kwa wananchi waliokuwa maeneo ya jirani kuweza kujisaidia kwenye mashamba yale ya miwa kulima vilimo vyengine. Lakini kumekuwa kuna tatizo kubwa sana baina ya mwekezaji huyu na wananchi.

Mhe. Naibu Spika, kama tunavyojua kiwanda hichi kilikuwa muda mrefu hakijafanya kazi, walipewa wale mashamba wakawa wanajilimia pale wanapata chochote. Mwekezaji kaja kapewa na serikali lakini hazalishi kitu, amewanyang'anya bure yale mashamba ambayo wananchi walikuwa wakijisaidia imekuwa ni ugomvi sasa. Hata katika kitabu hichi Mhe. Waziri ametuandikia humu namna gani walivyotengeneza mpaka kamati za kusuluhisha.

Lakini mimi nafikiri busara iliyokuwepo kwa sababu mwekezaji hatuzalishii ni bora tuwarejeshee mashamba yale wananchi waendelee kulima ili waweze kupata kipato. Maana hii serikali ni ya wananchi na wananchi ndio wale. Mhe. Naibu Spika, kama tunavyojua ardhi yetu ni ndogo sana hapa. Kwa hivyo, Mhe. Waziri atakapokuja kujumuisha atueleze mwekezaji huyu anaisaidia nini nchi yetu kutokana na uwekezaji wake, ni faida gani tunayoipata ili tuweze kuipima baina yake yeye na wale wananchi kuendelea kulima.

Kwa sababu kama yeye hazalishi kitu na tulitegemea azalishe sukari lakini kwa maelezo ya Mhe. Waziri hapa hajazalisha hata nusu tani ya sukari. Sukari inaendelea kupanda bei tu tulitegemea akizalisha yeye labda itashuka tutapata nafuu matokeo yake shilingi 1,800 mpaka shilingi 2,000 sasa hivi kilo ya sukari. Sasa huyu mimi sifikirii kama anatusaidia naona kama kaja kutukandamiza. Namuomba Mhe. Waziri atakapokuja atueleze faida gani tunayoipata. Kama hatupati mimi nashauri na hizo kamati zilizoundwa humu ni vyema tukamuweka pembeni huyu

akatupisha pale tuwape wananchi wetu wafaidike na matunda ya mapinduzi.

Mhe. Naibu Spika, kwa kweli mimi nilikuwa leo sitaki kusema mengi sana lakini nimalizie katika ukurasa wa 51Changamoto za Wizara. Mhe. Naibu Spika, Mhe. Waziri ameonesha changamoto nyingi sana lakini moja ambayo kidogo nimeona na mimi niizungumze ni haya matatizo ya wafanyabiashara wanayokumbana nayo katika bandari ya Dar es Salaam.

Mhe. Naibu Spika, ni kweli wafanyabiashara wetu wanapata matatizo katika bandari ya Dar es Salaam na hata Bagamoyo. Kwanza kuna tatizo la kusumbuliwa tu maadam wewe unateremsha mzigo wako unatoka Zanzibar kunakuwa na usumbufu. Maana leo kama utachukua TV moja tu una nyumba yako au una chumba kule Dar es Salaam unataka mwenyewe ukatazame basi ukifika pale unaambiwa ulipie tena kodi hata kama huku umeinunua dukani.

Mhe. Naibu Spika, hili ni tatizo, sifikirii kama mtu ananunua TV Kariakoo anakwenda nayo Magomeni au Mwananyamala kuna geti njiani anaambiwa huku unakokwenda nje ya Kariakoo sasa lipia. Maana *TRA* ni moja, hili tatizo ni sugu sana, usumbufu huu wa kulipa mara mbili haujaondoka, tumeshausemea sana na tunaendelea kuusemea.

Mhe. Naibu Spika, namuomba sana Mhe. Waziri atakapokuja hapa atueleze mikakati ya wizara yake aliyoipanga kuhakikisha kwamba usumbufu huu haupo tena. Pia ututajie ile siku ambayo mwisho wake utakuwa tarehe hii maana inaonekana bado. Tukiuliza maswali hapa mnatwambia tumeshazungumza sijui imeingizwa kwenye kero za Muungano. Sasa hebu hili mje mtwambie vizuri maana yake haiwezekani. Tunaambiwa *TRA* ni moja hapa umeshalipia unafika kule unalipia tena inakuwaje, mbona vinavyotoka kule vikija huku havilipiwi.

Mhe. Naibu Spika, namuomba Mhe. Waziri atakapokuja atusaidie maelezo ya kina katika suala hili ili turidhike na wananchi wetu waridhike wakienda wasipate huo usumbufu. Si kuridhika kwa maneno pawe na nia ya kweli kwamba hili jambo limeondoka na wale wenzetu wakubali kama kweli hili jambo tuache maana wanafanya kwa makusudi. Haiwezekani kwamba kelele tunazopiga, makubaliano mnayokubaliana, vikao mnavyokaa, lakini huku unamkuta afisa mdogo tu hata habari hana, ukenda pale anakwambia hayo ya wakubwa mimi siyaelewi lipa. Sasa mtu umeshafika pale hiyo TV utairejesha tena huku, kwanza hakubali uondoke nayo urudi anachotaka lazima uilipie, hutaki kuilipia inatiwa ghalani pale mpaka itaanza kuliwa na panya unasamehe mwenyewe.

Sasa Mhe. Naibu Spika, hili lipo tusifichane na halina kificho hili maana linafanywa dhahiri shahiri. Ningemuomba sana Mhe. Waziri atakapokuja aweze kutusaidia katika hili.

Mhe. Naibu Spika, baada ya kusema hayo, mimi sina tatizo na Mhe. Waziri leo namuwekea kwenye asilimia 80, asilimia 20 naiweka kibindoni kidogo atakapokuja kunipa maelezo haya basi mimi nitamrejeshea mwenyewe. Mhe. Naibu Spika, nakushukuru, ahsante sana.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Naibu Spika, nachukua nafasi hii kukushukuru kwa dhati kwa kunipa nafasi jioni hii niweze kutoa mchango wangu kwa ufupi kwa ajili ya kumsaidia Mhe. Waziri na kuwasaidia Wazanzibari wote kwa jumla.

Mhe. Naibu Spika, nimpongeze Mhe. Waziri kwa jinsi alivyotoa hotuba yake nzuri ambayo kwa kweli imeandikika vizuri na iko wazi kabisa.

Mhe. Naibu Spika, hoja yangu ya kwanza ni kwamba nimeona kwenye fungu la bajeti ya Ofisi Kuu Pemba imepanda kutoka milioni 163.4 mwaka jana hadi milioni 238.4 mwaka huu, limeongezeka kwa milioni 74.9.

Mhe. Naibu Spika, haya ni mafanikio mazuri na bila shaka kuna sababu za kuongezeka kwa fungu hili. Kwa hivyo, naomba Mhe. Waziri labda anifahamishe mafanikio haya ya kuongezeka kwa fungu hili yametokana na nini. Najua kuna masuala mengine itakuwa yameongezeka naomba Mhe. Waziri anielimishe kwa nini fungu hili limepanda.

Mhe. Naibu Spika, nimpongeze pia Mhe. Waziri leo mbali na kuja na hotuba yake ya bajeti amekuja na vitabu viwili vya kanuni, kanuni ambazo zinakusudia kusimamia mwendo mzima wa biashara na mtumiaji hapa Zanzibar. Mimi nimpongeze tu Mhe. Waziri na nimkumbushe kwamba Zanzibar tumekuwa si maskini wa kanuni wala sheria, lakini tumekuwa na umaskini wa utekelezaji na usimamizi.

Kwa hivyo, kanuni hizi mbili alizokuja nazo leo nimuombe Mhe.Waziri kwamba zinahitaji kusimamiwa kwa karibu sana, ili malengo na dhamira ya wizara yake yaweze kutekelezeka na Wazanzibari waweze kupata maslahi kama wizara hii ilivyodhamiria kwenye malengo mazima ya usimamizi wa sheria na kanuni kama zilivyotungwa na serikali.

Mhe. Naibu Spika, jengine ni Sekta ya Viwanda. Mhe. Naibu Spika, tulipokuwa tunachangia bajeti kuu tuliona serikali wanajisifia tu kwamba mchango wa viwanda Zanzibar kwa pato la taifa umeongezeka. Lakini ukiangalia viwanda vyenyewe ambavyo vimezungumzwa kwenye bajeti kuu ni viwanda vya *Esonara* na *Chapati* jambo ambalo kwa kweli si viwanda vya kujivunia kadri viwanda ambavyo vipo katika dunia ya leo.

Mhe. Naibu Spika, nadhani Mhe. Waziri sasa kuna haja ya kujipanga na wataalam wake kufufua viwanda vilivyokuwepo Zanzibar ambavyo vilileta mchango mkubwa katika miaka ya 60 na 70 kwa maendeleo ya Wazanzibari.

Mhe. Naibu Spika, tulikuwa na viwanda vingi kama viwanda vya sabuni, viwanda vya mafuta ya nazi na hata viwanda vya kamba kwa maana ya usumba. Leo vyote hivi vimeondoka na leo hii imebakia historia kwa Zanzibar. Mhe. Naibu Spika, nadhani Mhe. Waziri ana kila sababu ya kujipanga na wataalam wake kurejesha uhai wa viwanda vile kwa maendeleo ya Wazanzibari na nchi hii. Kwa sababu hatuna uwezo wa kujenga viwanda vikubwa hapa Zanzibar kutokana na athari za kimazingira. Lakini uwezo wa kujenga viwanda vidogo vidogo na kuviendeleza nadhani upo na serikali iwapo ikikusudia ina uwezo wa kufanya jambo hilo kwa ufanisi mkubwa na kwa maendeleo ya Wazanzibari.

Mhe. Naibu Spika, sambamba na hilo niseme tu kwamba Kiwanda cha Sukari Mahonda kama ambavyo wamezungumza wenzangu Wazanzibari wana hamu ya kujua kwa nini kiwanda kile hakifikii maendeleo. Kwa nini kunakuwa na kigugumizi kwenye kuendelea kwa kiwanda kile na hatujui kuna sababu gani ambazo zinakwaza kwa ajili ya kufikia malengo yaliyokusudiwa.

Mhe. Naibu Spika, kama mwekezaji huyu ameshindwa kufanya kiwanda hichi nadhani sasa ni wakati muafaka kwa serikali kufuta mkataba ule na kurejesha bonde lile kwa wakulima wa Zanzibar walioko Kaskazini “A” kwa ajili ya maendeleo ya kilimo badala ya kumuweka mwekezaji yule asiwe na tija kwa Wazanzibari.

Mhe. Naibu Spika, jengine nizungumzie suala zima la bei ya karafuu. Mhe. Naibu Spika, nimpongeze Mhe. Waziri na serikali kwa jumla kwa kuona haja ya kupandisha bei ya karafuu kutoka shilingi 5,000 hadi shilingi 12,000 kwa kilo, bei ambayo kwa kweli sio tu itaondosha matatizo ya kimaisha lakini itaondosha

vile vile suala zima la wimbi la magendo katika visiwa vyetu vya Unguja na Pemba.

Mhe. Naibu Spika, sambamba na hilo kabla ya kwenda mbele zaidi nimuombe sana Mhe. Waziri kwamba karafuu tu haitoshi kumpandishia tajiri kwa maana ya mmiliki, lakini njia ya busara kabisa ambayo itasaidia suala zima la karafuu ni kumpandishia pia mchumaji wa karafuu kwa maana ya kibarua. Mhe. Naibu Spika, nimuombe Mhe. Waziri atangaze rasmi bei ya mchumaji wa karafuu ni shilingi ngapi kwa kilo ili kuondosha lile tatizo la mgongano wa matajiri na wachumaji wetu. Kwa sababu wachumaji ndio nguvu kazi kubwa, wachumaji ndio wanyonge wengi, wachumaji wanahitaji kusaidiwa kupitia mgongo wake Mhe. Waziri.

Mhe. Naibu Spika, jengine nitoe wito kwamba kutokana na bei iliyopo hivi sasa hakuna sababu tena ya Wazanzibari kuzikimbiza karafuu zetu kwa njia ya magendo. Nadhani kama nimefahamu vizuri Mhe. Waziri siku ile aliahidi kwamba kila bei ya karafuu duniani ikipanda na Waziri atapandisha bei ya karafuu hapa Zanzibar. Kama hivyo ndivyo Mhe. Naibu Spika, basi hakuna haja tena Wazanzibari kuzipeleka karafuu zetu nje kwani zinaendeleza kudumaza uchumi wetu na kuongeza umaskini hapa Zanzibar.

Mhe. Naibu Spika, nimuombe pia Mhe. Waziri kwamba kwa Zanzibar suala la kuokota mpeta kwa watoto wetu ni jambo la kawaida. Wazanzibari watoto wetu wamejenga mazoea ya muda mrefu kwamba karafuu ya kuokota kwa jina la mpeta ni jambo la kawaida na jambo likizoeleka kwa jamii linakuwa kanuni na pia ni sheria. Kwa hivyo, hivi sasa kwa sababu ya upandaji mkubwa wa bei ya karafuu Mhe. Naibu Spika, watoto wetu wadogo ambao ni wanafunzi wa skuli na vyuo vya madrasa watapata tabu sana wakati wanapookota karafuu kwa matajiri.

Mhe. Naibu Spika, nimuombe Mhe. Waziri atoe muongozo kwamba matajiri wangezingatia karafuu zikiwa kwenye miti yao kwa maana ndio mali yao na tuwaachie watoto wetu pale chini waokote ili waweze kuwasaidia wazee wao ambao ni maskini sana wanapata msaada mkubwa kutokana na suala hili la watoto wetu wadogo kuokota mpeta.

Mhe. Naibu Spika, nadhani Mhe. Waziri angetoa muongozo na akawaomba kabisa matajiri wa karafuu kuwaachia watoto wetu kuendelea na utaratibu ule wa kuokota karafuu kwa jina la mpeta.

Mhe. Naibu Spika, sambamba na hilo nina suala ambalo Mhe. Waziri nahitaji anijibu kwa sababu nahitaji ufafanuzi na nahitaji kujua. Mhe. Naibu Spika, dunia ya siku hizi ni kama kijiji hakuna siri itakayokuwepo kati ya bei ya karafuu hapa Zanzibar na duniani kwa jumla. Mhe. Naibu Spika, ililetwa taarifa kwamba Zanzibar tumepata wawekezaji ambao wanakusudia kununua karafuu hapa Zanzibar na wamekuja na *quotation* tatu ambazo ni dola 12,000, dola 11,000 na dola 10,000.

Lakini Mhe. Naibu Spika, zipo taarifa kwamba serikali yetu imeamua kumuuzia mwekezaji huyu kwa dola 8,000 kwa tani na imeachwa ile dola 12,000, 11,000 na 10,000. Mhe. Naibu Spika, naomba kujua kwa nini serikali kama haiundi hivyo ikakubali kuacha *quotation* zile za juu na kuchukua *quotation* ya chini ya dola 8,000 kwa tani, jambo ambalo kama tukichukua ile bei ya juu maana yake kungekuwa na ongezeko kubwa la mapato kwa Zanzibar na bila shaka umaskini ungeendelea kupungua.

Mhe. Naibu Spika, zipo taarifa pia kwamba fedha za malipo haya ya ununuzi wa karafuu tayari zimeanza kuwasilishwa Benki ya Watu wa Zanzibar *(PBZ)*. Mhe. Naibu Spika, kama hivyo ndivyo labda Mhe. Waziri anambie ni nani huyu aliyekuja kununua karafuu zetu kwa bei hii ya dola 8,000 kwa tani na zipo taarifa kwamba yupo tayari kununua hata tani 10,000 kama itawezekana.

Mhe. Naibu Spika, suala langu hilo muhimu sana Mhe. Waziri akinijibu kwa kweli nitakuwa radhi na nitaunga mkono bajeti hii bila ya wasi wasi wowote. Kwani uwazi kwenye uwajibikaji Mhe. Naibu Spika, ndio jambo la msingi.

Mhe. Naibu Spika, suala la mwisho kwa upande wangu ni mfumko wa bei. Mhe. Naibu Spika, serikali imekuwa ikijenga hoja kwamba Zanzibar tumekuwa na mfumko wa bei kutokana na sababu zile za kiulimwengu. Kwa maana ya kwamba kulikuwa na sababu za kimazingira, kulikuwa na sababu za kiuharamia, kulikuwa na sababu za ongezeko la idadi ya watu hasa nchi za Mashariki ya Kati kama China na kwengineko.

Mhe. Naibu Spika, nachukua nafasi hii kumpongeza sana Mhe. Ismail Jussa Ladhu amekuwa ni mtendaji mzuri wa serikali kwa hoja hii. Amefanya ziara Unguja na Pemba kuwaeleza wananchi kwamba mfumko wa bei umesababishwa na athari za kilimwengu. Kwa hivyo, nimpongeze sana Mhe. Jussa amekuwa sio tu mwakilishi lakini amekuwa mtekelezaji mzuri kwa hoja hii ya serikali.

Lakini Mhe. Naibu Spika, katika ukurasa wa 16 Mhe. Waziri amekiri kwamba mbali ya sababu hizo zipo sababu ambazo zinasababishwa na usimamizi mbovu wa serikali, pia mbinu chafu za wafanyabiashara.

Mhe. Naibu Spika, hilo limethibitishwa ndani ya gazeti la Zanzibar Leo la leo ambalo ninalo hapa. Limesema kwamba yupo Mzanzibari mwekezaji ambaye alidhamiria kuleta mchele kwa bei ya chini mno. Lakini alipodhamiria hivyo basi wafanyabiashara wengine wameamua kumtishia maisha yake na wamemtaka aachane na suala hilo.

Mhe. Naibu Spika, kama hivyo ndivyo kwamba kuna mtu mwenye nia nzuri ya kuwasaidia Wazanzibari wenzake wanamtishia maisha yake kwa kweli huo ni ufisadi. Mimi Mhe. Naibu Spika, ningekuwa ndio Waziri basi huyu ningempa kipaumbele, ningesema kwamba huyu ndie anayefaa kuleta biashara ya mchele hapa Zanzibar na wote hawa ambao wanafanya ufisadi wa kutishia ningewanyima leseni za biashara kwa sababu hawafai kufanya biashara hapa kwa maslahi ya Wazanzibari.

Mhe. Naibu Spika, namuomba sana Mhe. Waziri kwamba kuna haja ya kuwatangaza watu hawa wenye nia nzuri ya kuleta bidhaa rahisi kwa ajili ya maslahi ya Wazanzibari wote na kuwaacha kabisa wale ambao wamekusudia kujilimbikizia mali kwa migongo ya wanyonge ambao kwa kweli hawana uwezo na wapo katika hali mbaya.

Mhe. Naibu Spika, baada ya mchango wangu huo na kwa sababu Mhe. Waziri nilimuomba anijibu suala la *quotation* ya karafuu naomba niseme tu kwamba nitaunga mkono hoja hii mia kwa mia baada ya kupata jibu la suala langu kama nilivyouliza. Mhe. Naibu Spika, nakushukuru.

Mhe. Mussa Ali Hassan: Mhe. Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuweza kuchangia bajeti hii ya Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko.

Mhe. Naibu Spika, kwanza sina budi nimshukuru Mwenyezi Mungu kuweza kunipa uwezo wa kuweza kuzungumzia bajeti hii pamoja na kuniwezesha kusimama hapa nikiwa mzima wa afya.

Mhe. Naibu Spika, pia sina budi kumpongeza Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko na Naibu Waziri pamoja na watendaji wake wote. Kwanza nawapongeza kwa mipango mizuri ya biashara ambayo imepangika vizuri pamoja na bajeti yake. Pia

niwapongeze kwa kutoa nafasi kwa wakulima wa biashara ya karafuu kuweza kupandisha bei ya zao hili hadi kufikia kiwango cha kimataifa shilingi 12,000. Tukizingatia kwamba Mhe. Waziri ameweza kushawishi biashara ya karafuu mpaka kufikia lengo la kwamba wananchi wote wamefurahia suala hili la bei ya karafuu.

Mhe. Naibu Spika, naelewa Mhe. Waziri pia anayo nafasi nyengine ya kuchangia kuweza kushusha bei ya vyakula kwa wananchi wakaweza kufurahi kama walivyofurahia wakulima. Kwa hivi sasa biashara ya chakula ni bei juu sana, kwa hivyo wananchi wote badala ya kufurahia tu wakulima walaji nao wanasikitika sana na wanamsubiri Mhe. Waziri ataliamua vipi suala la ushushaji wa bei ya chakula kwa hivi sasa.

Mhe. Naibu Spika, kwa kuwa tumepata bei nzuri ya karafuu bei hii haikuja tu kama ndoto ni wazi tumetoka nje kuweza kutafuta masoko mpaka tukagundua wapi tunaweza tukapata biashara hii bei ya juu. Kwa hivi sasa nampongeza Mhe. Waziri azidi kujifunga pamoja na sisi ma-*backbencher* wa kamati pamoja na wa Baraza hili la Wawakilishi kuweza kutoka nje pamoja nae ili kutafuta bei nyengine za mazao ambayo yanahitajika kupandishwa. Hasa kwa sisi wakulima wa maweni ambao tunategemea zao la pilipili hoho ni zao zuri la kitaifa la kuweza kutafuta bei nchi za nje.

Mhe. Naibu Spika, tukizingatia hivi sasa nchi nyingi za dunia zina vita sana na wanatumia sana mabomu ya moshi wa pilipili. Nafikiri tukiweza kulima pilipili tukapata bei nzuri sana na masoko nchi za nje na kuwapindishia bei wakulima wetu wakaweza kufurahia bei mpya kama ilivyokuwa bei ya karafuu.

Mhe. Naibu Spika, pia namuomba Mhe. Waziri azungumzie zaidi soko la mwani. Hivi sasa mwani uko bei ya chini sana na tunaweza kutoka nje tukatafuta bei ya mwani kuliko bei ambayo

iko sasa kwa kuwa walanguzi wananunua bei ndogo sana hapa nchini. Tunao uwezo wa kwenda nje ambako kuna bei nzuri kama tulivyoipata bei ya karafuu.

Mhe. Naibu Spika, hapo hapo ili wakulima wa aina nyingi wote tuwape moyo tunaomba kwamba bei zote za vyakula ambavyo tunavihitaji kutangazwa au bei za biashara kutangazwa tuzitangaze hadharani. Hivi sasa tunao ukulima mkubwa wa mambo ya mihogo. Tunaweza kulima muhogo na tukaweza kuweka chakula cha akiba katika maghala yetu endapo tutauchonga muhogo na ukawa mkavu. Hivyo, ipo haja ya kutangaza bei nzuri tu ya muhogo wakulima wakaweza kulipa muhogo kwa wingi tukahakikisha na sisi Zanzibar tunajitangaza kwamba tunalo ghala la akiba la chakula likitokea janga wakati wowote.

Mhe. Naibu Spika, mahindi hivi sasa yamekuwa hayakaushwi kama ilivyokuwa zamani, mahindi yote utakuta yanachomwa tu na wenye vigari vya kutembeza. Biashara hii tumeidharau sana wakati ni biashara nzuri ya kuweza kuweka akiba katika maghala yetu na ikasaidia pindi inapotokea njaa nchini. Ndio utakuta wenzetu Tanzania Bara wanatangaza hadharani kwamba tunazo tani fulani za chakula cha akiba, lakini sijasikia Zanzibar kutangaza kama tuna tani ngapi za chakula cha akiba na wakati tunao uwezo mzuri tu wa kuweza kupata chakula tunacholima wenyewe hapa nchini.

Mhe. Naibu Spika, hatuwezi kusema tunaweza kupata akiba ya chakula kwa mfano mapembe, mapembe tunajua huko kwao yamekaa muda gani. Mapembe tunaletewa hapa tayari yameshamaliza miaka 20 hatuwezi kuweka miaka mingine tena akiba. Lakini kama tutaweka mahindi, muhogo mkavu, tutakuwa tuna hakika kwamba muhogo wetu tumelima mwaka huu 2011 tunaweza kufika 2015 ni akiba nzuri tu nchini.

Mhe. Naibu Spika, namshauri Mhe. Waziri aweze kutoa hadharani bei za vyakula ambavyo tunaweza tukaweka akiba katika maghala yetu ili wananchi na wakulima wote kila mmoja akavuta upande wake. Mkulima wa karafuu anavuta upande wake, mkulima wa pilipili hoho anavuta upande wake, mkulima wa mahindi, mihogo, wote itakuwa kila mtu anachakarika kutafuta maisha na tutafikia katika lengo la utajiri Zanzibar kuliko hata hilo tunalosubiri la mafuta. Hivi vyakula vyetu tu tunaweza tukatajirika nchini kwetu kwa fedha za kigeni na tukahakikisha kwamba Zanzibar sasa inajitegemea.

Mhe. Naibu Spika, ni muda mrefu tunategemea nje wakati sisi wenyewe tuna uwezo mzuri wa kujitegemea wenyewe kama hivyo alivyoanza Waziri wa Biashaara, Viwanda na Masoko kulipandisha zao la karafuu. Nina hakika sasa Zanzibar itakuwa na uwezo wa fedha nyingi hapa nchini kwa sababu wananchi wengi hawana sababu tena ya kufanya magendo kutafuta kuhatarisha maisha yao, ni wazi atakwenda mjini kuuza karafuu na kurudi na kipeto cha pesa.

Mhe. Naibu Spika, kwa leo sina mchango mkubwa isipokuwa mimi na wananchi wangu wa Jimbo la Koani tunaunga mkono bajeti hii kwa asilimia mia kwa mia. Ahsante sana.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Naibu Spika, naomba nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu Subhanahu Wataala kwa kutujaalia uhai na uzima alaasiri hii ya leo kwa sababu tunaingia nyakati za usiku tukijadili Wizara hii ya Biashara, Viwanda na Masoko.

Mhe. Naibu Spika, pili, nikushukuru na wewe kwa kunipa nafasi hii. Tatu, nimpongeze sana Mhe. Waziri kwa hotuba yake nzuri kabisa ya bajeti ya Wizara hii ya Biashara, Viwanda na Masoko.

Mhe. Naibu Spika, nitangulize kusema kwamba kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Mji Mkongwe naiunga mkono hotuba hii. Baada ya kusema hayo Mhe. Naibu Spika, na ili uungwaji wangu mkono uende vizuri, naomba Mhe. Waziri anisaidie katika masuala kadhaa niliyokuwa nayo.

Mhe. Naibu Spika, kwanza naomba nianze mchango wangu na kidogo wasi wasi nilioupata katika hiki kitabu cha matakwimu ya mapato na matumizi. Kwanza kabisa Mhe. Naibu Spika, naomba niende katika ukurasa wa 31 wa kitabu hiki ambapo pia kuna maelezo yake ambayo yamefanana na ukurasa wa 64 wa hotuba ya waziri, ambapo amesema mapato ambayo yanategemewa kukusanywa na wizara hii ni milioni 30.

Mhe. Naibu Spika, nilikuwa najiuliza kwamba kwa wizara kama hii ambayo imebeba shughuli nzito za uzalishaji, hivi tunapaswa tutosheke sisi wawakilishi kwamba Sheikh Nassor Ahmed Mazrui na timu yake yote wanaweza kutukusanyia milioni 30 tu kwa mwaka mzima. Nilikuwa naomba suala hili kidogo atusaidie au ndio mapato yote huwa anayakusanya Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo kwamba yeye makusanyo yake hanakuwa yanamalizia kwenye 30 milioni tu. Nilikuwa naomba maelezo.

Hapo hapo Mhe. Naibu Spika, nilikuwa naomba nisaidiwe kwenye matumizi, nimepata wasi wasi kidogo na kupanda kwa kiwango kikubwa, kwa viwango vya mwaka jana na miaka iliopita na mwaka huu, na ili anielewe Mhe. Waziri naomba kutoa mifano.

Kwanza Mhe. Naibu Spika, kwa ujumla wake nikiangalia fungu la matumzi ya Idara ya Mipango Sera na Utafiti. Fungu hili Mhe. Naibu Spika, ili tuweze kulilinganisha vizuri, inabidi tulitizame kwa mwaka jana halafu mwaka huu tuchanganye mipango, sera

na utafiti na utawala na uendeshaji, kwa sababu zilikuja mbili kwa pamoja sasa hivi zimegawanywa.

Mhe. Naibu Spika, nikitizama kwa mwaka jana ilikuwa Idara ya Mipango Sera na Utafiti ni milioni 631,160,000, lakini kwa mwaka huu zikichanganywa mipango, sera na utafiti na utawala na uendeshaji zinakuwa milioni 786,743,000. Hapo pana nyongeza ya takriban zaidi ya milioni 100.

Lakini Idara ya Viwanda vile vile Mhe. Naibu Spika, kwenye ukurasa 266 wa kitabu hiki. Mwaka jana zilikuwa milioni 72,196,000 na mwaka huu zimekuwa ni milioni 181,460,000. Idara ya Biashara mwaka jana ilikuwa milioni 172,237,000 na mwaka huu zimekuwa ni milioni 255,397,000. Hata Ofisi Kuu Pemba, mwaka jana zilikuwa milioni 163,407,000 mwaka huu ni milioni 238,400,000. Kwa hivyo, katika fungu hili la matumizi kwa jumla yake tu kunaonekana kumepanda kwa kiwango kikubwa sana.

Mhe. Naibu Spika, pia niseme kwamba hizi ni gharama za utawala, mishahara na mambo mengine. Sasa nitowe mifano mahususi. Mhe. Naibu Spika, nikiangalia fungu la safari, unakuta fungu la wizara hii linakuwa kubwa sana. Ofisi Kuu Pemba fungu la safari ni milioni 26,500,000 za ndani na za nje. Mipango Sera na Utafiti ni milioni 40. Viwanda ni milioni 56,600,000, biashara ni milioni 35,500,000 na Utawala na Uendeshaji ni milioni 59,000,000. Kwa jumla wizara hii katika fungu la safari za ndani na nje ni milioni 237,600. Kuna ongezeko kubwa sana ukilinganisha na mwaka uliopita.

Mhe. Naibu Spika, nitowe mfano mwengine, katika fungu la mshahara na hapa pia nimepata wasi wasi. Kwa sababu mishahara tulivyoambiwa kama kuna nyongeza basi nyongeza ingekuja katika lile fungu ambalo Wizara ya Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo inalihodhi na baadae ndio litakuja kugaiwa baada

ya kufanywa marekebisho. Lakini tayari kwa bajeti hii hivi sasa fungu la mishahara limeongezeka mno ukilinganisha na idara mbali mbali.

Nianze tena kuangalia mipango, sera na utafiti kwa mwaka jana ilikuwa ni milioni 272,281,000 na mwaka huu nikichanganya mipango, sera na utafiti na utawala na uendeshaji zinakuwa ni milioni 23, 573,000, ukenda Ofisi Kuu Pemba zilikuwa milioni 70,899,000 na mwaka huu ni milioni 91,774,000. Ukenda kwenye viwanda zilikuwa milioni 25,549,000 na mwaka huu ni milioni 43,062,000 na ukenda kwenye biashara zilikuwa milioni 81,315,000 na mwaka huu ni milioni 106,374,000.

Mhe. Naibu Spika, naendelea mfano mwengine ni kwenye posho maalum. Unakuta idara ya mipango sera na utafiti kwa mwaka jana ilikuwa ni milioni 81,925,000 na mwaka huu ukichanganya mipango sera na utafiti na utawala na uendeshaji ambayo ndio iliyochanganywa na kuwa pamoja, unakuta ni milioni 53,873,000. Mfano, wa mwisho Mhe. Naibu Spika, ni kwenye viburudishaji. Viburudishaji kwa mwaka jana zilikuwa ni milioni 2 katika idara ya mipango sera na utafiti na kwa mwaka huu nikichanganya idara hizi zimegawanywa katika idara mbili, mipango sera utafiti utawala na uendeshaji, kule kuna milioni 10 na huku kuna milioni 5,500,000 jumla ni milioni 15,500,000.

Sasa Mhe. Naibu Spika, najiuliza kwamba mbona ukitizama kasma mbali mbali kama nilivyosema kuna kupanda kwa kasi sana, viwango hivi mbali mbali vya matumizi katika fungu la utawala limeongezeka kiasi hiki. Nilikuwa naomba maelezo atakapokuja Mhe. Waziri anisaidie.

Mhe. Naibu Spika, baada ya kuhoji katika kitabu hiki kuhusu masuala haya ya vifungu mabli mbali naomba sasa nije katika hotuba ya Mhe. Waziri. Nitaomba univumilie kidogo kwa sababu ilibidi nitumie muda wangu katika vifungu. Kwa sababu kama

nilivyosema, panapokuwa na matatizo inabidi tupate maelezo ili turidhike wakati wa kuja kuvipitisha na iwe fedha za wananchi zinatumika vile inavyokusudiwa.

Mhe. Naibu Spika, nikija kaktika hotuba ya Mhe. Waziri naomba nianze katika suala zima alilotuelezea kuhusu hali ya biashara na akatuelezea ya kule ulimwenguni na baadae akaja Zanzibar akizungumzia urari wa biashara ulivyo.

Mhe. Naibu Spika, nchi inayofanya biashara vizuri ni ile ambayo kuna urari mzuri baina ya uagiziaji na usafirishaji. Akitizama mifano aliyotupa ya kutoka Marekani, Asia na Ulaya kuna ulinganifu kidogo, Afrika tuko nyuma. Lakini katika Afrika tunaonekana Zanzibar tuko nyuma zaidi Mhe. Naibu Spika.

Mhe. Naibu Spika, hali mbaya Zanzibar imeoneka katika urari wa biashara baina ya Zanzibar na Tanzania Bara na mwenyewe ametuonesha pale kwamba uagiziaji kutoka Bara kuja Zanzibar ulikuwa milioni 19,651,000 kwa mwaka 2009. mwaka 2010 umeongezeka umefika milioni 23,268,000. Lakini usafirishaji kutoka Zanzibar kwenda Bara, unazidi kushuka. Mwaka 2009 ulikuwa milioni 4,256,000 na mwaka jana 2010 umekuwa milioni 3,303,000.

Mhe. Naibu Spika, swali langu ni kuwa je, ni nini *factors* hali hii. Mhe. Waziri katika hotuba yake katuambia kwamba ni kuongezeka kwa mahitaji na kukua kwa utalii. Mimi najiuliza kwa upande mwengine ni kiasi gani sera za kodi zinachangia hili. Sera za kodi upande wa pili na uzalishaji kwa upande wa Zanzibar. Mhe. Naibu Spika, naomba nianze na suala hili la kodi.

Mhe. Waziri katika hotuba yake mwenyewe kakiri katika ukurasa wa 10 pale kwamba kuna hili tatizo la kutozwa kodi mara mbili kwa bidhaa zinazopitia Zanzibar zikenda Bara. Lakini nilichosikitika katika hotuba yake kwenye ukurasa ule wa 10

kaielezea hali na akatuambia kwamba imejadiliwa katika kamati inayozungumzia kero za Muungano. Halafu akatuambia kuwa linajaribiwa kumalizwa kwa TRA kuanzisha hiki kitu kinachoitwa *import valuation data base*.

Mhe. Naibu Spika, mwisho alituambia kwamba wizara inafuatilia utekeleza wa utaratibu huo mpya ili kuweza kutoa taarifa hapo baadae. Hili suala tulivyoambiwa Mhe. Naibu Spika, humu ndani ya Baraza ni kwamba suala hili limemalizwa, imeshakubaliwa kwamba kusiwepo kodi mara mbili. Sasa yeye mwenyewe kakiri kwamba inaendelea na wafanyabiashara wetu jambo hili linawaumiza sana. Pia linachangia kwa kiasi kikubwa huu urari wa biashara huwa hauko sawa yaani hauna mizania. Kwa sababu ukitoa biashara Bara ukileta hapa hakuna mara mbili, kwa hivyo ni rahisi kuuteremsha kule mzigo na kuuleta hapa. Kwa hivyo, uagiziaji kutoka Bara utaongezeka. Lakini ukiutoa Zanzibar kuupeleka Bara unatozwa mara mbili. Kwa hivyo, kwa vyovyote utaangusha au uta-*discourage* ile hali nzima ya wafanyabiashara wa Zanzibar kupeleka bidhaa Bara. Katika hili Mhe. Naibu Spika, nilikuwa namuomba Mhe. Waziri anisaidie.

Mhe. Naibu Spika, kwa hapa nilikuwa naomba pia serikali kwa jumla ituambie, kwamba tume-*harmonize* kodi na ushuru, matokeo yake yanatuathiri kiasi hiki. Lakini je, suala hili ni halali ukizingatia kwamba mbona kipato chetu hakilingani. Maana yake kama tunazungumzia kuweka ulinganifu wa kodi baina ya Zanzibar na Bara, basi iwe kuna na ulinganifu wa kipato baina ya Bara na Zanzibar.

Lakini sote Mhe. Naibu Spika, ni mashahiti kwamba Zanzibar kipato cha wananchi wetu ni kidogo na hata mishahara yetu ni midogo. Sasa ni sawa au ni haki kwa watu kama hawa kuwekewa viwango sawa, hasa tukizingatia uchumi wetu unategemea Mhe. Naibu Spika, biashara ya mpito. Nilikuwa naomba suala hili anisaidie.

Hapo hapo Mhe. Naibu Spika, niseme jengine ambalo nadhani linachangia urari wa biashara kuwa hauko sawa ni kwa sababu Zanzibar hakuna uzalishaji. Sasa mimi najiuliza katika muhtadha mwengine, muhtadha wa hili soko la pamoja la Afrika ya Mashariki, kwamba ikiwa hatuzalishi humu ndani kwa hivyo, inaathiri pakubwa urari wa biashara baina ya Zanzibar na Bara. Je, tutakapoingizwa katika soko la pamoja sisi hatutogeuzwa soko la bidhaa la wengine, lanini sisi hatuna cha kupeleka katika hilo soko la pamoja la Afrika ya Mashariki. Kwa hivyo, Mhe. Naibu Spika, naomba suala hili Mhe. Waziri akija anisaidie sana kunipa maelezo.

Mhe. Naibu Spika, naomba nizungumzie suala zima la upandaji wa bei za bidhaa. Katika ukurasa wa 14 wa hotuba ya Mhe. Waziri katuelezea *factors* zilizopelekea bidhaa kupanda duniani. Mwenyewe Mhe. Waziri katika jadweli nambari 6 ambayo inaelezea bei kupanda duniani, akilinganisha na jadweli nambari 7(a) na 7(b), lile ongezeko la duniani kwa asilimia halilingani na Zanzibar. Duniani mchele umepanda kwa asilimia 7.3, lakini Zanzibar kwa reja reja umepanda kwa asilimia 20.24. Samahani kwa jumla na kwa reja reja kwa asilimia 20. Sukari duniani imepanda kwa asilimia 18.4, lakini Zanzibar imepanda kwa asilimia 27.6 kwa jumla na kwa reja reja kwa asilimia 38.46.

Mhe. Waziri kasema katika ukurasa wa 16, kuna suala la wafanyabiashara ambao wanatumia hizi mbinu tatu alizozitaja katika ukurasa wa 16, sina haja ya kuzirejea. Mhe. Hija Hassan katika mchango wake kasema hapa kwamba wapo wafanyabiashara wazalendo ambao wanakusudia kuleta bidhaa kwa bei ya chini ili kuwanufaisha wananchi, lakini kumekuwa na huu mchezo mchafu ulioripotiwa katika gazeti la Zanzibar Leo na Mhe. Waziri aliwahi kutamka hadharani kwamba kuna watu wametishiwa mpaka wametekwa nyara. Kwa hivyo, nilikuwa namuomba Mhe. Waziri katika hili aje atusaidie.

Mhe. Waziri, wizara yake, suala hili kwanza hakulitolea kauli katika hotuba yake, lakini Wizara yake ina mpango gani wa kuwalinda hawa na kulinda ushindani uliosawa, ili watu kama hawa waliokusudia kuwasaidia wananchi, wasije wakaathirika.

Mhe. Naibu Spika, hapo hapo katika bidhaa Mhe. Waziri katuambia kwamba unga wa ngano haikupanda bei kwa sababu kuna uzalishaji wa ndani hasa akimaanisha kwamba inatoka Bara. Najua kwamba Bara hawazalishi ngano, lakini huagizia ngano pale wao wakatengeneza unga wa ngano. Nikitizama lile jadweli la 4 linaonesha kwamba unga wa ngano Zanzibar uzalishaji ni ziro, lakini katika ukurasa wa 77 wa kitabu chake, katika viwanda ambavyo vimefanyiwa tathmini hapa kuna Kiwanda cha *Zanzibar Milling Cooperation* na katika bidhaa, imeandikwa unga wa ngano na unga wa mahindi. Kwa hivyo, naomba nisaidiwe suala hili, kwamba hiki kiwanda kwa nini hakizalishi hapa Zanzibar na tumeambiwa bidhaa zake ni hizo na kama hakizalishi ni kwa sababu gani zilizopelekea kukwama na wizara ina mpango gani wa kuzikwamua sababu kama hizo.

Mhe. Naibu Spika, niipongeze wizara katika upande wa biashara kwa hatua yake ya kuja na mpango wa kuanzisha maonesho ya biashara ya kimataifa hapa Zanzibar. Vile vile mpango wake wa kuanzisha *Sunday Market*. Nampongeza sana na naamini itasaidia sana kuitangaza Zanzibar. Jina la Zanzibar tu peke yake Mhe. Naibu Spika, linajiuza, kwa hivyo tukiweka maoneshao hapa basi mimi naamini tunaweza tukaifungulia Zanzibar milango zaidi na kuwa kituo cha biashara.

Mhe. Naibu Spika, vile vile katika biashara nipate maelezo kwenye ukurasa wa 37 katika kitabu cha Mhe. Waziri kuhusu suala la viwango hili na akatuambia kwamba bidhaa zote ambazo zimeharibiwa ambazo zilikuwa chini ya kiwango ni bidhaa zenye thamani ya bilioni 5.5. Mhe. Naibu Spika, mimi hapa kidogo

nimepata wasi wasi, hebu Mhe. Waziri atusaidie hakuna mchezo mchafu hapa kati ya wafanyabiashara hapa na watendaji wa wizara yake. Hivyo kweli bidhaa zilizoingia za chini ya kiwango kwa Zanzibar ni za bilioni 5.5 tu. Bahati mbaya muda ulikuwa mfupi sikujitayarisha, lakini nakumbuka wakati fulani Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais kupitia idara ya mazingira ilitoa, nakumbuka waziri Mhe. Fatma alitoa *figures* kwamba bidhaa za hii *west* peke yake zilikuwa ni nyingi mno zinazoingia Zanzibar na thamani yake ilitajwa wakati ule. Sasa tunapoambiwa kwa mwaka mzima bidhaa zilizoharibiwa ni za bilioni 5.5 tu, inatia mashaka sana. Je, wananchi wetu hakuna mchezo hapa wa kuziruhusu biashara nyengine ziendelee na kuweza kuendelea kuathiri afya za wananchi wetu. Nilikuwa naomba hilo tusaidiwe. Kwa sababu mimi Mhe. Naibu Spika, naamini bidhaa zinazoingia za chini ya kiwango bila shaka ni chini ya milioni 5.5 kwa mwaka uliopita. Hapo hapo nimpongeze waziri kwa hii hatua ya kuja na kifaa cha kuchunguza uchakachuaji wa mafuta kwenye ukurasa wa 37 katika hotuba yake Mhe. Waziri.

Mhe. Naibu Spika, mimi nadhani asiishie hapo, lakini suala zima la kudhibiti bei ambalo kalitaja katika ukurasa wa 38 wa hotuba yake, nafurahi leo katuletea kanuni zinazotuelekeza huko. Mhe. Naibu Spika, nadhani ni muhimu Mhe. Waziri alifanyie kazi haraka sana, kwa sababu kama nilivyosema hata kule kwenye bidhaa za vyakula ukitizama ule mlinganisho wa dhamani ya kupanda kwa bei duniani na hapa Zanzibar haulingani. Kwa hivyo, bila shaka kama alivyotueleza mwenyewe, kwamba kuna wafanyabiashara ambao hawapendi wananchi wetu wanawaathiri sana. Naomba katika suala hili asimamie haraka sana ili wananchi wetu wasiendele kuathirika, hasa kwa sababu mwezi wa Ramadhan unakuja na hiki ndio kipindi ambapo wananchi wengi tungetegemea wapate nafuu, lakini mara nyingi ndipo wanapokomolewa katika kipindikama hiki. Kwa hivyo, Mhe. Naibu Spika, naomba hilo pia anipe maelezo.

Mhe. Naibu Spika, nije kwa ufupi kabisa katika suala la viwanda. Katika hotuba yake Mhe. Waziri suala la viwanda kaitaja UNIDO. Moja katika maeneo ambayo mwenyewe kasema kwamba tumekuwa nyuma sana ni suala zima la kuanzisha viwanda na watu wetu wengi wameongezeka uwezo wao kimtaji, lakini wameishia katika biashara ile ile ya kuleta bidhaa kutoka nje wakauza, wanashindwa ule ujasiri wa kuingia katika kuanzisha viwanda. Sasa kwa kule Bara wenzetu wanayo *SIDO* ambayo inawasaidia sana wafanyabiashara, wale wanaotaka kuwekeza katika viwanda kuwasaidia ujuzi, kuwasaidia mitaji, na vitu vyengine kama hivyo na hata kupewa utaalamu kwa kupitia *SIDO*.

Mhe. Naibu Spika, wabunge wa Zanzibar mara nyingi waliwahi kuhoji kwamba kwa nini *SIDO* haitowi mafunzo kwa Zanzibar. Lakini jawabu ambalo walikuwa wanazipata ni kwamba masuala ya viwanda sio masuala ya Muungano na mimi nakubaliana na hilo. Kwa hivyo, nilikuwa nataka kumuuliza waziri haoni kwamba kuna haja ya kuanzisha taasisi pengine inayolingana na *SIDO* kwa upande wa Zanzibar, ili kwa kushirikiana na *UNIDO* waweze kuwasaidia wafanyabiashara wetu waweze kuwa na nguvu ya kujiingiza katika masuala haya ya viwanda.

Mhe. Naibu Spika, katika ukurasa wa 40 kwenye kitabu chake Mhe. Waziri ametaja mambo mengi ambayo yanawakwaza wafanyabiashara wetu wa Zanzibar, ili wasiweze kujiingiza katika kukwazisha viwanda. Nilikuwa nadhani mimi wizara yake ifanyekazi ya kuwasaidia hawa wafanyabiashara kuwapa *confidence*, kuwapa elimu, kuwapa maarifa na kuwapa *exposure* ya jinsi mambo haya yanavyofanyakazi nje, ili wafanyebiashara wetu waliokuwa wamenyanyuka kidogo waweze kutoka katika biashara ile ya kuleta bidhaa na kuuza tu, lakini waingie pia katika utayarishaji wa viwanda.

Mhe. Naibu Spika, mwisho kabisa nilikuwa naomba katika suala zima la kuweka mazingira mazuri ya biashara Mhe. Waziri aliangalie suala zima la utitiri wa gharama za leseni. Katika ripoti ya CAG Mhe. Naibu Spika, ukurasa wa 12, amezungumzia kwamba naomba nimnukuu.

> "kuwepo taasisi nyingi zinazotoa leseni za biashara, ukaguzi umebaini kwamba Zanzibar kuna taasisi nyingi zimepewa mamlaka ya kukusanya mapato ya leseni kulingana na shughuli za sekta husika. Kwa mfano, Kamisheni ya Utalii, *ZIPA*, Baraza la Manispaa, Idara ya Habari na Halmashauri za Wilaya. Hali hii inasababisha baadhi ya walipa leseni kukwepa kukata leseni kutokana na mgongano wa sheria za leseni kwa taasisi hizo. Vile vile hali hiyo inasababisha serikali kushindwa kudhibiti na kuweka kumbukumbu za wakata leseni za biashara katika sekta mbali mbali zilizopewa mamlaka ya kukusanya mapato yanayotokana na shughuli zao".

Mhe. Naibu Spika, mimi nadhani kuepusha hili ni kuongeza serikali upande mmoja kukusanya zaidi, lakini pia kuwapunguzia usumbufu wafanyabiashara kuwe na utaratibu wa ku-*synchronize* ili utoaji wa leseni uweze kuwa unawavutia watu kuendesha biashara vizuri zaidi.

Mhe. Naibu Spikia, baada ya kusema hayo kama nilivyosema mimi na kwa niaba yangu na kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Mji Mkongwe, naiunga mkono hotuba hii, lakini nitamuomba waziri akija anisaidie maelezo katika mambo hayo ambayo nimeyaibua. Nakushukuru sana Mhe. Naibu Spika, kwa kunivumilia, ahsante sana.

Mhe. Mohammed Haji Khalid: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, kwa jioni hii na mimi kupata nafasi ya kutoa machache niliyonayo. Mhe. Naibu Spika, kabla ya kutoa machache yangu

niliyonayo, kwanza nifanye marekebisho madogo kwenye jina langu. Mimi naitwa Mohammed Haji Khalid, sio Mahmoud.

Mhe. Naibu Spika, nianze sasa kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa jioni hii kuniwezesha kusimama hapa kutoa mawazo yangu kwenye bajeti hii ya Wizara ya Bishara, Viwanda na Masoko.

Pili nikushukuru na wewe Mhe. Naibu Spika, kwa kunipa nafasi hii na hatimaye nimshukuru waziri kwa kuwasilisha kwake bajeti hii. Lakini Mhe. Naibu Spika, nianze kwa kusema hivi, ni kawaida kwa mwanadamu kutarajia mema hata kama ishara ya mema hayo haipo. Mhe. Naibu Spika, kwenye bajeti hii wengi wetu tunatarajia mambo mazuri na wema. Lakini kwa mtizamo wangu nilipoiona hii kwa kweli matarajio ya mambo mema inaonesha kuwa hayapo.

Mhe. Naibu Spika, nasema hivyo kwa sababu gani. Kwa sababu nimetazama katika usafirishaji wa bidhaa kwenda nje huu unashuka mwaka hadi mwaka. Katika mwaka 2008 thamani ya pesa tulizopata ni 30.1 milioni, mwaka 2009 ni 29 na kidogo na mwaka 2010 ni 17. Kwa hivyo kiwango cha pesa tunazopata kwa kusafirisha zinashuka mwaka hadi mwaka. Lakini kiwango cha pesa tunazoziagizia kupeleka nje zinapanda nazo mwaka hadi mwaka. Kwa hivyo, sisi fedha za kuingiza ndani zinapungua, lakini fedha za kutoa nje zinaongezeka mwaka hadi mwaka. Kwa hivyo, hapa zinaonesha kwamba bidhaa tunazosafirisha zinapungua kwa kima kikubwa na zile tunazoagizia zinaongezeka mno. Hivyo fedha nyingi inatoka na kidogo tu ndio inayoingia, hapa hapajakuwa na tegemeo la kibiashara, kwa sababu tunatoa zaidi na sisi tunapata kidogo.

Mhe. Naibu Spika, ingawa zao la karafuu limetajwa kuwa linachangia kwa asilimia kubwa, lakini na kuzalisha kwake kunapungua kwa kima kikubwa. Hivi sasa asilimia kubwa ya

karafuu zetu zinakwenda nje ya Zanzibar, kuna nchi jirani inajipatia zaidi kuliko sisi wenyewe. Hii inatokana na nini. Inatokana na bei ndogo iliopo ya karafuu hapa nchini kwetu. Juzi serikali ilipojaribu kujitutumua kidogo, nizungumze kwa lugha ya kule kwetu, watu hawazungumzi kwa kilo, wanazungumza kwa pishi. Serikali imesema kuwa itanunua pishi moja ya karafuu kwa Shs. 15,000, watu wanachukulia bei ya mwanzo tu. Lakini watu wa magendo na wao wamepandisha wananunua baina ya Shs.14,000 hadi Shs. 20,000 kwa pishi, kwa hivyo wametupita. Kwa sababu sio nyingi kama inavyosemekana, kwa sababu karafuu ziko lakini sio nyingi kama inavyoonekana kuwa Pemba ziko karafuu, ziko kwa wastani.

Mhe. Naibu Spika, kwa sababu sio nyingi sana basi imani yangu serikali itashindwa na walanguzi kwa bei hii na karafuu zitaendelea kutoka nje ya Zanzibar na kwenda nchi jirani. Pamoja na kuwa serikali imetangaza mikakati mikubwa ya kuzilinda karafuu zisitoke nje, lakini kwa kuwa mwanadamu sikuzote anatarajia kupata zaidi na watu pia wataongeza mbinu ya kuzisafirisha. Sasa serikali imeamua kuwa itaongeza ulinzi kabambe, lakini ningeomba kwamba huu ulinzi utakaokuwepo usije kuvuka mipaka ikasababisha pengine hata hawa watu ambao sio raia wema, kwa sababu wanazisafirisha karafuu, lakini isije kusababisha kupoteza maisha yao kama ilivyokwisha kutokezea mara nyengine huko nyuma.

Mhe. Naibu Spika, tunazungumzia viwanda. Mwishoni mwa miaka ya 1970 au mwishoni mwa miaka ya 1960 tulikuwa navyo viwanda vingi vidogo vidogo vidogo hapa Zanzibar kikiwemo kiwanda cha viatu, kiwanda cha sigara, kiwanda cha maziwa na vyenginevyo. Lakini hatimaye kama vilivyojengwa na ndivyo vilivyopotea. Nadhani kwenye kuanzisha hivi viwanda hakukufanywa utafiti juu ya viwanda, kwa sababu kuanzisha kiwanda cha aina yoyote kuna masharti yake.

Kwanza kupatikana kwa mali ghafi. Kwa mfano tukifungua kiwanda cha viatu na tukitengeneza viatu vya ngozi, hatukufanya utafiti ngozi hii tutaipata wapi. Kiwanda kinahitaji tuwe na soko la hicho tutakachozalisha, hatukutafuta soko la viatu vyetu litakuwa wapi, jambo tutakalokuwa nalo ni *cheap labor*, kwa sababu wafanyakazi tulikuwa tunao, lakini tulikuwa hatuna soko, hatuna mali ghafi. Kwa sababu mali ghafi tunanunua nap engine kwa bei kubwa, tunachozalisha tunakiuza ndani, kiwanda hicho bila shaka itakuwa hakuna faida inayopatikana na hatimaye vilikufa kama vilivyoanzishwa.

Mhe. Naibu Spika, kuhusu kiwanda cha sigara, tumbatu inatoka Tanzania Bara tunaagizia, sigara ya Zanzibar Zaraha na Zakuchuja ilikuwa mwisho ni Makoongwe kuvutwa, yaani hazivuki ng'ambo ya pili ya Jamhuri. Kwa hivyo, ilikuwa hakuna msunguuko wa bidhaa hii kwa hivyo, viwanda vikafa. Sasa leo tuna lugha ya viwanda je tumefanya utafiti kuwa tunaweza kumudu viwanda. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, ndio maana nikasema ni kawaida ya mwanadamu kutegemea mema hata kama ishara ya mema hayo haipo. Kwa kweli hapa Mhe. Naibu Spika, haya yote yanayopangwa ishara ya kufanikiwa ni finyu mno. *(Makofi)*

Kwa kweli sisi wenyewe hatuna uwezo na tunategemea kubebwa na ubeleko ukichanika tutaanguka, kwa sababu sisi hatuna uzalishaji. Kwa hivyo, Mhe. Naibu Spika, ningeomba wizara hii haya mambo yote waliyopanga *base* yetu ni nini hata tukawa na matumaini kwamba tutakwamuka. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, bado bidhaa nyingi zinazoagiziwa, yaani zinazoingia nchini hazina viwango, hata hizi simu tunazotumia nyingi ni *fake*. Kwa mfano, nilipoondoka hapa kuna dereva wangu aliniambia Mheshimiwa nilitee simu, basi juzi naambiwa ile simu

imeshakufa, shida yangu kwamba simu imeshakufa tena nimeinunua mpya dukani. *(Makofi)*

Kwa hivyo, bado wafanyabiashara wetu kwa kiasi fulani wanachukua zile bidhaa ambazo huko kwao hazina soko tena na kuja Zanzibar kama ndio jaa la vifaa ambavyo havina thamani.

Mhe. Naibu Spika, wizara hii niseme Kipemba itabidi ifunge kibwebwe, kuhakikiksha kuwa Wazanzibari tunapata vitu vyenye viwango vya dunia ilivyo, kwa sababu sisi ni watu wa visiwa, lakini na sisi ni watu. Kwa hiyo, wafanyabiashara wetu wajitahidi kuona kwamba hawa Wazanzibari na wao ndio, tena wala si watu ni jaa kuwa tukaotokea tuje tuwatupee tu.

Kwa kweli bidhaa nyingi zipo za aina hii. Sasa sijui kama kuna utatifi au uhakika wowote kwamba bidhaa hizi zinapoingia kuwa wizara yako inazishughulikia au laa, kwa sababu mtu ameleta ndio basi.

Mhe. Naibu Spika: Mhe. Mjumbe, zimebakia dakika tano.

Mhe. Mohammed Haji Khalid: *Hewallah*. Mhe. Naibu Spika, bei za vyakula na mafuta ya kupikia na mimi sitaki kuyaita mafuta ya kula, kwa sababu mafuta hayaliwi ni kukiharibu Kiswahili. Kwa kweli kuna siku mtu atasema maji ya kula. *(Kicheko/Makofi)*

Bei za vyakula na mafuta bado zinapanda siku hadi siku, watu wanaouziwa uchumi unadizi kwenda chini siku hadi siku. Kwa hivyo, bei zinapanda, lakini mnunuzi hana uwezo. Mhe. Naibu Spika, biashara za zamani ilikuwa ni tofauti na za leo. Kwa mfano, zamani mfanyabiashara basi biashara ikizidi siku fulani ilikuwa anaiuza kwa bei pungufu na leo hakuna *discount* ya biashara, unataka utanunua kwa bei hiyo ambayo amekishwa kupanga, ikiwa hutaki basi ni hiyari yako.

Kutokana na hali hiyo, ndio maana vitu vinakaa mpaka vinapitwa na wakati, kwa sababu tu wafanyabiashara mara nyengine hawataki kuteremsha bei ili ile biashara inaondoka.

Mhe. Naibu Spika, naiomba Wizara hii ya Biashara, Viwanda na Masoko ambayo kwa upande mmoja inahusiana na bidhaa ambazo zinaliwa, hivyo ihakikishe kuwa bidhaa za vyakula zinazoingia nchini zinakuwa na viwango. Kwa kweli watu wengi wenye kensa ni Wazanzibari na sina hakika, lakini kwa bahari za mitaani wanasema mambo haya yanatokana na vyakula vibovu tunavyokula. *(Makofi)*

Kwa hivyo, ningeiomba wizara hii iwe ni mkombozi wa Wazanzibari, ikae na wafanyabiashara kwa huruma kabisa waone kuwa tunawahudumia wenzetu na wao muwafanyie milango yao ya biashara ifunguke. Kwa mfano, kaka yetu mlango ameufunga, basi jamani serikali mlango usukumeni, ili ufunguke. *(Makofi)*

Kwa kweli miaka ya karibuni watu walikuwa wakitoka Bara kwa ajili ya kuchukua bidhaa kama vile vitambaa pamoja na mambo mengine hapa Zanzibar, lakini leo *no body comes*, kwa nini kwa sababu kuna mtu mlango ameukomea na sisi nadhani hatuna ufunguo wa kufungulia. Mhe. Naibu Spika, kama hatukupata ufunguo, basi biashara Zanzibar itadidimia siku hadi siku.

Baada ya hayo, na kuwa kuwa Mhe. Naibu Spika umeshaniambia muda umemalizika, basi naunga mkono hoja. *(Makofi)*

Mhe. Ashura Sharif Ali: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika. Awali ya yote sina budi kumshukuru Mwenyezi Mungu Mtukufu *Subuhanahu Wataala*, aliyetujaalia uhai na uzima jioni hii tukawepo hapa kwa ajili ya kutekeleza majukumu yetu kwa maslahi ya taifa letu.

Mhe. Naibu Spika, sina budi pia nikupongeze na wewe nami kunipatia nafasi hii kwa jioni ya leo. *(Makofi)*

Vile vile sina budi nimpongeze Mhe. Waziri kwa hotuba yake jinsi ilivyokamilika pamoja na vile alivyoisoma na kuiwasisha kwetu. Mhe. Naibu Spika, pia nimpongeze Mhe. Naibu Waziri jinsi alivyokuwa makini kwa ajili ya kujibu maswali hapa Barazani. Kwa kweli sote ni mashuhuda kwamba mwanamke huyu alikuwa mahiri sana. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, nichukue fursa hii kwa kuwapongeza watendaji wote wa wizara hii. *(Makofi)*

Baada ya utanguliza wangu huo sasa nianze mchango wangu moja kwa moja kwa vile muda wenyewe ni mdogo, basi nianzie kwenye ukurasa wa 7 kuhusu hali ya biashara Zanzibar.

Mhe. Naibu Spika, ninayo imani kwamba wengi kati ya Wazanzibar wana historia kuwa Zanzibar ni Kitovu cha Biashara. Suala hili linakumbukwa sana kwamba hapa kwetu palikuwa ndio Kitovu cha Biashara na hiyo ndio historia ya nchi yetu. Hivyo, nina imani kwamba Mhe. Waziri wakati alipokuwa akipanga mipango yake ya bajeti pamoja na utekelezaji, basi alijuwa wazi kuwa anataka kuirejesha hadhi ya Zanzibar kibiashara. *(Makofi)*

Wazanzibari wamejenga matumaini makubwa katika wizara yako hii. Mhe. Naibu Spika, nasema hususani wanawake nao wamejenga matumaini makubwa katika mpango wako huu, ambapo hotuba yako umeisoma jana na tumepata vi-*memo* vingi vinavyogusa wizara hii jinsi ilivyojipanga. Mhe. Naibu Spika, hivyo naiomba Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko isimamie kwa kina utaratibu mzima unaohusiana na biashara kwa ajili ya maendeleo ya taifa hili, kwa vile Wazanzibari tuna historia ya biashara. *(Makofi)*

Nikiendelea na mchango wangu sasa niende kwenye ukurasa wa 10 kifungu cha 19 kuhusu uendeshaji wetu wa biashara baina ya Tanzania Bara na Visiwani. Mhe. Naibu Spika, kwa masikitiko makubwa sana Wazanzibari wanasikitishwa mno na hali hii ya wafanyabiashara za Zanzibar kulipishwa ushuru mara mbili. *(Makofi)*

Kwa kweli hali hii imekuwa ni ngumu mno na inaleta adha kwa Wazanzibari, yaani imekuwa ni kero kubwa na inatuletea bughudha, fitina na sisi wenyewe kutokujielewa ni ipi hasa bei ya kutangazwa kwa uhalisi, ili wananchi wakaweza kufaidika na biashara hizo zinazoletwa na wafanyabiashara wa Zanzibar. *(Makofi)*

Kutokana na hali hii tunaiomba Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko kutuelewa wazi wazi, kuna sababu zipi za msingi zinazopelekea wafanyabiashara wetu walipe ushuru mara mbili. Mhe. Naibu Spika, kwa sababu sisi ni taifa kama walivyowenzetu, tumeunga ubia wa biashara kwa ajili ya mapenzi na kufanyabiashara kwa pamoja kwa maslahi ya taifa hili la Tanzania na wao ni Bara na sisi Visiwani na hayo ndio malengo makuu. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, kama hivyo ndivyo, basi wizara ituambie ni lini hasa adha hii itawaondokea wafanyabiashara na Wazanzibari waweze kuondokana na hali hii? Suala hili Mhe. Naibu Spika, namuachia Mhe. Waziri, ili awajibu Wazanzibari akiwa yeye ni sehemu ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, kwa ajili ya kuona wapi sasa tunasimama wafanyabiashara. *(Makofi)*

Sasa nizungumzie suala la kuhusu wafanyabiasara wa Makontena Darajani. Mhe. Naibu Spika, hali ya biashara ya wafanyabiashara wa Makontena ilileta adha na udhia mkubwa na kuweza kufikia mahala ikawa kwetu ni kero na adha pamoja na kulikosesha mapato taifa na hadi wafanyabiashara kuwapelekea hasara.

Hivyo, naamini kwamba endapo Mhe. Waziri atachukua hatua za makusudi, kwa ajili ya kuwaendeleza wafanyabiashara hao na kuona kwamba eneo hili sasa tunataka tuliboreshe kwa kushirikiana na wafanyabiashara hao kwa kuwajengea maduka ya kisasa yatakayoweza kuipa haiba mji wetu na kuonesha kweli Zanzibar ni ya biashara. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, hali ilivyo sasa si nzuri na wala haivutii, lakini ipo haja katika wizara yako kukaa na wafanyabiashara hawa, ili kujenga maduka ya kisasa kabisa yanayokwenda na wakati wa leo pamoja na kiushindani wa kibiashara. *(Makofi)*

Kwa kweli wageni wengi wanaokuja nchi kwetu huwa wanavutiwa mno na biashara zetu, pia wanavutiwa mno na imani pamoja na utulivu wa nchi hii katika shughuli hizi. Kwa maana hiyo, wageni wengi wanapokuja hapa basi huona raha zaidi kuona utaratibu wa biashara, lakini hali sivyo ilivyo sasa. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, niseme kidogo kwamba huku nyuma ilifikia hadi wafanyabiashara kufungiwa bure maduka yao hali ambayo iliikosesha mapato taifa letu, kwani uchumi wetu au pato la taifa kwa asilimia kubwa wanatuchangia wafanyabiashara wetu na hii ni dhahiri hakuna asiyetambua hilo. *(Makofi)*

Nadhani tujiulize kidogo, hivi kuna sababu zipi za msingi ambazo zilipelekea kuweza kutokea hali ile. Mhe. Naibu Spika, kwa kuwa tayari imeshatokea wafanyabiashara walipata harasa kubwa na tuliwahi kuwatembelea na kuwauliza na hatimaye walifika Mahakamani na kesi walishinda, kwa sababu siku zote haki huwa haizami. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, hali hii si nzuri kutokea kwa Zanzibar mpya yenye sura ya Umoja wa Kitaifa. Hivyo, ikiwa tunahitaji maendeleo ya kweli basi lazima tubadilike na tuwe na utaratibu

mzima wa kufuatilia masuala yetu kwa ajili ya shughuli za maendeleo kwa Wazanzibari. *(Makofi)*

Kwa hiyo, kama tunahitaji maendeleo ya kweli basi lazima tupange sera, mipango pamoja na utaratibu madhubuti wa kuweza kuliongoza taifa letu na kufikia maendeleo ya kweli na kuwaondoshea wananchi umasikini na kero kubwa iliyotukabili ya umasikini uliokithiri. *(Makofi)*

Kutokana na hali hiyo, Mhe. Waziri lazima akae na wafanyabiashara asiwapoteze imani, ili uzalendo wao utusaidie katika hali hii ngumu tuliyonayo. Kwa kweli Wazanzibari si wakaidi ni watu wenye imani na mapenzi makubwa kwa taifa lako, lakini kulikoni. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, namuomba Mhe. Waziri suala hili aliangalie kwa jicho la huruma kabisa, kwa sababu mimi niwaamini sana Wazanzibari kwamba sisi tunauthamini sana umoja wetu. Sambamba na juhudi zilizochukuliwa na viongozi wetu wawili Mhe. Rais wetu Mstaafu wa Zanzibar wa Awamu ya Sita ambaye alileta Serikali ya Umoja wa Kitaifa pamoja na Maalim Seif Sharif Hamad, basi sisi tuna haja ya kulinda na kusimamia na kuona kwamba sasa tumezaa Zanzibar mpya ambayo wananchi wake wataishi kwa amani, utulivu pamoja na maendeleo ya kweli. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika: Mhe. Mjumbe, malizia muda umekwisha.

Mhe. Ashura Sharif Ali: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika.

Baada ya kusema hayo, kwa niaba ya wanawake wa Wilaya ya Kaskazini ‘B’ naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika: Waheshimiwa Wajumbe, nawashukuru kwa michango yao. Lakini bado tunao wachangiaji *backbencher* wanne pamoja na mawaziri wawili na tunategemea kesho asubuhi tumalize bajeti hii, ili jioni aje Mhe. Waziri mwengine. Kwa hivyo, wale ambao hawajatajwa waje mapema waweze kupata nafasi hizo.

(Saa 1:45 usiku Baraza liliahirishwa hadi tarehe 27/07/2011 saa 3:00 asubuhi)